Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 24 Juni, 2014

(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anna S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza Maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu, atakayeuliza swali la kwanza Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha.

Na. 293

Tatizo la Uchafu Katika Jiji la Dar es Salaam

MHE. MARYAM S. MSABAHA aliuliza:-

Jiji la Dar es Salaam linaongoza kwa uchafu na ombaomba, jambo ambalo linasababisha kero kwa wakazi wake na wageni wanaofika nchini.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kumaliza tatizo la ukusanyaji wa taka katika Jiji hilo?

(b) Je, Serikali inasema nini katika kutumia taka kutengeneza vitu vingine kama mbolea au kutumia taka hizo kufua umeme kama zinavyofanya nchi nyingine?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, changamoto inayolikabili Jiji la Dar es Salaam kuhusu usafi ni kuwepo kwa kiwango kikubwa cha uzalishaji wa taka ikilinganishwa na uwezo wa Jiji kuzoa taka hizo. Uzalishaji wa taka katika Jiji kwa sasa ni wastani wa tani 4,252 kwa siku wakati uwezo uliopo wa kuzoa taka ni wastani wa tani 2,126 kiasi cha 50% kwa siku.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hii Jiji limetumia shilingi bilioni moja (bilioni 1) kwa ajili ya kununulia mtambo mpya wa kusukuma taka, yaani *Buldozer D.8,* ununuzi wa malori mawili yenye tani 18 kwa ajili ya kuzoa taka na ununuzi wa *Compactor* moja kwa ajili ya kushindilia taka. Aidha, Jiji limeweka umeme ndani ya *Dampo*, ili *Dampo* liweze kupokea taka kwa saa 24.

Vile vile Mkoa umepitisha azimio kuwa, kila siku ya Jumamosi kutakuwa na shughuli ya usafi katika maeneo yote ya Jiji. Kila mtaa wamepewa jukumu la kusimamia usafi katika mtaa wao. Mkoa, Halmashauri na Kata kazi yao ni usimamizi na kukagua usafi kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepiga marufuku shughuli zote zinazofanyika kinyume cha Sheria katikati ya Jiji, zikiwemo biashara ya nguo barabarani, uchomaji wa mikishikaki, mahindi, Mama na baba-lishe, kupika kandokando ya barabara na mikokoteni. Vilevile Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ilifanya ukaguzi wa shughuli za usafi katika Halmashauri zote za Jiji na kuchukua hatua kwa Watendaji wa Mitaa na Maafisa Afya walioshindwa kusimamia usafi.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumia taka kwa ajili ya kutengeneza mbolea na umeme, tayari Makampuni 25 yameonesha nia ya kuwekeza katika miradi hiyo, yakiwemo makampuni 9 ambayo yatatengeneza mbolea ya mboji, Makampuni 12 kufua umeme na Makampuni 4 kutengeneza vitu mbalimbali, kama kwa mfano *Diesel* au *Ethanol.* Hatua iliyofikiwa hadi sasa ni uchambuzi wa uwezo na mashrti ya Makampuni hayo kuwekeza katika Miradi hiyo. *(Makofi)*

MHE. MARYAM S. MSABAHA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimwulize Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tulishuhudia tulipopata ugeni wa Rais Obama kutoka Marekani, Jiji la Dar es Salaam lilikuwa katika hali ya usafi, mgeni huyu alipoondoka Jiji lile lilirudi katika hali ya uchafu. Kipindi cha mvua makaro yote ya Dar es Salaam yanakuwa yanafumuka, vinatapakaa vinyesi na kusababisha milipuko ya maradhi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri anijibu swali hili. Ni mikakati gani ya Serikali ambayo ni ya kudhibiti hali hii ya makaro ambayo yanafumuka Dar es Salaam na kuurudisha Mji wa Dar es Salaam kuwa katika hali ya usafi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kila binadamu katika Tanzania hii ana haki katika Serikali yake, tunashuhudia ongezeko la omba omba, watu ambao wanaishi katika mazingira magumu na hata wageni wanapofika katika Jiji la Dar es Salaam wanakuwa wanawakera wageni wale na Tanzania inapata picha mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri; hamwoni sasa kuna mikakati ya Serikali kutenga maeneo maalum kuwajengea watu ambao hawana uwezo na mkawapa huduma za kijamii?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maryam Msabaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli. Alipokuja Rais Obama hapa, Mji wa Dar es Salaam ulipendeza ukawa mzuri. Mambo haya tunayozungumza hapa ni masuala ya *discipline*. *Discipline* maana yake ni kufanya jambo kama linavyotakiwa, kwa wakati unaotakiwa na mahali linapotakiwa.

Mheshimiwa Spika, ukiuchukua mkate ukasema hapa kwenye *toilet* hapa ni pasafi, ukasema unaweka mkate pale tutakwambia mkate haukai kwenye *toilet*. Ukichukua *toilet paper* ukaweka kwenye meza hapa, pamoja na kwamba ni safi, utaambiwa haikai hapo.

Mheshimiwa Spika, pakaenda pakafanyika haya yote yanafanyika na jambo analozungumza Mheshimiwa Maryam Msabaha ni jambo la msingi, mimi niko *conscious* na *politics* na *economics* za Dar es Salaam, nazielewa. Tumezungumza hizi habari tumewekana sawa tumesema na Sheria zimewekwa pale na utaratibu umewekwa kwamba, jamani hapa watakaa watu fulani, hapa watakaa watu fulani na hapa watakaa watu fulani, unakaa kidogo, unaona watu wanarudi kidogo-kidogo. Humu ndani umesikia maelekezo yaliyotolewa na Bunge hapa, tumetakiwa tuende kwenye Kamati tuende tukakae tuzungumze, tuseme tunakaakaaje.

Mheshimiwa Spika, Wabunge walitoka hapa wengine wamekwenda Jeshini. Ukienda, kuna mahali panaitwa *Smart Area,* Jeshini unapokwenda kwenye *Smart Area* hutembei tu hivi unatembea mwendo hivi, kuna mwendo unaotembea kwa *discipline* ya namna fulani. Ndicho kilichosemwa kwa Dar es Salaam pale, kikasemwa kwamba, hebu tuuweke mji ule uwe na *discipline* maalum watu wakienda pale kila mtu aheshimu taratibu zilizoko pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni *Member of Parliament* hapa anazungumza jambo la msingi. Mimi naomba nichukue nafasi hii, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuwaomba Viongozi wote tuoneshe kukomaa katika jambo hili. Kukomaa maana yake ni kufanya jambo hata kama hulitaki, ndio maana ya kukomaa. Tusaidiane wote sisi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Moshi na Mwanza pale, wamesifiwa wamekwenda mpaka *Rio-De-Janeiro* kwa sababu, ya kazi nzuri iliyofanyika pale, wameweka *discipline*. Wakitoka wale wakishafika Upare pale, wakiingia Mji wa Moshi pale, watu wote wanachukua mishikaki, wanachukua mifupa ya kuku wanaweka kwenye *packet,* hakuna kutupa tena. Wanangoja wahamie tena kwenye eneo lingine ambalo halina nidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Mwanza imefanya hivyo na kama Moshi imefanya hivyo na sisi wote tunawasifu hapa, mimi naomba tuichukue kauli ya Mheshimiwa Maryam Msabaha itumike kama Kauli ya Siku na Sheria ya Siku kutunza Miji yetu iwe katika hali ya usafi. *(Makofi)*

Mhesimiwa Spika, la pili. Mheshimiwa Maryam anasema kuna ongezeko la ombaomba, nenda kasome *The Political Economy of Capitalism,* nenda kasome *The Political Economy of Socialism* zitakuonesha mambo haya. Hapa kinachozungumzwa ni suala la *relations of Production*. Unafika mahali unakuta umetengeneza kundi la watu hivi, limetupwa barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ninachotaka kusema kwa kifupi hapa, usije ukanisimamisha Mama Spika. Hii ombaomba hapa, akina Matonya waliondolewa pale, wakaambiwa warudi, wakaondoka wakaenda zao, kidogo kidogo unaona wamerudi tena barabarani. Mimi nafahamu habari ya Matonya, ndio nafahamu, sasa nisije tena nikapata mgogoro hapa.

Mheshimiwa Spika, anasema habari ya *Rehabilitation Centres* na nini, zimeanza kufunguliwa, kule Mbagala wameanza kuzifungua. Sisi kama Halmashauri tunalichukua jambo hili, watu wanaozurura barabarani, kama wanazurura, watoto wadogo wanapozurura barabarani. Ukikuta wanatembea barabarani, wale watoto kama hawana baba, hawana mama na nini, baba yao ni Halmashauri na huu ndio ujumbe tunaoupokea hapa.

Mtu yeyote anataka kwenda kutoa hela pale akasema mimi nilitumia hela hizi kwa ajili ya kuwasaidia hawa ombaomba, ili wawekewe Kituo pale. Hata akija *CAG* atasema mapato haya na matumizi haya ni sahihi yapite, tunalichukua hili jambo Mheshimiwa. Tutakwenda kufanya hivyo kama alivyoelekeza. *(Makofi)*

SPIKA: Naona suala lenyewe limechukua dakika 10 badala ya 5. Tunaendelea na Wizara ya, eeh! Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, tumewahi kutoa mwelekeo na Sera za za Serikali juu ya kuwahifadhi na kuwatunza watu wasiojiweza, wakiwemo hawa wanaoishi katika mazingira magumu. Jukumu la kuwalea na kuwatunza watu waliopo kwenye mazingira magumu, wakiwemo hawa watoto, walemavu na watu wasiojiweza, jukumu la kwanza kabisa ni jukumu la familia, ni jukumu la jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo jukumu la Serikali peke yake kwa sababu, hakuna watoto hawa wanaokwenda barabarani ambao hawatoki kwenye jamii fulani. Katika mazingira ya Tanzania, tunavyojijua sisi tulivyolelewa, tunaishi katika familia pana sana. Kwa hiyo, pamoja na kwamba, Serikali itachukua jukumu lake, lakini jukumu la kwanza ni la familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulishatoa wito na Sera yetu inasema wazi kwamba, familia ichukue jukumu la kwanza. Ndugu wa karibu wachukue jukumu la kwanza, lakini baada ya hapo ndio tunakuja sasa ikishindikana kabisa kwa wale ambao hawana familia, hawana Ndugu, ndio inakuja jukumu sasa la Serikali za Vijiji na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa Dar es Salaam anapouliza Mheshimiwa Mbunge, tulishawahi kusema hapa, hata Mheshimiwa Mbunge mmoja aliwahi kusema, tunataka tuwaambie wale watu wanaowatumia vibaya hawa vijana kama mtaji wao wa kutengeneza pesa. Kuna watu wanawatumia vijana wengine na watu wengine kufanya hii shughuli ya omba omba, lakini kwa madhumuni ya kujitajirisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumewahi kuwajua, tumewahi kupeleleza taarifa zao kutoka kwa wale vijana tukagundua kwamba, kuna watu wengine unakuta kabisa wanalala, lakini fedha zile zinachukuliwa na watu walio wazima. Kwa hiyo, ziko tabia ambazo zinafanywa na watu ambao sio walemavu, watu ambao wanawatuma vijana wale kwenda kufanya ile kazi. Kwa hiyo, yote haya ni mambo ambayo yanasababishwa na jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Mbunge ajue kwamba, jukumu la kuwahifadhi hawa ombaomba na watu wasiojiweza kwanza ni jukumu la familia. Pamoja na hizo Halmashauri alizosema, lakini Halmashauri ni *Secondary, Primary* jamii ya Watanzania sisi wote tushirikiane katika kuwahifadhi hawa watu wasiojiweza.

SPIKA: Mmenichukulia dakika 13, sasa naendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Waride Bakari Jabu?

Na. 294

Uhalifu wa Tindikali na Ulipuaji Mabomu

MHE. WARIDE BAKARI JABU aliuliza:-

Yako matukio mengi makubwa ya uhalifu wa matumizi ya tindikali, ulipuaji mabomu na kadhalika, yanayotokea siku hizi mahali mbalimbali na hayaeleweki lini upelelezi wake wa kuwapata watuhumiwa utakamilika.

Je, ni nini Kauli ya Serikali kuhusu suala hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembe Samaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumejitokeza matukio ya uhalifu ya kudhuru watu na tindikali. Jumla ya matukio 11 yameripotiwa hapa nchini katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Arusha, Geita, Zanzibar, ambapo jumla ya watu 13 wameathirika.

Mheshimiwa Spika, matukio ya watu kumwagiwa tindikali hufanywa kwa siri na watu wasiojulikana ambao humlenga mwathirika usoni na hivyo kufanya utambuzi wa watuhumiwa kuwa mgumu.

Hata hivyo, Jeshi la Polisi limeendelea na uchunguzi wa kina wa matukio hayo, ambapo watuhumiwa watano wamekamatwa na kufikishwa Mahakamani na upelelezi wa matukio ya Zanzibar yaliyojitokeza unaendelea. Jumla ya watu 25 wamekamatwa na kuhojiwa na Polisi huko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kukabiliana na matumizi haramu ya tindikali Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, (*DPP),* na Mkemia Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar liliendesha *operation* kubwa, ili kupunguza matumizi holela ya tindikali. *Operation* hiyo imeonesha mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa milipuko ya mabomu jumla ya matukio 9 yaliripotiwa katika Mkoa wa Arusha, Morogoro, Lindi, Dar es Salaam, Mwanza na Zanzibar, ambako jumla ya watu 12 waliuwawa na 137 kujeruhiwa. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama linaendelea kufuatilia matukio hayo. Kwa sasa timu hiyo inaendelea na uchunguzi wa kisayansi, ili kubaini waingizaji wa milipuko ya mabomu hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawahakikishia wananchi kuwa imejidhatiti kukabiliana na vitendo vya uhalifu vya aina zote na hatua za Kisheria zitachukuliwa dhidi ya mtu au kikundi chochote kitakachothibitika kuhusika na matukio hayo.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii, kupitia Bunge lako Tukufu, kuwaomba wananchi wote kwa ujumla kuchukua tahadhari na mtu au kikundi chochote kinachofanya vitendo vinavyoashiria uhalifu, hususan ule wa tindikali na mabomu. Taarifa zitolewe haraka kwenye vyombo vya dola, ili hatua stahiki zichukuliwe.

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Jeshi la Polisi hutangaza kufanya upelelezi kwa matukio haya tuliyoyataja, lakini wananchi huwa hawaambiwi upelelezi ule ulivyoendelea. Na kwa kuwa, hivi karibuni Zanzibar walipelekwa mpaka Wapelelezi kutoka Marekani, *FBI,* kuchunguza lile tukio la kuuliwa kwa Padri Mushi.

Je, nilitaka kujua upelelezi ule umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Nilitaka kujua, hivi karibuni tumetaarifiwa kuwa kumetokea mlipuko unaosadikiwa ni wa bomu pale Darajani Mjini Unguja na umesababisha kifo cha mtu mmoja na kadhaa wamepata majeruhi. Nilitaka kujua je, Serikali inasema nini kuhusu tukio hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge Waride, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa nini Serikali au Jeshi la Polisi halitoi matokeo ya upelelezi. Upelelezi mara nyingi unakuwa ni mrefu katika matukio kama haya. Kama nilivyosema kurushiana tindikali inafanywa na mtu pengine yuko juu ya chombo na yule ambaye anarushiwa anarushiwa kwenye macho, kiasi ambacho anashindwa kusaidia Polisi katika kutoa taarifa.

Mheshimiwa Spika, lakini katika hatua za upelelezi, hasa zile za mwanzo, unaweza ukaharibu upelelezi kwa kutoa taarifa ya ulichopata. Hata hivyo kuna taarifa ambazo hutolewa ambazo ni *scanned,* ambazo hazina *depth,* hazina maelezo ya kina kila hatua inapofikiwa. Kwa hiyo, nafikiri kitu muhimu ni tuendelee kufuatilia vyombo vya habari kwa sababu, mara zote Jeshi la Polisi, kupitia Msemaji wake, huwa wanatoa Taarifa kama hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, angalau kama hazikutoka kwamba, tumefikia wapi? Tumeshika wangapi? Inatolewa pale ile siku watuhumiwa wanapokwenda Mahakamani. Hata hivyo Jeshi la Polisi litajitahidi kutoa zile taarifa ambazo haziwezi kuwa na madhara kwa upelelezi ambao utakuwa unaendelea.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu mlipuko wa Darajani; ni kweli kwamba, kulitokea mlipuko Darajani na mlipuko huu ulisababisha kifo cha mtu mmoja na majeruhi saba. Marehemu alizikwa na majeruhi wakatibiwa katika Hospitali za Mjini Unguja na hatimaye mpaka tarehe ya juzi wote walikuwa wametoka Hospitali.

Mheshimiwa Spika, upelelezi wa tukio hili umeanza na tunao watu tayari tumewakamata, tunaendelea kuwahoji, ili tupate taarifa nyingine. Tunawaomba wananchi ambao waliona tukio hili au wana taarifa yoyote kwa sababu, upelelezi bado ni unaanza, waendelee kutusaidia kutoa taarifa walizonazo.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi ni kwamba, niwaombe Watanzania kuacha tabia hizi za kuleta madhara kwa wenzao ambao hawana hatia katika lolote ambalo wanalifikiria. Tuendelee kuvumiliana siku zote kutakuwa na tofauti za haya mambo na jambo zuri ni kuvumiliana na kufanya vikao kuliko kuendelea kutumia silaha hizi ambazo zinaumiza na kupoteza maisha.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kunipa nafasi. Nataka kuuliza kumekuwa na matukio ya mauaji ya wahalifu ndani ya mikono ya polisi. Ndani ya mwezi huu matukio mawili pale Musoma Mkoa wa Mara jana wahutumiwa wanaokamatwa kwa kosa la kucheza kamari na uzururaji na uzembe. Mheshimiwa Waziri Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na mauaji haya ya watuhumiwa ndani ya mikono ya polisi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA N DANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Katiba na Sheria tulizonazo za nchi hii haziko chini ya mtu yoyote yule kwamba hakuna mtu ambaye yuko juu ya Katiba au yuko juu ya sheria. Polisi ambao wamehusika kufanya matukio haya tutayachunguza au tumeanza kuyachunguza na lolote litakalojitokeza basi hatua stahiki zitachukuliwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria ya nchi hii. *(Makofi)*

Na. 295

Maslahi ya Askari

MHE. SAID MUSSA ZUBEIR (K.n.y. MHE. JAKU HASHIM AYOUB) aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia Askari Polisi wanapoumia kazini kwa kuwa kazi wanazozifanya zinahatarisha maisha yao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia upya haki ya likizo ya uzazi na haki ya likizo ya mwaka kwa askari ili zisipingane na misingi ya haki za wafanyakazi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali huwalipa askari polisi wanaumia au kufariki wakiwa kazini. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya fidia ya askari polisi na Magereza ya mwaka 2010 iliyotangazwa kwenye gazeti chini ya *GN 270* ya tarehe 30 Julai, 2010.

(b) Mheshimiwa Spika, likizo ya Askari Polisi zipo kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za ajira za jeshi la polisi. Utaratibu huu unazingatia masharti ya ajira ya askari ambapo hupewa likizo ya siku 84 kwa kipindi cha miaka mitatu, sawa na siku 28 kwa kila mwaka. Hivyo ni kweli kwamba taratibu za likizo na uzazi na likizo za mwaka zinalingana na misingi ya haki za wafanyakazi. Hata hivyo katika maboresho yanayoendelea kufanywa na Jeshi la Polisi taratibu mbalimbali zitaangaliwa upya ili kuweka maslahi yawe mazuri zaidi.

MHE. SAID MUSSA ZUBEIR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimshukuru Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa majibu mafupi na yenye mwekeleo. Nilikuwa na maswali mawili, kwanza nilikuwa nataka kuelewa viwango vya fidia kati ya anayeumia na wanaofariki, fidia zao zikoje kuhusiana na viwango.

Kuna mkanganyiko mkubwa wa unaohusiana na masuala ya likizo, nataka atoe ufafanuzi tu wa likizo ya uzazi na ugonjwa kwenye Wizara yake.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu viwango vya fidia vya askari wanaoumia au kufariki kazini, kwa mujibu wa kanuni nilizosisema, viwango vinaanza shilingi milioni moja mpaka milioni tano kwa wale wanaoumia kulingana na *percentage* ya maumivu kama itakavyokadiriwa na madaktari. Halafu kwa yule ambaye amepoteza maisha kabisa fidia kwa familia ni shilingi milioni 15.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba likizo ya kawaida inatofautiana na ya watumishi wengine kwamba wanapewa kwa miezi mitatu kwa maana ya kwamba miaka mitatu apewe likizo askari lakini anapopewa anapewa siku zake 28 mara tatu. Likizo za uzazi ni kama wanavyopewa wazazi wengine kwenye utumishi umma na hivyo hivyo likizo za ugonjwa hazitofautiani na watumishi wa kawaida wa Serikalini.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipatia nafasi niulize na mimi swali. Ni kweli kwamba likizo kwa askari wetu imekuwa ni tatizo hususan askari wetu wa jimbo la Kwimba na kwingineko kote nchini, ukizingatia wanaume hawapewi likizo ya uzazi kwa ajili ya wake zao ili waweze kuwasaidia mambo madogo madogo wakati wamejifungua. Sasa Serikali iko tayari kurekebisha sheria na kuwapatia askari wetu wanaume likizo ya uzazi ya kutosha?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, likizo tunapopata watoto inawezekana ikawa ni muhimu kwa baba na mama na suala hili nafikiri sio kwa jeshi la polisi tu kwa sababu sio polisi peke yao ambao wangestahiki au askari hata sisi tuliofanya siasa na wengine.

Ni bahati mbaya kwamba sera zetu hazijatufikisha pa kuwapa likizo ya uzazi wanaume, nafikiri tuna haki ya kuitetea na pale tutakapokubaliana basi na askari watapata baada ya kukubaliwa kwenye *main stream.*

NAIBU SPIKA: Jamani muda umekwenda sana naomba niendelee na maswali mengine, lakini likizo kwa wanasiasa mna likizo nyie. Tuende Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

Na. 296

Kuwawezesha Wavuvi Wadogo wa Ziwa Victoria

MHE. JASSON S. RWEIKIZA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuwawezesha Wavuvi wadogo wadogo wa Ziwa Victoria badala ya kuwazuia tu kuvua kwa kutumia vifaa ambavyo sio endelevu?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa rasilimali za uvuvi na mazingira yake zinakuwa endelevu Serikali inatekeleza sheria ya uvuvi, Namba 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 ambayo imeainisha zana za uvuvi zinazoruhusiwa kutumika ili rasilimali za uvuvi ziweze kuwa endelevu.

Pia sheria hiyo imeainisha maeneo ya uvuvi, ambayo ni mazalio na makulio ya samaki ambapo shughuli za uvuvi haziruhusiwi kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na jitihada za kuwawezesha wavuvi wadogo kwa kuhakikisha kuwa zana za vyombo vya uvuvi vinapatikana kwa bei nafuu.

Katika jitihada hizo Serikali imefuta kodi ya ongezeko la thamani yaani *VAT* kwenye injini, za kupachika *outboard engine,* nyuzi za kushonea nyavu za uvuvi *fishing twines* na vifungashio. Vilevile kulingana na *East Africa Publication on Common External Tariff,* injini za uvuvi, malighafi

zinazotumika kutengeneza zana mbalimbali za uvuvi na viambata vyake hupewa punguzo la kodi ama kufutiwa kodi kabisa ili kuwawezesha wavuvui kumudu bei za vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Benki ya Rasilimali ya *TIB* kupitia dirisha lake la kilimo imewezesha miradi minne ya uvuvi yenye thamani ya shilingi bilioni 1,512,656,328/= katika Halmashauri za Sumbawanga, Ukerewe mmoja, Ilemela mmoja, Muleba moja na miradi hiyo imewezesha upatikanaji wa boti nne za uvuvi na vifaa vya kuhifadhia samaki katika Halmashauri ya Sumbawanga. Boti sita (6) za uvuvi katika Halmashauri ya Ukerewe na boti 28 za uvuvi, injini za boti 20 na boti moja ya doria katika Halmashauri Ilemela.

Pia Benki ya *TIB* imewezesha uboreshaji wa ufugaji wa samaki kwa kupanua mabwawa ya samaki na kujenga kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki kwa wafugaji wa samaki katika Halmashauri ya Muleba. Aidha, Serikali inatekeleza mfumo wa kutoa ruzuku kwa wavuvi, ambapo kupitia Vyama vya Ushirika wavuvi watapata zaidi ya zana za uvuvi, boti na viambata vyake kuchangia asilimia 60 ya bei na Serikali kuchangia asilimia 40.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru majibu mazuri ya Serikali lakini nina swali moja. Ni dhahiri kwamba wananchi hawa wanaponunua vifaa hivi ambavyo si halali haviruhusiwi wanavinunua sehemu ambazo ni halali madukani na wanaotengeneza vifaa hivi viwandani na wanaoviuza wanajulikana. Kwanini Serikali inasubiri kwamba wananchi wavinunue halafu waje wanyang'anywe zile nyavu na maboti yao na nini wapate hasara kubwa hawa maskini badala ya kuzuia wale wanaotengeneza ili visiwafikie wananchi kupata hasara kubwa kama waliyoipata?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rweikiza, kama ifuatavyo. Kimsingi kwanza hivi vifaa vinaitwa haramu, kinapokuwa kitu haramu inamaana hakitengenezwi katika njia iliyo wazi.

Kwa hiyo, wale wanaotengeneza kwa njia hiyo harama na kufanya biashara hiyo haramu wote ni wanavunja sheria. Kwa hiyo, wakikamatwa wote wanashughulikiwa, hata sasa hivi kuna operesheni inaendelea haiachi madukani au kama kuna viwanda ili kuhakikisha kwamba wote wanakamatwa na wanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pale Bukoba kwa maana ya Bukoba Mjini na Bukoba Vijijini wako wafugaji ambao wanafuga samaki kwenye mabwawa. Lakini tatizo lao ni kupata elimu sahihi na mashine ya kuweza kutengeneza chakula cha samaki kwa sababu samaki wanakula chakula kilicho kwenye fomu ya *perets* na Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja aliahidi kuwanunulia mashine moja angalau ya kuanzia kwenye mkoa huo.

Je, ni lini Serikali sasa itaweza kuwanunulia hiyo mashine na kutoa elimu sasa hiii kwa hawa wanaotaka kufuga samaki wa mabwawa?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo.

Ni kweli hilo eneo au vikundi vinavyofuga samaki katika wilaya ya Bukoba na mkoa wa Kagera wanafanya juhudi kubwa sana katika ufugaji wa samaki na mimi ningependa kuwapongeza sana wananchi wa Kagera kwa sababu wameonyesha mwitikio mkubwa sana.

Ni kweli kuna tatizo la mashine za kutengeneza vyakula sasa hivi kuna kampuni moja inakamisheni imeleta mitambo inaanza uzalishaji kwa majaribio, lakini ile ahadi ya Waziri Mkuu tutaifuatilia ili kuona kwamba kikundi hicho kinasaidiwa. Mimi kikundi hicho nimekitembelea wanafanya juhudi kubwa sana na sasa hivi katika mpango wetu wa Bajeti wa mwaka huu tunategemea kwamba tutakua na fungu kwa ajili ya kusaidia vikundi vya namna hii kikiwemo kikundi hicho cha Kagera.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, wapo samaki katika ziwa Victoria ambao kwa asili yake hawakui, kwa maana ya furu na dagaa na nyavu zinazoruhusiwa haziwezi kuwakamata samaki wale na ni lazima wavuliwe. Nilipenda kujua Serikali inawashauri nini wavuvi wanaotaka furu na dagaa?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nijibu swali la Mheshimiwa Nyerere, kama ifuatavyo:-

Katika ziwa Victoria kwanza nimfahamishe tu kwamba baada ya kupandikiza samaki yule aina ya Sangara ikolojia ya ziwa Victoria imebadilika sana kulikuwa na aina ya hao samaki tunaoita furu zaidi ya aina 300, lakini baada ya sangara kuingia ambao chakula chao kikuu mojawapo ni hao furu, sasa hivi wamebaki aina 16 tu ya furu, kiasi kwamba ndiyo maana hata ukiyaona maji ya ziwa Victoria samaki hao ndiyo waliokuwa kitu kinatiwa pratozi ambayo ndiyo ile kijani inayoonekana ndani ya ziwa. Sasa moja ya sababu ya kuchafuka sana ni kwa sababu ya kupungua kwa furu.

Kwa hiyo, kinachofanyika sasa utafiti unaendelea ili kuona namna gani aina ya hao samaki wanaweza wakarejeshwa ili warejeshe ili ikolojia. Lakini japo lakini jema ni kwa sababu sasa sangara wanavunwa sana sasa hivi na wamepungua sana, hii natoa tena fursa kwa aina ya hao furu kukua. *(Makofi)*

Na. 297

Gharama za Ada – Chuo Kikuu

MHE. ISMAIL A. RAGE aliuliza:-

Gharama za kulipia Ada ya masomo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na Vyuo Vikuu vingine ni kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala zima la elimu na Ada katika vyuo mbalimbali katika nchi yetu Tanzania limekuwa likitofautiana kwa muda mrefu. Kwa sasa Tanzania ina jumla ya vyuo vikuu 53 na Taasisi 21 zinazotoa shahada na sera ya elimu ya juu ya mwaka 1999 kifungu Namba 6, 4, 3 kinaruhusu taasisi za elimu ya juu kupanga ada katika vyuo hivyo kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia idadi ya vyuo niliyoitoa awali naomba nitoe mifano ya Ada za Kozi kadhaa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma. Katika *program* za Uhandisi, chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatoza ada ya Tshs. 1,300,000/= kwa mwaka, wakati Chuo Kikuu cha Dodoma, kinatoza Tshs. 1,500,000/= kwa mwaka…

SPIKA: Hebu rudia tena, umechanganya hizo.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, hapana.

SPIKA: Rudia tena.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Tanzania ina jumla ya Vyuo Vikuu 53 na Taasisi 21 zinazotoa Shahada. Sera ya elimu ya juu ya mwaka 1999 kifungu 6, 4, 3 kinaruhusu Taasisi za elimu za juu kupanga na kusimamia vyanzo vya mapato ikiwa ni pamoja na kutoza Ada za masomo. Gharama za Ada ya masomo katika Chuo Kikuu hutegemea chuo na *program* ambayo mwanafunzi anasomea.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia idadi ya vyuo niliyoitoa awali naomba nitoe Mifano ya Ada za Kozi kadhaa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma. Katika *program* za Uhandisi, chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatoza Ada ya Tshs. 1,300,000/= kwa mwaka, wakati Chuo Kikuu cha Dodoma, kinatoza Tshs.1,500,000/= kwa mwaka.

Katika *program* ya Sayansi na ualimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatoza Tshs. 1,300,000/= wakati Chuo Kikuu cha Dodoma kinatoza Tshs. 1,200,000/=. Aidha katika *program* za Ualimu wa Masomo ya Sayansi ya Jamii, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatoza Tshs. 1,500,000/= wakati Chuo Kikuu cha Dodoma kinatoza Tshs. 800,000/=.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia tofauti za kiasi cha Ada kinachotozwa na vikuu nchini, Serikali ilifanya utafiti wa kina kwa kushirikisha wadau mbalimbali ili kuweza kupanga Ada elekezi kwa *program* zote zinazofundishwa katika Vyuo Vikuu vyote. Mwongozo wa Ada elekezi ulizinduliwa tarehe 13 Machi, 2014 na Ada mpya zitaanza kutumika mara tu baada ya utaratibu wa mfumo huo mpya kukamilika.

\

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Katika Vyuo vya Utumishi hasa Chuo cha Dar es salaam, Singida, Mtwara na Tabora wanafunzi wanalipa shilingi milioni 1,015,000/= kwa mwaka, malazi 350,000/= Chakula kwa mwezi shilingi 300,000/= takribani kama shilingi milioni nne na ushee.

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia hawa vijana na wao wapate mikopo?

Je, ni lini Serikali itafuatilia Ada katika vyuo binafsi ambavyo ni vya juu sana kuliko vya Serikali.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumshukuru sana Mheshimiwa Aden Rage, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kusimamia elimu katika Jimbo lake lakini hasa katika Chuo hiki cha Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa nilizonazo tu pale katika chuo chetu kuna Zahanati nzuri sana na Mheshimiwa Aden Rage amekuwa akiisaidia sana ili kuwahudumia wanafunzi na wananchi kwa ujumla.

Sasa nirudi kwenye maswali ya msingi ya Mheshimiwa Aden Rage haya ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ada ya kozi ya *Diploma* katika Chuo cha Utumishi kilichopo Tabora ni takribani milioni moja na karibu 1,025,000/= lakini ukilinganisha ada ya kozi hiyo hiyo ya *Diploma* katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha pale pale Tabora wao ada yao ni takribani milioni moja laki nne na kama arobaini na tano hivi. Sasa ukilinganisha vyuo hivyo viwili utakuta kwamba bado ada ya Chuo cha Utumishi wa Umma iko chini ukilinganisha na ile ada ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha. Hata hivyo, Mheshimiwa Aden Rage anasema hilo si suala kwanza la msingi lakini ni lini wanafunzi hawa watapatiwa mikopo kama wanavyopatiwa wanafunzi wengine.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunajitahidi sana shida tunayoipata watoto wetu wengi wa Kitanzania wanapopata mikopo hii ya elimu ya juu hawana tabia ya kuirudisha kwa wakati. Kwa hiyo, Serikali inaendelea kufanya utaratibu wa kuhakikisha mikopo hii irudishwe halafu iweze kuwatosheleza wanafunzi wengine zaidi ya zile kozi ambazo ni za kipaumbele katika nchi yetu ya Kitanzania. Mara hayo yakiweza kukaa vizuri, tutafanya hiyo kazi kwa kozi zote licha ya zile kozi ambazo ni za kipaumbele na wanafunzi wengine watapatiwa hiyo nafasi.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Aden Rage ameniuliza tena, ada za vyuo vikuu na hasa Vyuo Vikuu binafsi ni kubwa sana. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, lakini nimesema katika majibu ya msingi kwa sasa Serikali imeamua kuleta muundo wa Ada elekezi kwa Vyuo vyote vya Serikali na visivyo vya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lengo letu sasa ni kuviagiza Vyuo hivi Ada zote zitakazotozwa kwa wanafunzi kwanza ziwe halali, ziendane na uhalisia wa *program* zinazotolewa kwenye vyuo hivyo, lakini tunataka ku-*discourage* tabia ya baadhi ya Taasisi na Vyuo Vikuu kutumia Ada kama fedha ya uendeshaji katika Vyuo vyao.

Kwa hiyo, hali hii imeanza kutekelezwa, Serikali tumemaliza maandalizi ya maelekezo hayo, tunategemea baada ya muda si mrefu ada elekezi zitafanyiwa kazi na Tume ya Vyuo Vikuu itasimamia suala hili kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, niwahikishie Wabunge na Watanzania wote kuwa Serikali imeona tatizo hili na inalifanyia kazi. *(Makofi)*

SPIKA: Haya tunaendelea kwa sababu tuna maswali matano kwa dakika 15 kwa sababu tumesema sana, kwa hiyo tunaendelea na swali linalofuata.

Mheshimiwa Namelock Edward Sokoine, kwa niaba yake Mheshimiwa Betty E. Machangu.

Na. 298

Watu Wanaosomea Ualimu

MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MHE. NAMELOCK E. SOKOINE aliuliza:-

Serikali imeamua kutoa mikopo kwa watu wanaotaka kusomea Ualimu lakini imejitokeza hali kuwa baadhi ya watu wakishapata Shahada ya Kwanza ya Ualimu huamua kusomea fani nyingine na kuachana na Ualimu.

Je, Serikali inawabanaje watu hawa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wiziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Namelock E. Sokoine, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya walimu wa Shule za Sekondari nchini ni 89,500 lakini waliopo ni 74,250 na upungufu ni 15,250. Ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa walimu, Serikali iliamua kufanya Fani ya Ualimu kuwa mojawapo ya kipaumbele katika utoaji wa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa fursa ya kuajiri walimu wote wenye sifa mara tu wanapohitaji mafunzo yao wakiwemo wenye shahada. Hata hivyo, imebainika kuwa idadi ndogo ya walimu huamua kuacha kazi ya ualimu na kujishughulisha na kazi nyingine. Kwa mfano, mwaka 2011/2012, idadi ya walimu walioacha kazi ya ualimu na kujiunga na kazi nyingine ni 217,000 kati ya 52,146 sawa na asilimia 0.42. Aidha, mwaka 2012/2013, idadi ya walimu walioacha kazi ya ualimu na kujiunga na kazi nyingine ni 220,000 kati ya 74,250 sawa na asilimia 0.03.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua za awali za maandalizi ya kuangalia namna ya kuweka utaratibu utakaombana ama kumwelekeza mwalimu aliyenufaika na mkopo kutumikia katika kada ya ualimu kwa kipindi fulani kabla ya kuamua kuingia katika kada nyingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuinua ubora wa mazingira ya kufanyia kazi walimu ili wahitimu waweze kujiunga na ajira ya ualimu na kudumu katika ajira hiyo. *(Makofi)*

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali ya nyongeza mawili. Swali la kwanza, miaka ya 1970 mpaka 2000 Serikali ilikuwa na huo utaratibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, anaousema ulikuwa unaitwa Bondi kwamba mwajiriwa wa Serikali yoyote anaweka Bondi na Serikali kwamba hataondoka kwenye ile ajira mpaka labda miaka mitatu au mitano. Kwa nini waliondoa mfumo huo?

Ajira zimekuwa za matatizo sana na kwa hali ya kawaida ungetegemea mwanafunzi aliyekopa fedha kwa ajili ya elimu ya juu ule mkopo alipe kwa kukatwa mshahara kwenye ajira yake. Kwa sababu ya matatizo ya ajira, Serikali inaweza kutueleza kwamba hizi fedha zitapatikanaje?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi naomba.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, mifumo hii ya usimamizi wa ajira katika nchi yetu ya Tanzania imekuwa ikibadilika mara kwa mara kutokana

na hali halisi ya mazingira na hali halisi ya namna ya Utumishi wa umma katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, uliona miaka ile ya 70 tulikuwa na huo mfumo wa Bondi lakini hapo katikati uliondoka kulingana na mazingira ya utumishi wa umma katika nchi yetu ya Tanzania.

Kwa hali hiyo ndiyo maana sasa Serikali baada ya kuondoa imeona kuna umuhimu wa kurudisha tena katika sekta mbalimbali ambazo ni za kipaumbele na hivyo tunajipanga kuurudisha tena hili hasa kukidhi mahitaji ya walimu katika nchi yetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awe tu na amani haya yote yanaendana na mifumo inavyokwenda ya utumishi na mabadiliko ya kimazingira katika ajira zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua ni namna gani sisi kama Serikali tumejipanga kwa sababu kuna wanafunzi wanapata mikopo lakini hawapati ajira. Kuna wanafunzi wanapata mikopo wakwenda kufanya kzi nje ya nchi ya Tanzania na uwezo wa kupata hii mikopo unakuwa mgumu.

Naomba nilihakikishie Bunge lako tukufu sisi kama Serikali tatizo hili tumeliona, tumefanya mikakati mbalimbali, kwa mfano sasa hivi nchi yetu ina utaratibu wa kuanzisha vitambulisho vya Uraia, kupitia kwenye vitambulisho hivi vya Uraia tutawambua Watanzania wote waliofaidika na mikopo yetu na tunaweka taratibu maalum kabisa za kuwafikia na kuweza kukata fedha zao hizo, ama kwenye ajira rasmi ambazo watazipata, ama kwenye ajira zisizo rasmi kwa sababu wote tutakuwa tumewatambua na wako katika nchi yetu.

Kwa mfano, wale wanaoenda kufanya kazi nje ya Tanzania, tumewasiliana sasa na watu wa Uhamiaji, watu hao hawatapata *VISA* za kwenda nje ya nchi kabla hawajalipa mikopo ambayo wamelipiwa na nchi yetu ya Tanzania na ndipo waende wakafanye kazi huko nje. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunayo mikakati mingi na Waheshimiwa Wabunge wakitaka tutawaletea yote, tutawaletea lakini tumejipanga na tumetambua tatizo hili. *(Makofi)*

SPIKA: Maswali na majibu ya maswali marefu dakika ni tatu wakati maswali ni mengi. Ninaingia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Rukia Kassim, atauliza swali linalofuata.

Na. 299

Madhara Yatokanayo na Dawa za Kuongeza Maumbile

MHE. RUKIA KASIM AHMED aliuliza:-

Kumejitokeza baadhi ya akina mama kutumia dawa za kuongeza makalio pamoja na baadhi ya wanaume kutumia dawa za kurefusha maumbile yao.

Je, Serikali inaweza kutuambia ni madhara gani wanayoyapata baada ya kutumia dawa hizo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa haijawahi kusajili dawa yoyote hapa nchini kwa ajili ya kuongeza makalio kwa akina mama au kurefusha maumbile ya akina baba. Hii inamaanisha kuwa bidhaa hizo hazitambuliki kwa matumizi ya binadamu kwa kuwa hazijasajiliwa na hivyo Mamlaka kutokuwa na taarifa za kisayansi zilizowasilishwa na watengenezaji wa bidhaa hizo ili kuhakikiwa kitaalamu ikiwa ni pamoja na madhara yanayotarajiwa kutokea pindi bidhaa hiyo itakapotumika kwa binadamu.

Mheshimiwa Spika, rai yangu ni kuwa wale wote wanaoingiza nchini kemikali hizo kwa kificho pamoja na wale wanaotumia waache mara moja. Aidha, hatua kali aitachukuliwa kwa yeyote atakayebainika kuziingiza hapa nchini. *(Makofi)*

MHE. RUKIA KASIM AHMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kuna baadhi ya magazeti yanatoa matangazo ya wauzaji wa madawa haya pamoja na nchi anayotoka haya madawa na namba za simu za wauzaji.

Je, ni kwa nini Serikali haijawahi kuwakamata na kuwafungulia mashataka wauzaji hawa wanaoleta madawa ambayo yanaathiri Watanzania?

Pili, endapo watumiaji wa madawa haya wamedhurika.

Je, Serikali iko tayari yule mwuzaji kumlipa fidia huyu ambaye ameathirika na madawa haya?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

(a) Katika magazeti pamoja na kule nchi zinakotoka dawa hizi, matangazo hayo katika magazeti kwa kufuata sheria namba moja ya mwaka 2003 ya Mamlaka ya Chakula na Dawa na Vipodozi imebainisha barabara dawa zile ambazo zinaingia nchini zile ambazo zimesajiliwa. Viwanda vya kutengeneza dawa hizo ni viwanda vile ambavyo vimesajiliwa hapa nchini. Katika taarifa tulizonazo hatujasajili dawa wala kiwanda cha aina yoyote hiyo.

Kwa hiyo, tunaomba ushirikiano kwa wale wote watakaobaini haya tusaidiane taarifa zipatikane na hatua kali ziweze kuchukuliwa. Kwa sababu taarifa tunazozipata kwa wale watumiaji katika maeneo mengine hapa nchini zinafanyika kwa kificho na wakati mwingine katika mahoteli. Kwa hiyo, tunaomba ushirikiano na vyombo vya serikali visaidie kudhibiti suala hili.

Madhara mengine yanaweza kujitokeza mtumiaji anaweza, kwa mfano kama ni mama tako moja likawa dogo lingine kubwa. Lakini pia mwingine hata matiti, titi moja likawa kubwa na jingine dogo na kwa akina baba wakati mwingine umbile linaweza likawa kama mkufu.

Kwa hiyo, ni vizuri madhara haya tukayaepuka. Tunatoa kauli kali kwa wale wote ambao ni watumiaji waache mara moja. (*Makofi/Kicheko*)

(b) Mheshimiwa Spika, suala la kulipa fidia si jukumu la Serikali kwa sababu ni utaratibu ambao mtumiaji anatumia kwa hiari yako bila kuishirikisha Serikali. Serikali kwa sheria tulinayo namba 1 ya mwaka 2003 ya Mamlaka ya Chakula na Dawa na Vipodozi hairuhusiwi. *(Makofi/Kicheko*)

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mimi siko kwenye makalio wala maumbile makubwa au madogo.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili hili nilitoa maelezo binafsi kuhusu matatizo ya mashine za mionzi katika Hospitali yetu ya *Ocean Road* lakini Wizara iliji-*commit* kwamba itachukua hatua za dharura lakini mpaka ninavyoongea hivi sasa bado zile mashine hazifanyi kazi na akina mama ambao wana kansa ya shingo ya uzazi wanaendelea kupata tabu. Hili jambo *serious* ningependa kupata majibu kwa Serikali hiyo hatua ya dharura inachukua miezi mingapi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ni swali zito, siyo penyewe lakini suala zito. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Ndugu yetu Esther Bulaya, Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Mara kwa ufuatiliaji wa karibu sana katika Tiba ya Saratani ya Shingo ya Kizazi kwa akina mama. Ni kweli taarifa ambayo Serikali ilitoa hapa kama kauli ya Serikali jambo hili kweli limeshughulikiwa kidharura kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 Mei, 2014 mwezi uliopita Fedha zipatazo Dola za Kimarekani 221,000 zililipwa kwa Kampuni ya *Thero-tronics* ya kule Canada. Fedha hizo baada ya kuwa zimelipwa wataalam walikuja nchini katika mashine mbili zilizokuwa zimeharibika moja ilikuwa inahitaji ukarabati na nyingine ilikuwa inahitaji kifaa cha *Source* ya *Cobalt* ambayo inatoa mionzi ya *gamma rays* ambayo inasaidia kutibu saratani ya Kansa ya Kizazi.

Wataalam hawa wamekuja wamefanya service katika mashine moja ambayo ilikuwa inahitaji service. Kifaa kingine kile baada ya fedha hizi kulipwa kule Canada kinatakiwa kitengenezwe katika kiwanda ndani ya miezi mitatu. Utengenezaji wa kifaa hiki ambacho ni *cobalt source* ambayo inatoa mionzi hii ya gamma rays ambayo ndiyo inatibu saratani au kansa kazi hiyo inaendelea na mara itakapokamilika kifaa hicho kitaingia hapa nchini. *(Makofi)*

Na. 300

Kurahisisha Matibabu kwa Wagonjwa wa Ukimwi

MHE. DKT. KHAMIS A. KIGWANGALLA aliuliza:-

Wagonjwa wa UKIMWI hutibiwa katika kliniki maalum na dawa za kupunguza makali ya ugonjwa yanayoambatana na UKIMWI pia hutolewa kwenye madirisha maalum. Kwa kuwa uelewa wa ugonjwa huu sasa ni mkubwa na madaktari wengi wanauelewa.

(a) Je, kwa nini Serikali isiruhusu hospitali zote kutibu Wagonjwa hao, ili wagonjwa wengi waweze kwenda kwa Madaktari wanaowataka?

(b) Je, kwa nini dawa za kupunguza makali ya ugonjwa huo zisiwepo kwenye hospitali zote na hata kwenye maduka ya dawa ili wenye uwezo wanunue huko kwani wapo wagonjwa zaidi ya milioni moja wanaohitaji dawa hizo na uwezo wa Serikali ni kuhudumia wagonjwa laki tatu na nusu (350,000) tu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Khamis A. Kigwangalla, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Desemba 2013 hospitali zote, vituo vya afya vyote na baadhi ya zahanati nchini zilikuwa zinatoa huduma za matunzo na tiba ikijumuisha dawa za kupunguza makali ya Virusi Vya UKIMWI (VVU) kwa watu wanaoishi na Virusi. Jumla ya vituo vya kutolea huduma hiyo ni 1,209 ikilinganishwa na vituo 96 vilivyokuwa vinatoa huduma hiyo mwaka 2005.

Aidha, huduma hii hutolewa kwenye vituo vya umma na vya binafsi pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali bila malipo baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa. Pia mgonjwa ana uhuru wa kuchagua kituo cha kupata matibabu bila kujali ni cha umma, binafsi au taasisi ya kidini ikiwamo dakitari au mtoa huduma anayemtaka.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda pia kilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa uwezo wa Serikali kuhudumia watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI siyo 350,000 tu kwani mpaka kufikia Desemba 2013 wagonjwa walikuwa wameandikishwa kwenye vituo vinavyotoa nchi nzima ni 1,366,402 na wapatao 850,274 walikuwa wameshaanzishiwa dawa za kupunguza makali ya Virusi vya UKIMWI. Aidha, Wizara inaendelea kuwaandikisha watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na kuwaanzishia dawa kutegemea na mwongozo wa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kutoa huduma bora za matunzo na tiba kwa WAVIU ikiwemo kupata dawa sahihi bila malipo nchi nzima. Hata hivyo Sheria ya Mamlaka ya Chakula na Dawa ya mwaka 2003 na Sheria ya Baraza ka Famasia ya mwaka 2011 hazimzuii mfanyabiashara aliyesajiliwa kufanya biashara ya dawa, kuuza dawa za kupunguza makali ya VVU.

Nia ya Serikali ni kuhakikisha WAVIU wanapata huduma inayotakiwa kwa kuzingatia kuwa wanahitaji ufuatiliaji wa karibu ili kupunguza uwezekano wa VVU kujenga usugu dhidi ya makundi ya dawa yaliyoidhinishwa kutumika nchini.

SPIKA: Ahsante sana, Dkt. Kigwangalla swali la nyongeza.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa tiba na huduma zote za Virusi vya Ukimwi, kuanzia kinga na hata madawa yanategemea kwa kiasi kikubwa fedha za wafadhili kutoka nje ya nchi.

Je, Serikali haioni kama ni hatari kutegemea fedha hizi kwa ajili ya kutoa dawa hizi na huduma nyingine kwa wagonjwa wetu?

Lakini la pili, nilipenda kujua, ni hatua gani zimechukuliwa mpaka sasa kwa babu Maarufu wa Samunge, ambaye aliibuka na dawa ambayo alidai kwamba inatibu Virusi vya Ukimwi pamoja na magonjwa mengine na hata baadhi ya viongozi waliomo humu ndani walishiriki kupata kikombe cha Babu. Sasa ni hatua gani zimechukuliwa hasa baada ya kubainika kwamba Kikombe cha Babu hakikuwa tiba ya aina yeyote ile bali ilikuwa ni kikombe cha kurahisisha zaidi safari ya wagonjwa kuelekea kwenye umauti? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba jibu kwa kifupi muda umeisha.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo.

Sehemu ya (a), suala la matibabu chini ya makubaliano ya kidunia kupitia *Global Fund* pamoja na fedha ya mfuko wa pamoja, dawa hizi kwa ughali wake ni vizuri kununua kwa pamoja kwa utaratibu ambao unaitwa *Pooled Procurement Mechanism.*

Kupitia utaratibu huu *Global Fund* wanaweza kununua kutoka viwandani katika gharama ambayo ni nafuu kuliko ambayo tungeweza kununua kutoka kwa mfuko wetu sisi, kwa fedha yetu ya ndani.

Lakini kawaida Serikali tunatenga fedha ya dharura pale ambapo kama hakuna uwezekano huo tuweze kununua sisi wenyewe, na ndiyo sababu katika Bajeti ambayo inakuja, kusaidia kugomboa dawa hizi kutoka nje tumeanza kutenga japo fedha kidogo, takriban bilioni tano kwa ajili ya kusaidia ugomboaji.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya (b), juu ya suala la matibabu ya Samunge kupitita kwa Babu wengi wakimwita hivyo. Suala la kuchukua hatua, hakuna ushahidi ambao ulibainika kwamba aliyetumia dawa au kikombe kile cha Babu kapata madhara kutokana na kikombe, kutokana na kikombe kwa utafiti ambao Wizara ya Afya ilifanya kupitia Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binaadamu *(NIMRI)*.

Kwa hiyo ile dawa haikuwa na madhara moja kwa moja kumdhuru binaadamu, kwa hiyo kama kuna bahati mbaya Mtanzania aliyefariki ni kutokana na ugonjwa aliokuwa nao.

SPIKA: Haya, tuendelee na swali linafuata, muda umekwisha, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Suleiman Said Bungara.

Na. 301

Magofu Yetu Nchini

MHE. SELEMANI SAID BUNGARA aliuliza:-

Sera ya Serikali yetu inataka magofu yote hasa ya kihistoria yabaki kuwa mali ya Serikali na Kilwa ni miongoni mwa maeneo nchini yenye magofu ya aina hiyo.

(a) Je Serikali inasema nini juu ya kuuzwa kwa gofu lililopo Bandarini Kilwa Kivinje?

(b) Je, ni lini Serikali Serikali itachukua hatua ya kulirejesha gofu hilo mikononi mwake?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bundara, Mbunge wa Kilwa, naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, sera ya Malikale ya Mwaka 2008 inatoa fursa kwa wadau mbalimbali kumili, kutumia, kuhifadhi na kusimamia malikale zilizopo katika maeneo yao. Aidha utekelezaji wa sera hii umezingatiwa katika sheria ya malikale Namba 333 fasili ya mwaka 2002 ambayo inafanunua fursa hiyo na kutoa mwongozo wa utekelezaji. Kwa sheria hiyo si magofu yote ni mali ya Serikali hata kama yameorodheshwa katika tangazo la Serikali kuwa ni urithi wa taifa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye (a(na (b), kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna gofu katika Bandari ya Kilwa Kivinje lililouzwa na Shirika la Ununuzi wa Mazao lijulikanalo kwa jina la Ilulu. Jengo hili liliuzwa kwa bwana Hamisi Bikwaje Mfanyabiashara ambaye alikuwa akitumia kama ghala la kuhifadhia mzigo.

Mheshimiwa Spika, (b), kama nilivyoeleza hapo awali, si kosa mtu binafsi kumiliki na kutumia jengo la kale, ingawaje ulitokea mgogoro wa muda mrefu uliofikia kuhatarisha amani kati ya wananchi wa Kilwa Kivinje na Mmiliki aliyeuziwa gofu hilo. Wananchi walihoji, iweje mtu binafsi ameuziwa gofu ambali ni mali ya wanakivinje kwa matumizi binafsi. Wananchi walifikia hatua ya kuzuia shughuli za biashara za mmiliki huyo kwa kufunga milango ya jengo hilo na kufanya makusanyo isivyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshachukua hatua za kulirejesha gofu hilo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ili litumike kama chanzo cha mapato kwa halmashauri kwa faida ya wananchi walio wengi. Makubaliano hayo yalifikiwa katika vikao mbalimbali vilivyowashirikisha Wizara yangu. Aidha Mkuu wa Wilaya ya kilwa bwana Abdallah Ulege alitangaza uamuzi huo katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kilwa Kivinje tarehe 8 Desemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, ni faraja yangu kwamba Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa, pia alishiriki katika muafaka huo na kupta fursa ya kuwahutubia wananchi ambao walipokea uamuzi huo kwa shangwe kubwa na kurejea kwa hali ya usalama na amani katika eneo hilo. *(Makofi)*

MHE. SELEMANI SAID BUNGARA: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa umekiri kwamba Ilulu imeuza gofu hilo ilihali gofu hilo ni la Serikali.

Je, Ilulu ilipata mamlaka wapi ya kuuza gofu hilo?

Kwa kuwa pia umekiri kwamba Serikali imechukua hatua ya kulirejesha gofu hilo katika Halmashauri ya Kilwa, Je, jibu lako huoni si sahihi kwa sababu mpaka sasa hivi kuna kesi tarehe 9 Julai, 2014 katika Kahakama Kuu ya Mtwara?

SPIKA: Mheshimiwa sasa kama kuna kesi mbona hatupaswi kujibu. Jibu sehemu ya kwanza.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Selemani Said Bungara, (a.k.a Bwege), kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, jengo lile halikuwa mali ya Serikali, lilikuwa linamilikiwa na shirika la ununuzi wa mazao lijulikanalo kwa jina la Ilulu. Kwa hiyo, walikuwa wana haki zote za kufanya watakalo.

Kwa hiyo waliliuza kwa mamlaka waliyokuwa nayo, lakini kilichojitokeza wananchi walikuwa na *interest* na lile jengo wakapiga makelele sana. Wizara Maliasili na Utalii, kwa

kushirikiana na Halmashauri walikaa vikao mbalimbali wakatengeneza utaratibu wa kuhakikisha kuwa lile jengo linarudi kwa wananchi.

Makubaliano waliyokubaliana ni kwamba Mahakama ilitoa Mamlaka kwamba yule mtu alipwe milioni thelathini na tano, na mpaka sasa hivi ameshalipwa milioni kumi na tano. Hata anavyosema kwamba kesi iko mahakamani, sawa, yeye ni Diwani katika eneo lile na lile jengo limekabidhiwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. *(Makofi)*

SPIKA: Swali la Nyongeza Mheshimiwa Mangungu, kwa sababu ni wa huko huko. *(Makofi)*

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningependa kujua kwamba Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ni kwa nini mpaka leo haikubali kutoa gawio la mapato yanayotokana na watalii wanaokwenda kwenye magofu ya Kilwa Kisiwani.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Murtaza Mangungu, swali lake la nyongeza, kama ifuatavyo.

Kuna mazungumzo ambayo yameanza kati ya Wizara yangu pamoja na Halmashauri ya Wilaya kuhusu namna tutakavyowagawia mapato. Nataka nimhakikishie tu kwamba mazungumzo haya tumefikia hatua za juu kabisa na muda si mrefu tutajua ni asilimia ngapi tutawapatia Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa muda wa Maswali umekwisha, niwatambue wageni. Waheshimiwa Wabunge mtatusaidia sana kama wageni wenu mnapeleka kwenye ofisi inayohusika kuliko kuandika kwa maandiko ambayo mengine hatuwezi hata kuyasoma, inakuwa shughuli. Kwa hiyo naomba, utaratibu ni huo, kama una wageni wako peleka ofisi inayohusika ili waandikwe vizuri, sasa kusoma soma hapa inakuwa si vizuri sana. Kwanza kabisa naomba niwatambue wageni wailioko hapa, kuna Mheshimiwa Diwani na Naibu Meya wa Mji wa Morogoro, Mheshimiwa Lidya Mbiaji, pia ni mdogo wangu mimi huyo, Naibu Meya wa Morogoro. *(Makofi)*

Wageni wengine waheshimiwa, kuna wageni wa Mheshimiwa Stephen Wassira, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu, ambao ni waasisi wa CCM (1997) wakiwa wanachama wa *TANU* na ambao kwa sasa ni wawakilishi wa Baraza la Wazee Mkoa wa Mara, wakiongozwa na Mzee Ramadhan Mawazo Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Mkoa wa Mara. Mzee Ramadhan Mawazo tunaomba asimame alipo, ahaa! Na wenzake, ahsante karibuni sana.

Kuna wageni wengine wa Mheshimiwa Wassira kutoka Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Daniel Zenda, Katibu Wilaya, Mkoa wa Vyuo vya Elimu ya Juu Dar es Salaam, hao nao wasimame walipo, ahaa, wako pale ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Naibu Waziri wa Fedha, ambao ni Ndugu Mtoka Bonaventura Nyabitwano na Ndugu Cecilia John Mihayo, kutoka Singida na hao wasimame walipo, ahsante sana naona mmoja tu.

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Juma Suleiman Nkamia, Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ambaye ni Ndugu Kenny Salvatory Festo, Mwenyekiti wa *Voice of Youth Mwanza,* huyu Ndugu Kenny yuko wapi? Ahaa! yuko pale, okay.

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Ezekiel Maige wakiongozwa na Ndugu Mabala Mlolwa, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kahama, naomba wasimame huyu na wenzake, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ambao ni wanafunzi 33 wa Shahada ya Kwanza ya Sayansi ya Afya ya Akili na Utengamao - kutoka Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa, kilichoko Lushoto, Mkoa wa Tanga. Naomba hawa wanafunzi 33 wasimame walipo, ahaa, ahsanteni sana, nashukuru sana, msome kwa bidii. *(Makofi)*

Tuna wageni sita (6) ambao ni makada wa CCM kutoka Mwanza nyumbani alipozaliwa mama Tunu Pinda, Mke wa Waziri Mkuu wakiongozwa na Mwenyekiti wa Vijana Mkoa wa Dodoma na hawa wageni pia wasimame, alaa, wako pale ahsante sana, ahsante sana.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Profesa Stephen Hilary Ngonyani (Maji Marefu - Profesa Maji Marefu) siyo Profesa Stephen, Profesa Maji Marefu Stephen Hilary, ambao ni viongozi wa *Tanzania Youth Against Drugs,* vijana wanaopambana na madawa ya kulevya, wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu David George na Ndugu Shaaban Salehe, hawa wenyewe wako wapi, wapambanaji, ahsante tunawatakia kazi njema, hilo ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Juma Njwayo, ambao ni wanafunzi 16 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, naomba na wenyewe wasimame walipo kama wamepata nafasi. Ahsante sana karibuni.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa John Mnyika, ambaye ni Ndugu Renatus Mrashani, Ndugu Mrashani yuko wapi, yuko pale, ahsante sana, karibuni sana.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa, ambao ni *Reverend Canon Elias Mwizagi,* Diwani wa Kata ya Biharamulo Mjini na Ndugu Linus Mayenje. Mheshimiwa Diwani yuko wapi, ahsante sana na Ndugu yake, ahsanteni sana karibuni sana.

Tuna wageni 39 wa Mheshimiwa Adam Kigoma Malima, Naibu Waziri wa Fedha kutoka Mkuranga Jimboni kwake ambao ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mkuranga Ndugu Omar Kungwa, sijui yuko wapi Mwenyekiti huyu, yuko pale. Yuko Ndugu Naima Malima - Mke wa Mheshimiwa Malima, yuko pale kwenye *Speaker's Gallery,* wako Madiwani 15 kutoka Kata mbali mbali za Wilaya ya Mkuranga, naomba Madiwani wote wasimame, ahsanteni sana Waheshimiwa Madiwani, ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, ambaye ni Ndugu Francis Joseph Nyerere, mdogo wake naye asimame alipo, ahsante, karibu. Tuna wageni wanane wa Mheshimiwa Dkt. Cyril A. Chami, ambao ni Ndugu Mouldine Castico kutoka CCM Makao Makuu akiambatana na familia yake na hawa nao wasimame walipo, ahsante sana, kweli wapo ni watoto wadogo wadogo huko.

Wageni waliokuja Bungeni kwa ajili ya mafunzo, tuna mabalozi 39 wa Maliasili wa kujitolea chini ya Taasisi ya *Rafiki Foundation* ya Arusha wakiongozwa na Mchungaji Ndugu Clement Matwiga, ambaye ndiye Mkurugenzi wa Taasisi hii. Hawa 39 naomba wasimame. Ahsanteni sana, karibuni sana.

Halafu tuna wanafunzi wengine 76 kutoka Chuo cha Kumbukumbu cha Hubert Kairuki kutoka Dar es Salaam ambao kwa sasa wapo kwenye mazoezi kwa vitendo katika Hospitali ya

Mirembe Dodoma. Madaktari hawa wanafunzi nao wasimame, wamekosa nafasi, nadhani watakuja baadaye.

Wanafunzi hamsini kutoka Chuo cha Biblia Kanisa la *Tanzania Assemblies of God* cha Dodoma, na hao kama wapo wasimame, ahsanteni sana, haya, tunawatakieni mafunzo mema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tumekuwa na matangazo ya wageni wengi, kuna huyu mmoja ambaye, haya kuna wageni wa Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mbunge wa Solwa, yuko Ndugu Nicodemus Kuboja, huyu Ndugu Kuboja ni Mwenyekiti wa Wachimbaji Wadogo Wadogo wa Mkoa wa Shinyanga. Yuko wapi Bwana Kuboja, ahaa! Yuko pale, yuko Ndugu Joseph Mathias, Mwenyekiti wa Wachimbaji Wadogo Wadogo wa Kitotolya na yeye asimame, ahsante sana.

Kuna Ndugu Pastory Nindwa Mhasibu *SACCOS* Makitolyo, ahsante sana, karibuni sana, tunawatakia kazi njema. *(Makofi)*

Katibu, tunaendelea na kazi. Katibu.

UCHAGUZI

Uchaguzi wa Wajumbe Wawili wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi – Muhimbili
na
Uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi ya Utawala ya Chuo cha Ufundi Arusha

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mwongozo wa Spika

SPIKA: Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ninaomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7). Wakati mjadala wa Bajeti unaendelea kuna maeneo mengi ambayo kama Wabunge na mimi mmojawapo, tulipokuwa tunajadili Bajeti ya Viwanda na Biashara, nilikuwa nimeshika Shilingi kuhusiana na suala la Wamachinga na Serikali ilisema itatoa Kauli kabla Bunge halijaisha.

Mheshimiwa Spika, nimesoma ratiba naona hakuna nafasi ya Kauli ya Serikali, nilitaka kujua Mwongozo wako, TAMISEMI walisema wangetuelekeza namna gani mambo haya yatafanyika kwa sababu Wamachinga nchi nzima wamekuwa wakipata matatizo, hususan Iringa Mjini na maeneo mengine.

Kwa hiyo, nilitaka nijue, naona Bunge linakwenda ukingoni. Serikali inaleta tamko gani kuhusiana na tatizo hilo kabla hatujaondoka hapa kwa sababu tulikuwa tumetoa Shilingi. *(Makofi)*

SPIKA: Haya, ahsante, naomba ukae, huo ni Mwongozo. Tutajibu wakati muafaka, tunaendelea, Katibu.

KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, maelezo ya Msimamizi wa Uchanguzi.

SPIKA: Naomba utulivu na watu wakae sehemu zao. Katibu endelea, Mkurugenzi.

KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo mafupi kuhusu utaratibu wa kujaza nafasi za nasibu za Baraza la Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili na Bodi ya Utawala ya Chuo cha Ufundi Arusha.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowatangazia tarehe 19 Juni, 2014 kuwa leo siku ya Jumanne, tarehe 24 Juni, 2014 kutakuwa na Uchaguzi wa kujaza nafasi mbili za Wajumbe la Baraza la Chuo Kikuu cha Afya – Muhimbili na nafasi moja kwa ajili ya Bodi ya Utawala ya Chuo cha ufundi Arusha.

Mpaka jana tarehe 23 Juni, 2014 saa 10.00 jioni Wabunge waliorejesha fomu ni hawa wafuatao.

Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi - Muhimbili nafasi zilizokuwa zinaombwa ni mbili, waliorejesha fomu ni wawili, ambao ni Mheshimiwa Beatrice Shelukindo na Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utawala ya Chuo cha Ufundi, Arusha nafasi iliyotakiwa ni moja, aliyerejesha fomu ni mmoja, naye ni Mheshimiwa Athumani Rashid Mfutakamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Masharti ya Kanuni Namba Saba, Nyongeza ya Pili (Namba 7 (2) wagombea hao wamepita bila kupingwa. *(Vigelegele/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Vigelegele/Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana. Kwa hiyo ninawatangaza Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimwia Dkt. Maua Daftari, kwamba sasa ndio watakaokuwa wawakilishi wetu katika Chuo Kikuu cha Afya, Sayansi Shirikishi Muhimbili.

Halafu ninamtangaza Mheshimiwa Eng. Athumani R. Mufutakamba, kuwa Mwakilishi wetu katika Bodi ya Utawala ya Chuo cha Ufundi, Arusha. Kwa hiyo, ninawapongeza kwa nafasi mlizoshika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge miongoni mwenu kuna wanaoleta vikaratasi bila kuandika. Ninao wageni wa Mheshimiwa Pauline Gekul, ambao ni Fausta Philipo, huyu ni dada yake. Yupo pia na mwanawe Irenelanta Slaa. Ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2013 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo ni siku ya kukamilisha shughuli hizi. Kwa hiyo, tumekuwa tunajadili kupitia sekta mbalimbali katika hotuba hizi. Sekta nyingine watoa hoja hawataweza kuzijibu. Kuna wahusika wenyewe. Kwa hiyo kuna Mawaziri wanaohusika, hivyo basi hao ndio nitakaoanza nao kwa leo hii. Nitaanza na Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Titus Miengeya Kamani, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, watatumia dakika kumi kila mmoja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao. Nianze moja kwa moja na kuunga mkono Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala kubwa ambalo lilizungumziwa na Wabunge wengi, suala hili la *Pay As You Earn*. Kwamba Tanzania tunawatoza kodi wafanyakazi, kodi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hiyo hoja ni hoja ya Vyama vya Wafanyakazi, chini ya *Umbrella* ya *TUCTA*. Mheshimiwa Chiligati alinisaidia kwa kiasi fulani, kwamba mwaka 2008 *(PAYE)* ilikuwa ni asilimia 18. Tulipokaa na *TUCTA,* yaani Vyama vya Wafanyakazi, waliomba kwamba tupunguze kidogo kidogo na tufikie *single digit*. Kwa hiyo, kuanzia mwaka 2008 tumepunguza na sasa hivi tumefikia asilimia 12. Lengo letu ni kufikia asilimai 9 yaani *single digit* kama Wabunge walivyoshauri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *(PAYE)* huwa hatupangi sisi peke yetu na mishahara huwa hatupangi peke yetu. Huwa kuna Baraza la Majadiliano katika Utumishi wa Umma, kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma Sura 105. Kwa hiyo, sisi tunakaa na vyama vya Wafanyakazi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninawasihi, mkitulia tutanufakika na elimu hii tunayostahili. Lakini ninaona kila mtu anafanya shughuli zake humu ndani ya Ukumbi wa Bunge.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, tunajadiliana. Tukishajadiliana tunakubaliana, ya kwamba kima cha chini, kiwe kiasi gani na *(PAYE)* tunaipunguza kwa kiasi gani.

Kwa hiyo tusifikirie kwamba tunaopanga mishahara ni Serikali peke yetu. Huwa tunashirikisha vyama vya Wafanyakazi, na mara ya mwisho tumekaa na Baraza la Majadiliano tarehe 5 Mei, 2014, tumepanga kima cha chini ya mshahra tukakubaliana kwa pamoja na kupunguza asimia moja ya *(PAYE)*. Kwa hiyo, tumepunguza asilimia moja ya *(PAYE)*. Lakini *at the same time* tumeongeza kima cha chini cha mshahara kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, niseme ya kwamba kwa awamu hii, tumeongeza sana kima cha chini cha mshahara. Kwa mfano mwaka 2013, ilikuwa asilimia 41. Mwaka huu siwezi nikasema lakini tumepunguza *(PAYE)*na tumeongeza kima cha chini cha mshahara na tukakubaliana kabisa na vyama vya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge msilione kwamba hili hatulifanyii kazi. Vyama vya Wafanyakazi vinafanya kazi vizuri sana na tunaelewana nao vizuri sana. Ndiyo maana unaona sasa hivi hakuna malalamiko kwa sababu tunakaa nao mara kwa mara kujadiliana kuhusu maslahi ya wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mwaka huu tu Chama cha Walimu, kwa mwaka 2013 tulikaa nao mara tano, kujdiliana maslahi na jinsi gani ya kuboresha huduma za Walimu. Chama cha Walimu kwa mwaka huu pia kuhusu mambo ya malimbikizo na madai mengine. Tulikaa pamoja, tulihakiki pamoja na tunafanya kazi kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu ucheleweshaji wa mishahara. Serikali kuanzia mwaka 2006, tumejipangia kwamba mshahara uwe unatoka tarehe 25 kwa kila mwezi. Kwa hiyo, kuanzia tarehe 23 mpaka tarehe 25 kila mwezi, mshahara uwe unatoka. Lakini kuna baadhi ya miezi, mishahara inachelewa kwa sababu zifuatazo. Moja, miezi ambayo tunaajiri Walimu. Miezi ambayo tunaajiri Madaktari, kwa kuwa wanaripoti kwa wakati tofauti tofauti.

Kwa hiyo, hata *Pay Roll* inachelewa kutengenezwa. Kwa hiyo, unakuta mshahara unachelewa. Kwa mfano katika mwezi uliopita, mwezi Mei na mwezi Aprili, 2014 mshahara ulichelewa kwa sababu ilibidi tuvute *Pay Roll* mpaka tarehe 14 Aprili, 2014 ili tuweze ku-*accommodate* Walimu wengi zaidi na niunganishe hapo hapo kuhusu Walimu wapya ambao hawakupata mishahara yao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi katika mfumo wetu yaani ule wa *Loson Version 9.0* au tunauita Mfumo wa Taarifa za Watumishi pamoja na Mishahara. Mfanyakazi akiripoti tu kazini, hujaza *personal particulars* ikiwa ni pamona na vyeti vyake vya kuzaliwa. Pamoja na vyeti vyake vya masomo, vinaambatanishwa kwa pamoja na kuingizwa kwenye mfumo. Iwapo hakujaza hizo *Personal Particulars* na kama hakuleta vyeti *orginal* mfumo wetu una-*reject* na kama taarifa zake zinakuwa tofauti. Pengine mwaka wa kuzaliwa unakuwa tofauti na ulioko kwenye vyeti vyake. Mfumo wetu una-*reject*.

Ikitokea hivyo, mfanyakazi huyo hawezi akapata mshahara kwa wakati. Ndiyo maana utakuta Walimu wengi hawakupata mshahara kwa wakati kwa sababu wengi hawakuleta vyeti vyao *orginal,* kwa hiyo kwa mwezi husika, alikuwa hawezi akapata mshahara. Wengine walileta vyeti ambavyo vinatofauti, kwa maana ya cheti cha Sekondari na cheti cha Ualimu na cheti cha kuzaliwa vinatofautiana. Hivyo mfumo wetu una-*reject*. Kwa hiyo tunarudisha taarifa kwa mwajiri ili aweze akafanya masahihisho. *By the time* anarudishiwa kufanya masahihisho, sisi *Pay Roll* yetu imeishapita.

Kwa hiyo wengi wa Walimu ambao hawakupata mshahara ni wale walioripoti baada ya tarehe tarehe 15, Aprili, 2014 yaani wakati tumeishafunga *Pay Roll* na wengine ni kwa sababu hizo ambazo labda hakuambatanisha cheti cha kuzaliwa. Hakuambatanisha cheti *original* na utakuta kwenye mfumo wetu inaonyesha kabisa kwamba huyu *system* imem-*reject* kwa sababu hana cheti cha kuzaliwa. Huyu ime-*reject* kwa sababu taarifa zake haziko sahihi. Kwa hiyo, baadhi ya Walimu kwa kweli wamepata matatizo ambayo hawakupata mshahara kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la Igunga lilikuwa ni tofauti kidogo. Ni kwamba kuna baadhi ya Walimu, baada ya kusahihisha zile taarifa zao na kuingiza kwenye mfumo wa *Human Capital Management Information System* pale Utumishi zilikataa kuingia. Kwa kuwa zilikuwa zimechelewa, kwa hiyo Walimu hao 66 wakapata matatizo ya kutopata mshahara. Lakini tumeisha-*reconcile* ilikuwa ni tatizo la mfumo na siyo tatizo la Mwajiri au tatizo la Utumishi, kwa hiyo hilo tumeishalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu malimbikizo ya mishahara kwa mwaka huu 2014, tumelipa jumla ya shilingi bilioni 45.1 mpaka kufikia mwezi Mei, 2014 na kiasi kilichopangwa kulipwa kama malimbikizo ni shiingi bilioni 50. Kwa hiyo, utakuta tumefikia lengo *at least* la asilimia 90,

zilizobakia kwenye mfumo ni shilingi bilioni 5 tu. Kwa hiyo Serikali inajitahidi sana kuhakikisha kwamba tunalipa hayo madeni.

Suala lingine ni suala la chombo kimoja Uajiri cha Walimu. Ninaomba nimwarifu Mheshimiwa Mama Margareth S. Sitta, kwamba ule ugomvi wetu ninaona wetu ninaona sasa hivi umekwisha. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba chombo kimoja cha Walimu kitaanzishwa. Sasa ninaomba nieleweke kwamba ile ahadi yangu niliyoitoa kwamba nitakutana na Wadau yaani Waheshimiwa Wabunge na Kamati ya Mheshimiwa Margareth Sitta, sintakutana nao katika kipindi hiki. Nitakutana nao wakati tunakiunda hicho chombo ili kiwe cha aina gani, ili niwashirikishe, ili tuweze tukaaunda chombo ambacho kitasaidia kwa kiasi kikubwa kwa upande wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa tatizo la ajira kwa kweli tatizo la ajira ni la nchi nzima. Niwaambie tu kwamba *ratio* ya ajira ni kwamba ni moja kwa tatu mpaka moja kwa tano kwa Tanzania. Kwa hiyo, pengine mtaniuliza kwamba lile la Uhamiaji lilikuwaje. Lile upande wa vyombo vya Ulinzi na Usalama mfumo wao ni tofauti na mfumo ambao tunaajiri katika Utumishi wa Umma au Watumishi wengine.

Lakini nafasi sasa hivi tumezitoa kwa wingi na wanao-*apply* ni wengi na wale wanao *qualify* kwa mara nyingi tunawachukua sisi katika ile Sekretarieti ya ajira, tunawachukua lakini tunawakeka kwenye *Data Bank* kwa wale wanaofaulu. Kwa hiyo, nafasi zikitokea, tuna wa *off load,* badala ya kuwafanyia *interview*.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, kengele ya pili, imegonga.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, atafutiwa na Waziri wa Uchukuzi. Samahani ninafanya mabadliko kidogo. Waziri wa Uchukuzi, atasubiri na badala yake atakuja Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ahsante ili na mimi nichangie katika hoja hii iliyoko mbele yetu na mimi nianze kwa kuunga mkono Bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengi sana yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na Sekta hizi za Mifugo na Uvuvi. Hii inaonyesha ni kwa jinsi gani Watanzania wanavyozidhamini sekta hizi katika uchumi na maisha ya wananchi. Kwanza labda nianzie na eneo moja ambalo ni kuhusu mchango wa sekta hizi katika pato la taifa.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine sekta hizi zinaonekana kama vile hazichangii kwa kiasi kikubwa lakini ninafikiri ni kutokana na jinsi zinavyofanyiwa mahesabu yake kwa sababu sekta hizi ni za uzalishaji. Zinavyozalisha zile bidhaa za msingi zinaingizwa kwenye viwanda. Sasa viwanda vinavyochakata unakuta kwamba makadirio ya hesabu ya mazao ya mifugo na uvuvi yanaonekana kama mchango wake uko Wizara ya Viwanda na inaonekana kama hayachangii kwa kiasi kikubwa.

Lakini saa tunawasiliana na Tanzania *Bureau of Statistics* ili kuweka takwimu sahihi. Kwa sababu mazao kama vile ngozi. Samaki, maziwa yanavyoachakatwa na viwanda basi hesabu yake haionekanai kama imechangiwa na sekta hizi moja kwa moja. Lakini ni dhamira ya Serikali

kujitahidi katika nyanja yoyote ile kuhakikisha kwamba sekta hizi zinachiangia kwa kiasi kikubwa zaidi katika pato taifa.

Mheshimiwa Spika, lilizunguzwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi suala la kuvutia uwekezaji katika sekta hizi, kwamba labda hazivutii sana. Ni kweli kwa muda sasa zimekuwa zikivutia kidogo kidogo. Lakini kwa muda wa hivi karibuni, kuna mvuto mkubwa sana. Kwa sababu sekta hizi zinatangazwa. Kitaifa na kimataifa, na tumeweka vivutio vya namna mbalimbali ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanawekeza mitaji mikubwa katika sekta hizi. Ni muhimu sana kuwekeza kwa maana ndiyo eneo litakalovutia masoko. Sasa hivi kwa mfano kwa viwanda vya nyama. Licha ya viwanda ambavyo vipo.

Lakini sasa hivi kuna hatua nzuri sana zinaendelea za kujenga kile Kiwanda cha nyama cha Ruvu, kwa kupitia Shirika letu la *National Ranching Company*. Lakini sasa hivi kuna timu ya taasisi za Tanzania iko India, kuwasiliana na Kampuni kubwa ya Alana, ambayo na yenyewe inataka kuanza kujenga kiwanda kikubwa cha nyama hapo hapo maeneo ya jirani na Ruvu, tayari eneo tumeishawapatia.

Lakini vilevile wanaangalia uwezekono wa kukifufua kiwanda cha Nyama cha Mbeya, tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, imeishatoa idhini hatua za uwekezaji ziendelee. Lakini kuna kiwanda kinachojengwa Shinyanga na Zhngwai ya China. Kuna kiwanda cha Morogoro pale Tendaji, na kiwanda kingine kimejengwa Magu cha Alpha. Lakini kuna viwanda ambavyo viko kwenye mchakato sasa hivi wa kuendelea na ujenzi ikiwemo kile cha Iringa, Mwanza na Kule Kagera kupitia Kampuni ya *Agro Ranching*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuna mvuto mkuwba sana na tunapenda tutumie nafasi hii kuwahamasisha wananchi wa Tanzania ambao wanaezawakawekeza mitaji yao katika maeoeno haya. Mifugo iko mingi, na soko liko kubwa.

Lakini vilevile sasa hivi kuna viwanda tayari saba vimeishafunguliwa vya Ngozi na kuna kiwanda kingine kitafunguliwa mwezi Julai, kule Arusha. Viwanda hivi sasa tunavihamasisha, kutoka katika ile hatua ya uchakataji wa hatua ya awali ili waingie kwenye *final products,* ambazo hizi zitajenga ajira kubwa na vile vile kuongea mapato kwa taifa letu.

Vile vile wako wasindikaji wadogo wadogo ambao na wenyewe wanavyo viwanda hivi vya usindikaji wa ngozi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa zao la Maziwa. Tayari tunavyo viwanda 74 katika maeneo mbalimbali vyenye ukubwa tofauti tofauti na Watanzani wengi wameonyesha hamasa kubwa na tunaendelea kuwahamasisha.

Kwa mfano wiki mbili zilizopita tulikuwa kule Musoma kwenye wiki ya Maziwa ambako tumetia hamasa kubwa sana, kuvutia Wawekezaji katika masuala ya Maziwa. Lakini haya yatafanikiwa zaidi kama vilevile kuna mashamba makubwa ya uzalishaji.

Kwa hiyo, sasa hivi vilevile tunaendelea kuvutia tayari kuna shamba kubwa. Mashamba makubwa yanafunguliwa kule Njombe, Tanga kwa ajili ya Ng'ombe wa Maziwa na Mara. Lakini vilevile katika Mbuzi na Kondoo. Kule Kagera sasa hivi kuna Kampuni kubwa ya Ubia wa *NARCO,* Kampuni ya Kimarekani na Urabuni, wameanzisha shamba kubwa katika mashamba yetu ya Kagoma, Kikurura na *Mabale Complex*.

Mheshimiwa Spika, vilevile wapo wafugaji wadogo wadogo ambao wanajifunza kutokana na uzalishaji huo wa kisasa. Lakini vilevile hii inaenda katika sekta zote za uvuvi. Katika

utengenezaji wa maboti, ufugaji wa samaki na Wabunge wengi sana wameongelea suala la ufugaji wa samaki, ambao tunatafuta ufumbuzi, licha ya kwamba tuna fedha kwenye Bajeti ya kuhamasisha ufugaji wa samaki, lakini tunatafuta fedha zaidi nje ya Bajeti hii ili kuona kwamba tunaweza tukavutia Watanzania wengi zaidi wakaingia katika ufugaji wa samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limeongelewa sana suala la migogoro kati ya Wafugaji na wakulima na watumiaji wengine wa ardhi. Serikali haijafumba macho kabisa katika hili suala. Kwanza kuna juhudi kubwa zinazoendelea sasa. Lakini pamoja na hizo juhudi, ninapenda kuwahamasisha wananchi wote ikiwa ni pamoja na wafugaji. Mambo ya kulalamikia maeneo ya kuchungia.

Kwanza ni lazima tujitathmini wenyewe katika maeneo yetu tuliyonayo, katika ngazi ya Kaya, katika ngazi ya kijiji, ya Wilaya na Mikoa. Kwa maana kwamba ni lazima tukubaliane, kwamba mifugo ni shughuli muhimu na inahitaji maeneo maalum kwa ajili ya maendeleo.

Lakini kama Serikali tumeafikiana na kuangalia upya. Maeneo ya mashamba yaliyokuwa ya Serikali ambayo hayatumiki vizuri kwa ajili ya maendeleo ya Mifugo yaweze kurejeshwa kwa wananchi kwa ajili ya kusaidia kupunguza uhaba wa maeneo ya malisho ya mifugo.

Lakini vile vile mashanba yetu ya *NARCO,* ambayo yalikuwa hayatumiki vizuri na yenyewe tunayangalia.

Lakini tumeafikiana vile kuangalia maeneo yaliyokuwa mwanzoni kama maeneo ya uhifadhi ambayo yamepoteza sifa ya kuwa maeneo ya hifadhi, ili yaweze kutumika kwa ajili ya maendeleo ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wamezungumzia sana suala la fidia kwa wananchi ambao mifugo yao imepotea wakati wa *operation.* Sasa hivi kuna Tume ya Kimahakama ambayo inaendelea. Kwa hiyo, tulidhani ni vema tukasubiri Tume hii ikatoa taarifa yake, kwa sababu itatoa maelekezo ya namna ya kushughulikia masuala ya namna hiyo.

Lakini tutakuwa na mkutano mkubwa wa wadau wa kuangalia kwa ujumla jinsi sekta ya mifugo inavyoweza kujenga uchumi wa nchi hii na kujenga uchumi wa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uvuvi, limezunguzwa sana namna gani Uvuvi, hasa uvuvi wa Bahari Kuu unavyoweza kuongeza mapato kwa Taifa letu. Tumefanya kazi kubwa ya kuangalia namna ya kuvutia na kuhakikisha kwamba kwanza Meli zinazoingia kwenye Bahari Kuu ya Tanzania zinalipa ushuru inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, katika mamlaka ya bahari kuu kuna vyombo ambavyo tayari vimeshafungwa vya kuweza kuangalia meli zote zinazokuwa kwenye maeneo yetu kuhakikisha kwamba zina kibali na sasa tuna mawasiliano na Wizara ya Ulinzi kwa sababu suala hili la kuingia kwenye maeneo ya ardhi ya Tanzania bila kibali ni suala la kiusalama vile vile ili tuwe na mfumo wa kuweza kufuatilia kuhakikisha kwamba meli zinazoingia kwenye maji yetu zinalipa tozo inayostahili.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile, tunapenda kuwavutia Watanzania kwa sababu kulipia mapato ya leseni kwa meli za uvuvi ni kitu kidogo sana, mapato makubwa yatakuwepo kama bidhaa zile zinachakatwa ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, tunataka tuvutie Watanzania wengi waingie huko, lakini tunaangalia tatizo moja ambalo nilikuwa nasema la *levy* ya mafuta

kwamba linakwamisha kuvutia Watanzania kuwekeza huko. Tunaongea na Wizara ya Fedha tuone ni namna gani hili tunalisimamia ili tuwavutie Watanzania wengi waingie huko.

Kuna bandari ya uvuvi…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante!

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mathias Chikawe atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja ya bajeti ya Taifa. Nianze kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na ni bajeti ambayo nafikiri itatutoa hapa tulipo na kutupigisha hatua moja zaidi mbele.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia sekta ambayo naiongoza ya usalama ndani ya nchi hii na michango yao kwa ujumla imekuwa ikielekeza kuonesha changamoto zinazokabili Idara mbalimbali ambazo ziko chini ya Wizara yangu.

Wizara yangu ina Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Uhamiaji na Jeshi la Zimamoto na majeshi haya yanafanya kazi kwa muda wa saa 24 kwa siku saba kila mwaka. Ni majeshi ambayo yako vitani muda wowote na ni majeshi ambayo yana watu wengi na yako karibu sana na wananchi na yanagusana sana sana na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni majeshi ambayo changamoto zake nyingi wananchi wanazifahamu na Waheshimiwa Wabunge wamezisema. Yapo matatizo yanayotokea baina ya majeshi haya, yanasuguana wakati mwingine na wananchi ndiyo maana sisi tupo hapa kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, zipo hoja chache sana mahususi, ukiacha kwamba Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia matatizo ya nyumba za watumishi, majengo machavu, vifaa haba vya kutendea kazi majeshi haya na kadhalika. Hizo ndiyo changamoto ambazo sisi tunapaswa kuzikabili.

Mheshimiwa Spika, lakini zipo hoja ambazo zimezungumzwa ambazo ni chache, lakini ni muhimu zikapata au zikatolewa maelezo na nyingi hasa zilizungumzwa jana, zikihusu vitendo vya uhalifu ambavyo vimefanywa na ambapo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanadhani pengine hakuna hatua zilizochukuliwa dhidi ya watendaji wa vitendo hivyo.

Moja, kulikuwa na kesi ambayo imezungumzwa ya mfungwa kumbaka mtoto hapa Mjini Dodoma. Ni kweli kesi hii ipo, mnamo tarehe 9 Juni, 2014, katika maeneo ya Kambi ya Polisi hapahapa Dodoma mfungwa mmoja alimbaka mtoto mdogo mwenye umri unaosadikiwa kuwa ni miaka 10, mwanafunzi wa Shule ya Msingi. Mfungwa huyu alikuwa amehukumiwa kule Singida kwa kosa la kunajisi na akahukumiwa miaka 30. Sasa Singida hakuna Magereza ya muda mrefu ya kuweka watu kwa vifungo vya muda mrefu, kwa hiyo, mtu huyu akahamishiwa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, akiwa hapa ndani ya gereza akaonesha mwenendo mzuri sana, alifanya kazi vizuri, akaonesha nidhamu ya hali ya juu, kwa hiyo akaaminiwa na kuitwa Mnyampara mle ndani. Siku moja wakachukuliwa yeye na wenzake wawili kwenda kufanya kazi kwenye Kambi ya Polisi, hapo ndipo alipotenda tendo hilo na huyu bwana amekamatwa kwa sababu yuko gerezani, kilichotokea ni kwamba amepelekwa Mahakamani kwa kushtakiwa kwa kosa la kubaka na kesi yake ni ya Jinai, namba 106 ya 2014 na itatajwa tena tarehe 8 Julai.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, walikuwa wanadhani kwamba labda Magereza imezuia mtu huyu asishtakiwe, lakini si kweli kwani mtu huyu ameshtakiwa na kesi yake ni hiyo na Askari Polisi ambao walikuwa wamewachukua kuwapeleka kwenye hiyo kazi, nao pia wamechukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria na taratibu za Polisi na wamefunguliwa mashtaka ya kijeshi. Sasa hilo lilikuwa ni moja ambalo lilizungumzwa jana na likasemwa kwamba Wizara haifanyi lolote kuhusu jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, tukio lingine ni la kubaka mtoto vile vile ambalo lilitokea Musoma, mtoto mdogo kabisa wa mwaka mmoja na miezi kumi. Hili pia lilisemwa ndani ya Bunge hili na likasemwa kwamba Polisi hawajafanya lolote.

Ukweli ni kwamba, mtuhumiwa ambaye ni kijana wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari huko, huyu ni mtoto wa shemeji yake ambaye aliachwa naye nyumbani ili amtunze, basi akatenda kitendo hicho na kumjeruhi mtoto huyo vibaya. Kijana huyu amekamatwa na majirani na sasa hivi yuko Mahakamani ameshtakiwa kwa kosa la kubaka. Kwa hiyo, hatua zimechukuliwa na Jeshi la Polisi kwa kumpeleka Mahakamani kama inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, jana pia Mheshimiwa Mbunge wa Micheweni alizungumza kuhusu Polisi ambaye alikamata mtu akiwa na tindikali, halafu akamwambia aimwage hiyo tindikali kwa maana ya kutaka kumlinda yule mtu. Sasa taarifa nilizopata ni tofauti kidogo, kwani taarifa za awali zinaonesha kwamba siku za karibuni kumetokea mgogoro kati ya Polisi Micheweni na wanafamilia wa familia fulani ya Mheshimiwa Bihindi ambaye ni Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wanagombea ardhi.

Mheshimiwa Spika, Polisi wana ardhi yao, wana hati yao na hii familia nayo ilipata kipande cha ardhi ya urithi wakagawana gawana, ndugu wengine wakajenga na huyu Bihindi hakujenga, sasa Polisi walipoamua kujenga sehemu yao ndiyo ukazuka ugomvi kati ya Polisi na familia hii.

Mheshimiwa Spika, hatua tulizochukua kwanza ni kuhakikisha kwamba Polisi hati yao ipo *intact,* tukawaambia hawa mabwana kama wana matatizo fungueni jalada, halafu itachunguzwa kesi yao na kama kuna kesi tutakwenda Mahakamani, watatoa vielelezo vyao kwamba mpaka wao unaishia wapi na kadhalika. Sasa ndiyo ikazuka hii kesi ya kusema kuna Polisi ambaye amekamata mtu na tindikali halafu akaimwaga.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba hatuamini kwamba ile ni tindikali, lakini pili tumechukua hatua kuhakikisha kwamba Mkemia Mkuu wa Serikali anaichunguza na kuona kama je, ni tindikali kama inavyodaiwa? Polisi walikuwa hawaamini kama ni tindikali ndiyo maana ikamwagwa, lakini kama wananchi wanadhani kama ni tindikali, basi ushahidi utapatikana baada ya kupata maelezo ya Mkemia Mkuu wa Serikali na akishasema kama ni tindikali, basi tutachukua hatua za kinidhamu na kisheria dhidi ya Polisi huyu ambaye inasemekana amemwaga tindikali ikiwa kama ni ushahidi. Kwa hiyo, jambo linaloendelea pale sasa hivi ni uchunguzi unaofanywa na Mkemia Mkuu kuthibisha kama hiyo ni tindikali, lakini sisi tunaamini kwamba hiyo haikuwa ni tindikali.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie moja la mwisho ambalo inaonekana kama ni mgogoro baina ya *NIDA* na *NEC* kwenye ununuzi wa mashine za kibailolojia kwa ajili ya vitambulisho vya Taifa na kwa pia kwa ajili ya Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, vyombo hivi viwili vyote ni vya Serikali na vyote vina majukumu ambayo yangeweza kusemwa yanafanana, lakini kila mtu mahitaji yake ni tofauti. Anapotengeneza kitambulisho cha Taifa *NIDA* anahitaji taarifa tofauti na *NEC,* naye anahitaji taarifa tofauti. Kwa hiyo, kila mmoja akawa anajaribu kwenda kufanya peke yake, lakini baadaye Serikali ikasema hapana, kwa sababu *at the end of the day* mnatengeneza *database* ya Watanzania na *NEC* ninyi mnataka *database* ya wapiga kura, basi fanyeni kazi kwa pamoja, mnunue vyombo vinavyofanana ili taarifa ziingie kwenye *database* moja wote mtaitumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndiyo sasa hivi *NIDA* na *NEC* wanafanya kazi hiyo, watanunua hizo zinaitwa *Mobile Enrolment Units* ambazo zitawasaidia *NIDA* na *NEC* na *NEC* wakimaliza *NIDA* wataendelea na vifaa hivyo hivyo. Kwa hiyo, Serikali tulichofanya ni kujaribu kuweka nguvu kwa pamoja ili kuifanya kazi hii ionekane ni ya Serikali badala ya kuonekana ni ya *NIDA* peke yake au *NEC* peke yake.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwashukuru tu Waheshimiwa Wabunge, kwani safari hii hata bajeti yangu mmeipitisha vizuri kwa sababu mnatambua changamoto zinazokabili idara ambazo zipo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru kwa nafasi hii. Kama Waziri wa Kazi na Ajira naomba kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia suala hili wakati wa kuchangia bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia, naomba nikubaliane na wengi kwamba ajira ni tatizo, mnaweza kuita jina lolote, lakini ajira ni tatizo la Kitaifa na Kimataifa na tunajua *unemployment rate* ya kwetu mwisho ni 11.7% lakini sasa hivi tupo tena kwenye utafiti wa nguvukazi ili kujaribu kuona *unemployment rate* imepanda au imeshuka kwa kiasi gani, tutashukuru Mungu kama itakuwa imeshuka.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba katika utafiti wa ajira na mapato ambao umefanywa mwaka 2012, ulionesha kwamba, kuna ongezeko la ajira kwa 13.8% kwa vijana kati ya miaka 15 mpaka 24 na hizi ni ajira za muda mrefu ambazo zinapelekea kazi ya staha. Kazi ya staha ni ile ambayo kwanza ni kazi ya muda mrefu na ni kazi ya kipato kizuri, lakini ni kazi ambayo inampa mfanyakazi hifadhi ya jamii na ni kazi ambayo inapunguza *unemployment rate*.

Mheshimiwa Spika, pia tunajua kwamba ajira zipo katika sekta mbili, sekta rasmi na sekta isiyo rasmi. Sekta rasmi inahusisha sekta ya umma kwa maana wale wanaoajiriwa na Serikali na sekta binafsi ni ambayo inahusisha viwanda na watu binafsi. Sasa katika utafiti huo ilionekana kwamba sekta binafsi iliongezeka ajira kwa 64.2% na sekta ya umma kwa 35.8%.

Mheshimiwa Spika, hii ina maana gani? Hii ina maana kwamba sekta binafsi ndiyo mwajiri mkubwa na lazima tukubali, sekta ya umma kama alivyosema Mheshimiwa Celina ina

limitations zake, inategemea uchumi umekua kiasi gani, nafasi za ajira zimeweza kutengenezwa kiasi gani, lakini sekta binafsi kila mahali na kila nchi duniani kote ndiyo inayotengeneza ajira na kwa kutambua hilo Serikali imefanya nini?

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo Serikali imeona iweke mazingira rafiki kwenye sekta binafsi kwa maana ya wawekezaji. Imeweka mazingira mazuri katika miundombinu kwa maana ya barabara, kwa maana ya Nishati na Madini, kwa maana ya mawasiliano na kwa kweli ndiyo maeneo ambayo yameingizwa kwenye *Big Results Now* na matokeo yameanza kuonekana.

Mheshimiwa Spika, ningekuwa na nafsi ningeweza kutaja takwimu zoe za ajira zilizotokana na kuongeza uwekezaji katika nchi yetu. Hii ina maana basi, wananchi na wanasiasa tusiwabeze wawekezaji kwa sababu hawa kazi yao ni kutusaidia kutengeneza ajira na si maadui. Kwa hiyo, kwa kweli tuwe pamoja na Serikali tunapozungumzia sala la uwekezaji katika maeneo yote kwa ajili ya kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia hapa nchi za *South East Asia* za akina Singapore, Vietnam, Thailand, Malaysia, ni kwa sababu sasa hivi uwekezaji kwa mfano, China ambayo sasa hivi mishahara ya wafanyakazi ni mikubwa, hakuna anayevutiwa kupeleka huko uwekezaji kwa sababu watalipa mishahara mikubwa. Kwa hiyo, uwekezaji unakwenda katika hizi nchi ambazo ni za *South East Asia* kwa ajili ya kuwapata *at least cheap labour* na wana *outsource*.

Mheshimiwa Spika, hata America na nchi za Magharibi zina-*outsource* katika hizi nchi na kwa kukumbatia huo uwekezaji ndiyo maana fursa za ajira zinaongezeka. Kwa hiyo, nafikiri niliseme hili, *of course the lowest* nchi ambayo ina *unemployment rate* ambayo ni ya chini kabisa ni nchi ya Qatar duniani, ndiyo ambao ina *lowest unemployment rate* ya 0.5% kwa maana kwamba katika watu 200 ni watu wawili tu hawajaajiriwa, lakini hiyo ni *peculiar*!

Mheshimiwa Spika, lakini kuna nchi kwa mfano, *South Africa,* ni nchi yenye uchumi mkubwa sana katika Bara la Afrika na katika nchi 50 zenye uchumi mkubwa ni *South Africa,* lakini *unemployment rate* ya *South Africa* ni 24.9%, nimesema sisi tuliyonayo ni 11.7%. Kwa hiyo, kitu ambacho kinaongeza ajira ni uwekezaji, lakini pia kama tulivyosema katika sera yetu ajira kwamba Serikali itashirikiana na wadau wengine katika kutoa fursa za ajira na wadau ni pamoja na sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kabla hatujailaumu Serikali, hatujasema Serikali haifanyi chochote, hatujasema kwamba tupeni nchi sisi tutatengeneza ajira, nafikiri kitu cha kwanza, hebu onesha wewe mahali ulipo kwamba umesaidia vipi kama mdau katika suala hili la kutengeneza ajira, kusaidia angalau vijana katika Jimbo lako wewe mwenyewe, kuwasaidia au kuwahamasisha wajiunge katika vikundi, *at least* kutengeneza hii ajira ambayo iko katika sekta isiyo rasmi ambayo sasa hivi kwa kweli kazi ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunarasimisha.

Mheshimiwa Spika, juzi tulikuwa katika mkutano wa *ILO* yaani Shirika la Kazi Duniani, sasa hivi mazungumzo ni kurasimisha sekta isiyo rasmi na Serikalini tumefanya hiyo na MKURABITA imefanya hivyo. Pia nimezungumza na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, katika kutekeleza miradi yao kuandikisha wanachama, basi wahakikishe sasa wana-*identify* vikundi, wanarasimisha sekta hii isiyo rasmi ili kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa kwa kweli msiwadanganye na msiichonganishe Serikali na vijana wao na wananchi kwamba, Serikali haifanyi kitu chochote, maana tunasema *charity starts at home and your home is your* Jimbo. Tuoneshe katika Jimbo

lako umefanya nini ili kuhakikisha kwamba angalau vijana wachache ulionao kabla hujapewa nchi kubwa hii, umeweza kuwasaidia kutafuta ajira. Kwa hiyo, msibeze kazi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la vijana kuchagua kazi. Vijana kwa kweli ndiyo nguvukazi ya Taifa na kama nilivyosema katika utafiti huu ambao unafanywa sasa hivi unaishia Februari tutaweza kujua nguvukazi tuliyonayo ni kiasi gani na tunajua vijana wanaoingia katika soko la ajira ni wengi zaidi ya 800,000 sasa hivi kulingana na hali halisi ya wanaohitimu vyuo vya elimu ya juu, lakini tatizo vijana wanachagua kazi.

Mheshimiwa Spika, mmezungumzia sana suala la Uhamiaji yaani vijana waliokwenda katika usaili. Nimeambiwa kwamba kati ya vigezo ambavyo vilikuwa vinatakiwa ni umri usizidi miaka 30. Vijana 4,000 katika usaili ule walienguliwa kutokana na umri mkubwa, sasa najiuliza hivi kweli wote hawa walikuwa hawana ajira? Kwa hiyo, vijana wakishaona kwamba hapa mahali naweza nikapata labda mshahara mnono au kuna maslahi, wanaacha ajira aliyokuwa nayo anatafuta ajira nyingine.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu nimeambiwa pia katika Wizara hiyo hiyo kwamba walipotangaza ajira ya zimamoto, vijana hawakujitokeza ilibidi waendelee kutafuta, lakini waliposikia Uhamiaji basi wakajaa pale. Hii ni kuchagua ajira, vijana wengi wanataka kufanya kazi za uhasibu, vijana wengi wanataka kufanya kazi ambazo *at least* wanaona kwamba wata *break even* haraka.

Mheshimiwa Spika, nafikiri ni wakati umefika sasa kwamba vijana msitafute kuchagua ajira kwa sababu tunasema ajira ni kazi yoyote inayoweza kukupatia kipato na ndiyo maana kwa kweli naomba sana Waheshimiwa tusaidiane badala ya kulaumu, basi tusaidiane kuwasaidia vijana kutafuta ajira.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la *internship*, nimeongea na Chama cha Waajiri *ATE* kwamba sasa hivi vijana wetu wanapotoka vyuo vikuu kwa mfano, wanahangaika …

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Kengele ya pili?

SPIKA: Ndiyo.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja!!

SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, atafutiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii nami pia kuweza kuchangia bajeti hii, hasa katika kutoa ufafanuzi wa maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameshauri, lakini pia wamesisitiza kuwa ni muhimu kutilia mkazo ili bajeti hii iweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwenye sekta ya elimu yale yote ambayo mmechangia tutayapa nafasi likiwemo na lile jambo ambalo mmelizungumza sana la posho ya mazingira magumu ya Walimu wetu. Nami nakiri kwamba yako maeneo ambayo yana ugumu wa kuyafikia, lakini pia hata kuishi kwa sababu tu hakuna nyumba za kuishi pale kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili Serikali tumelipa kipaumbele kwa kutambua matatizo yaliyopo na awali mwaka 2012, katika bajeti zetu tuliwahi kuzungumzia kutenga fedha ya kuwapa Walimu wanaokwenda kwenye maeneo haya, lakini jambo hili tulikaa zaidi na kutafakari kwa pamoja kati yetu TAMISEMI na Wizara ya Elimu na kuona kwamba jambo hili tukilifanya hivyo lingeweza kuwa si endelevu kwa sababu kama unampa Mwalimu mpya sh. 500,000/= kwenda kufanya kazi kwenye maeneo magumu, atatumia kwa wiki mbili tu, halafu anabaki anaendelea katika maisha magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha msingi ambacho tumekubaliana ni kuamua kuboresha mazingira kwa kujenga nyumba nzuri ili Mwalimu anapokwenda kazini akute nyumba, aweze kufanya kazi yake. Kwa kweli mpango huu unaendelea kutekelezwa, tumetenga fedha shilingi milioni 500 katika Halmashauri tulizozibainisha kwamba, ziko katika mazingira magumu, tumezipeleka fedha zile ili waweze kujenga nyumba nzuri na hii ni kwa Kurugenzi zote mbili ya Msingi na Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi hiyo imeshaanza, tumeshasambaza fedha hizo kwenye Halmashauri 40 na sasa nawaahidi Waheshimiwa Wabunge nitawaletea orodha ya zile Halmashauri zilizonufaika kwa awamu ya kwanza. Tutaendelea na awamu ya pili ili halmashauri hizi ziweze kupata nyumba za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatujaishia hapo tu, tunao ule mpango wa nyumba 1200, lakini huu umeenda kwenye Sekondari zaidi, tunaboresha miundombinu ya shule za sekondari nchini na tumeanza na Halmashauri mbili mbili. Tayari kazi inaendelea kwa shule 264, tutakuja shule 528 na baadaye shule 408. Shule hizi kati ya mambo yanayofanywa pale ndani ni pamoja na ujenzi wa nyumba za Walimu kwa lengo lile lile la kuboresha na kuondoa mazingira magumu ambayo Mwalimu anayakabili pale.

Mheshimiwa Spika, bado Serikali imeamua kuunda chombo kinachoitwa Bodi ya Mishahara na Motisha. Chombo hiki kazi yake mara zote ni kufanya mapitio ya mishahara ya Watumishi, lakini pia kama kuna posho mbalimbali na namna yoyote ile ambayo inamfanya mtumishi kunufaika akiwa kwenye utumishi wake. Lengo ni kuboresha mazingira ya utumishi wa mtumishi akiwemo na Mwalimu. Kwa hiyo, mipango yote huu ya Serikali ambayo inaendelea kutekelezwa ni kwa lengo la kuondoa ugumu wa maeneo ambayo watumishi wetu wanakwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo lilizungumziwa sana ni suala la madeni. Namshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais ameeleza vizuri jitihada za Serikali za ulipaji wa madeni mbalimbali. Juzi wakati najibu swali la msingi nilieleza kwamba, suala la madeni lipo na litakuwepo kwa sababu watumishi wanaendelea na utumishi wao, lakini kazi kubwa tunayoifanya sasa ni kuhakikisha tunaondoa mrundikano wa madeni ya watumishi wetu wakiwemo Walimu.

Mheshimiwa Spika, tulichokifanya sasa ni kuhakikisha kwamba, tunautumia muundo ambao utakuwa unatambua madeni na kuyalipa mara moja. Tumeanza kwa mtandao ambao ameueleza Mheshimiwa Waziri huu wa *Low Zone* ambao unabaini deni na kulipa mara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Walimu madeni tuliyonayo sana sana yako katika maeneo makubwa mawili; eneo la kwanza ni lile ambalo ni la likizo, uhamisho, masomo na matibabu. Eneo hili tunaendelea kulipa vizuri kwa sababu tunapeleka *OC* kwa Wakurugenzi zikiwa na maelekezo kwamba, fedha hizi ni kwa ajili ya likizo, matibabu na uhamisho wa ndani.

Kwa hiyo, jambo hili linaendelea vizuri na nashukuru vikao vyote ambavyo nimefanya na Walimu maeneo haya kwa kweli pamoja na kwamba, matatizo bado yanaendelea kwa

sababu labda upungufu wa fedha tunazowapelekea, lakini wanajitahidi sana kulipa na tunajaribu kupunguza na tutaendelea kuhakikisha kwamba, hatuna mrundikano wa madeni kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni yale malimbikizo ya mishahara ambayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, ameyaeleza sana ambayo yanalipwa moja kwa moja na Wizara hii. Hili nataka niseme kwamba, pamoja na mipango yote tuliyonayo sisi Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa Walimu, lakini bado Wizara ambayo leo hii tunaiombea bajeti yake nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge tuipitishe hii bajeti ili sisi tuendelee kulipa haya madeni, kwa sababu baada ya uhakika wa madeni ambayo Walimu wamehakikiwa yakaonesha takwimu ya shilingi bilioni 61 kiuhalisia madeni haya siyo shilingi bilioni 61.

Mheshimiwa Spika, tumeanza kuhakiki na kila tunapohakiki tunalipa na uhakiki ambao umeanza mwezi wa Nane mwaka jana mpaka tarehe 30 Aprili, tumeshalipa jumla ya shilingi bilioni 23.4 za madeni ambayo yanaendelea kuhakikiwa. Tunaamini tutakamilisha uhakiki huo, madeni yote yatakwisha na kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kwa kupitia mwaka huu wa fedha tutakuwa tumekamilisha kulipa madeni haya. Baada ya hapo, tumeamua sasa kuweka utaratibu mzuri ambao hautapelekea kuwa na mrundikano wa madeni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kuwasihi Walimu popote walipo na niseme tu Waheshimiwa Wabunge jambo hili tumelizingatia na tunalifanyia kazi ili tuweze kupata tija.

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo pia lilizungumzwa sana ni lile ambalo Mheshimiwa Lissu alisema Serikali imewadanya Watanzania. Nataka kusema kwamba, wakati mwingine tuwe tunayazungumza haya tukiwa wahalisia. Sisi tumeeleza hapa kwamba, tulitenga shilingi bilioni 12.4 kwa ajili ya utengenezaji wa Madawati nchini na tumeshatangaza zabuni na kazi hiyo imeshaanza. Usambazaji umeanza tarehe Mosi mwezi wa Sita na tunakamilisha tarehe 30 mwezi wa Nane, bajeti yetu sisi tumekuja kuisoma hapa ndani ya mwezi wa Sita, hivi tungesemaje hapa kwa Watanzania, siyo kwamba tumeanza kusambaza?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Madawati yanaendelea kusambazwana mpaka leo hii mikoa Sita imeshapata kwa Halmashauri zote 41 na tunaendelea na usambazaji. Tunahakikisha awamu ya kwanza Halmashauri zote nchini zitapata madawati yake kufikia Agosti, 30. Kwa hiyo, kazi inaendelea na tunapotoa ripoti lazima tuwaambie kwamba tunaendelea kusambaza madawati. Sasa tunachodanganya ni kipi, ni kwa sababu hatujafika Ikungi? Tutahakikisha kwamba, tutafika Ikungi na maeneo mengine na kila Halmashauri itanufaika kwa kupata madawati 756 awamu ya kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili tumeshatangaza zabuni kwa sababu tulipotangaza zabuni awamu ya kwanza tulinufaika kwa kupata bei ndogo, fedha iliyobaki yote tumetangaza, tarehe 27 keshokutwa tunafungua zabuni zile ili tupate Wazabuni watakaotengeneza Madawati. Tuna uhakika kila Halmashauri itapata jumla ya madawati awamu ya kwanza na ya pili siyo chini ya Madawati 902. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna uhakika kila Halmashauri nchini itapata madawati na Waheshimiwa Wabunge mtapata madawati kwenye maeneo yenu, tusaidieni kubaini shule zenye upungufu wa madawati ili tuwapelekee madawati yaweze kutumika. Kwa hiyo, hiyo ndiyo kauli yangu ya msingi na hakuna mahali popote ambapo Serikali tumedanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la ajira mpya ambalo lipo, tuliajiari Walimu 36,339. Tunashukuru zaidi ya 33,080 wameripoti katika vituo vya mpaka tarehe 30 Mei, lakini bado tuliwapa muda mpaka tarehe 20 juzi kuhakikisha kwamba wanaripoti. Takwimu tulizopata bado imebaki vilevile 33,080 ndiyo wameripoti. Wajibu wetu kwa kuwa tulikuwa na kibali chetu ni kuziba mapengo ili kukamilisha kibali tulichokipata. Mapengo ambayo yapo sasa ni Walimu 3,251 na ni lazima tuyajaze.

Mheshimiwa Spika, Walimu ambao walikuwa hawajapata ajira na wako sokoni, tulifanya sensa tukabaini jumla yao walikuwa 2,701 na Walimu 1,728 tumeshatoa majina yao na wote tumeshatoa kwenye mtandao, tumewasambaza kuziba mapengo kwenye Halmashauri zote ambazo Walimu wa awali hawakuripoti. Kwa hiyo, tunawataka kati ya tarehe 27 na 30 wawe wamesharipoti kwenye Halmashauri ambazo wamepangiwa. Kwenye eneo hili hakutakuwa na mabadiliko kwa sababu wanakwenda kuziba mapengo yaliyo wazi, kwa hiyo tusipate usumbufu tena wa kutaka kubadilishiwa.

Waheshimiwa Wabunge na Walimu wote ambao wamemaliza kozi za Ualimu kwa ngazi ya *Diploma, Degree* na *Grade A*, majina yameshatoka kwenye mtandao wa Ofisi ya Waziri Mkuu, waangalie majina yao na waende wakaripoti mara moja ili pia waweze kufanya kazi yao.

Mheshimiwa Spika, bado tuna mapengo ya Walimu zaidi ya 1,528 pia. Katika hili nataka nieleze kwamba, wale Walimu ambao walisoma kozi ambazo nilikuwa ninazieleza hapa mwanzo za *Bachelor of Education with Psychology, with Administration*, zote zile tumezi-*accommodate* na kwa hiyo tumewapangia kazi waende wakaripoti kwenye vituo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka niwasihi jambo hili tunaanza sasa kuwashauri vijana wetu wa kidato cha sita kwamba, ni bora sasa wachague kozi za kusoma kwenye Vyuo Vikuu zinazowaingiza kwenye soko. Sisi Ofisi ya Waziri Mkuu tunahitaji sana Walimu ambao wamesomea pia na masomo mawili kwa ngazi ya *degree* ya kufundishia Sekondari. Kwa hiyo, huo ndiyo wito wangu kwa vijana ambao wanakwenda kusoma *degrees*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ni hili la matokeo ya kidato cha tano kama ambavyo yametoka na tulitangaza. Tumeshaeleza vijana wetu kwa kweli tumepata mafanikio makubwa, nataka kusema kwamba, sasa hata shule zetu za Kata zimeweza kutoa *input* ya kutosha kwenye matokeo haya kwa vijana waliokwenda kidato cha tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shule zetu kwa tathmini ambayo tumeifanya kati ya vijana 74,214 ambao wamepata *pass* za kwenda kidato cha tano na sasa tumepata nafasi za vijana 50,000 tu kwenda kwenye *A Level* kwa sababu ya upungufu wa shule, kati ya shule za Kata 3,347 shule 989 zimepata nafasi ya kutoa vijana kwenda kidato cha tano. Kwa hiyo, shule zetu zinafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii sana kuwashukuru na kuwapongeza Walimu wetu nchini kwa kazi nzuri wanayoifanya, kwa jitihada walizozionesha na mchango wao kwa Taifa.

SPIKA: Muda umekwisha.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZAMIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono, naomba pia Wabunge tuunge mkono kwenye bajeti yetu ili tuweze kwenda kufanya shughuli zetu. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa badala ya Mheshimiwa Mary Nagu ambaye ataendelea baadaye, nitamwita Mheshimiwa Zambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Seif Rashid na atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Muhongo. Dakika 10 siyo nyingi!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ili niweze kujibu hoja hizi zilizojitokeza na najibu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, mwanzo kabisa naomba niseme kwamba, naunga mkono hoja ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Waziri anayehusika na mambo ya mipango.

Mheshimiwa Spika, mambo yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wanachangia Bajeti Kuu ya Serikali, masuala yaliyogusa sekta ya kilimo ni mengi sana, lakini nitaomba nijibu yale nitakayoweza ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kwa kiasi chake. Naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia na kwa kuweza kwa kweli kuisimamia Serikali katika eneo hili vizuri, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nianze na swali la kwanza linalohusu masuala ya pamba. Suala la pamba limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge, wengine kwa hisia kali na wengine wakitaka ionekane kama kweli Serikali haiwajali wananchi au wakulima wanaohusika na kilimo cha pamba.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme hili si kweli hata kidogo na badala yake Serikali imekuwa inathamini makundi yote yanayojihusisha na shughuli za kilimo katika nchi hii kwa uzito wake, lakini kuna kiwango tu ambacho Serikali inaweza ikafanya na ikifika mahali haiwezi basi tunategemea hata wananchi wenyewe pia waweze kuiunga mkono Serikali kwa maana ya kushiriki kadri wanavyoweza.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, suala la pamba mwaka huu na kwa sababu hoja ni nyingi niseme tu kwa kifupi; kwanza tumetangaza bei ya sh. 750. Nilitoa ufafanuzi hapa Bungeni wiki iliyopita kwamba, bei ambayo wanunuzi wanapaswa kununulia pamba ni sh. 750, lakini katika hilo na kwa maelekezo ya Serikali, tuliwaambia Wakuu wa Mikoa na Wilaya zote zinazohusika, wawaruhusu wafanyabiashara wanaonunua pamba wanunue kwa sh. 750 lakini sehemu ya *CESS* italipwa na Serikali kwa ujumla kwa maana ya Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, hili suala sisi Serikalini tumeshalizungumza na tumeshakubaliana. Kwa hiyo, Wakuu wa Mikoa wasiendelee tena kuhoji kwamba *CESS* inalipwa namna gani? Tumeshakubaliana na ni matumaini yangu na pia nizitoe wasiwasi Halmashauri zinazohusika kwamba, baada ya bajeti hii kupita na ikiwezekana robo ya mwanzo ya bajeti hii Serikali Kuu itaanza kulipa sehemu ya *CESS* hizi kwa Halmashauri zinazohusika bila kuchelewa sana.

Mheshimiwa Spika, ni mpango wa Serikali, kwa hiyo, tutaendelea kuzihudumia hizi Halmashauri zinazolima pamba tukijua kwamba, wengine wanasema wamekopa kwenye benki kwa ajili ya kuhudumia Halmashauri zao. Tunajua hilo, kwa hiyo, tutahakikisha kwamba Serikali na sisi tutashauriana, tuhakikishe kwamba, hazicheleweshwi sana. Hilo la pamba naomba niseme hivyo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sisi Wizara ya Kilimo tumekuwa tunajiuliza kila inapofika msimu wa pamba kunakuwa na matatizo sana hasa tunapoanza na bei. Sasa Wizara ya Kilimo tumejipanga, tutazunguka mikoa yote inayolima pamba nchini na katika kipindi cha mwezi wa

Nane mpaka wa Tisa tutakuwa tumepita ili tuzungumze na wakulima wote wanafikiri ni namna gani tunaweza tukatatua matatizo yanayoikabili sekta ya pamba ili tusiwe kila msimu unapoanza basi tunaingia kwenye matatizo ya suala la bei.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutapita katika mikoa hiyo tutazungumza pamoja na kilimo cha mkataba ambacho kimezua pia hofu sana miongoni mwa wakulima na Waheshimiwa Wabunge. Tutapita katika mikoa hiyo tutazungumza mambo haya kwa ujumla na undani sana.

Mheshimiwa Spika, lakini tunataka pia tuanzishe Mfuko wa Kinga ya Bei (*Price Stabilization Fund*). Hili Wizara ya Kilimo tunalizungumza na ni matumaini yetu kwamba, muda siyo mrefu sana tutalipeleka katika vikao vikubwa huko Serikalini ili tuweze kulipatia ufumbuzi na pale bei ya mazao inapoyumba basi tuwe na Mfuko ambao unaweza ukatoa fidia kuliko utaratibu ambao unatumika sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo ningelizungumza, ni ununuzi wa mahindi. Suala hili pia limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na wengi wameonesha wasiwasi. Naomba niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge. Moja, najua tunadaiwa kodi ya *CESS* ambayo Halmashauri zinadai karibu shilingi bilioni 5.7 na hili tumejipanga pia baada ya bajeti hii kupitishwa tutakaa pamoja tuangalie namna ya kulipa hili deni la mahindi kwa maana ya *CESS* katika Halmashauri zote zilizouza mahindi *NFRA*, deni linalofikia shilingi bilioni 5.7.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wasafirishaji mpaka sasa hawajalipwa karibu shilingi bilioni 5.6 na gharama zote hizi tunategemea tuzilipe muda siyo mrefu sana. Pia Wakala *(NFRA)* na wenyewe tumejipanga, tumepewa kibali na Mheshimiwa Rais cha kuuza baadhi ya mahindi ambayo yako kwenye maghala yetu na tunafikiri baada ya kuuza baadhi ya fedha zitakazopatikana zitatumika katika kulipa madeni haya ambayo Wakala wetu *NFRA* unadaiwa na Serikali. Kwa hiyo, tumejipanga na tunadhani mambo yakienda vizuri katika robo ya mwanzo ya mwaka wa fedha tunaweza tukawa tumeshalipa madeni yote.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu pia naomba niseme kwamba, Wakala wetu utaendelea kununua mahindi, tutanunua pia mpunga na mtama kidogo kule Shinyanga. Wakati fulani niliwahi kujibu hapa Bungeni kwamba, hatutanunua mtama, lakini baada ya kujipanga na kuona kwamba wakulima katika Mkoa wa Shinya na maeneo ya Kishapu wamelima sana, basi tumetenga kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya kuweza kununua mtama kidogo kutoka kwa wakulima wa maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limeulizwa jambo kwamba mwaka jana wakulima wengi wanaohusiana na utaratibu wa pembejeo tulikuwa tumewashawishi waingie kwenye vikundi halafu vikundi hivyo vingekopeshwa fedha kwa ajili ya kununua pembejeo. Bahati mbaya sana mipango haikwenda kama ilivyokuwa imepangwa, kwa hiyo, vikundi hivyo havikuweza kukopesha fedha. Hata hivyo, ilijengwa dhana kwamba, baada ya vikundi hivyo kuweka fedha hizo fedha zilichukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie wananchi wengi wa Tanzania kwamba, zile fedha ambazo walichanga wenyewe kwenye vikundi ni za kwao wala siyo za Serikali. Sasa baada ya mpango huo kutofanikiwa sana mwaka jana, mwaka huu tumejipanga vizuri tuhakikishe kwamba, vikundi hivyo vinaweza vikakopeshwa.

Mheshimiwa Spika, kupitia idara yetu inayohusika na masuala ya mbolea pale Wizarani mpaka sasa tumeshaandikisha vikundi 829 katika mikoa 14 na uandikishaji au kuvitambua vikundi hivi vya *SACCOS* au *AMCOS* vinaendelea kutambuliwa katika mikoa yote iliyobaki. Mwaka huu kwa sababu tumetenga fedha katika bajeti ya Serikali takribani shilingi bilioni 89,

basi tutakapokuwa tumekamilisha utaratibu huo tutaingia mikataba na benki na zitakopesha kwa utaratibu maalum kupitia kwenye vikundi. Kwa hiyo, naomba niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali inatambua jitihada hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini limezungumzwa suala la stakabadhi ya mazao ghalani na wengine wakasema utaratibu huu siyo mzuri. Naomba niwasihi wananchi wa Tanzania na wakulima, utaratibu wa stakabadhi ya mazao ghalani ni mzuri, pale ambapo haukutumika vizuri unaweza ukaonekana kwamba ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, lakini kimsingi sasa hivi tunakwenda na utaratibu pia wa *commodity exchange*. Huu utaratibu utatusaidia sana kwa sababu wakulima wanatakiwa wakusanye mazao yao kwenye maghala yao na utaratibu huu maana yake ni kwamba, watapewa stakabadhi na kitakachouzwa sasa pale ni risiti zao ambazo watakuwa wameziweka pale. Kwa sababu utaratibu utakuwa umeshawekwa, aina na ubora wa mazao vitakuwa vimeshatambuliwa. Kwa hiyo, tukishakuwa pale kutakuwa na nguvu kubwa ya soko kwa maana ya wananchi kuliko utaratibu ambao unatumika sasa hivi wa kila mtu kwenda kununua mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, sasa tunajua ziko kasoro katika utaratibu wa stakabadhi ya mazao ghalani sasa hivi, tunajitahidi kuzipitia ili tuweze kuhakikisha kwamba, tunazirekebisha.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda niseme kwamba, limeshajitokeza suala la mizani kwenye pamba na sikulisema wakati ule. Suala la mizani kwenye unununzi wa zao la pamba ni linazungumzwa kwa hisia kali sana kwamba, kuna wizi. Nataka niwaombe na kuwasihi wale wanununzi wote wa pamba ambao siyo waaminifu wanatumia mizani ambazo wamezirekebisha au wame-*temper* nazo waache kuwaibia wakulima. Siyo kwenye zao hili tu, mahali popote ambapo mizani zinatumika, naomba waache ku-*temper* na mizani hizo.

Mheshimiwa Spika, tutajitahidi kufuatilia kwa karibu na wale ambao watabainika kwa kweli Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na wenzetu wa Viwanda na Biashara ambao ndiyo wenye masuala haya, tutaomba tusaidiane nao ili tuhakikishe kwamba, tunaweza tukawalinda wakulima wetu ili wasipate kuibiwa na wale wenzetu ambao hawatutakii mema.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la mnyauko wa migomba kule Kagera. Nimefanya ziara kule na nitaomba tutoe hapa kauli ya Serikali kuhusu hali ambayo tumeiona kule. Kwa hiyo, hili naomba nisizungumze sana, tukipata nafasi tutatoa Kauli ya Serikali hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu bei ya mazao mengine kwa ujumla niseme kwamba muarobaini wake itakuwa ni kuwa na utaratibu wa kuwa na *commodity exchange* ambao nafikiri tukifika hapo tutakuwa kabisa tunaweza tukawahudumia wananchi wetu na wakapata bei nzuri za mazao bila matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya suala la muda na kwa sababu hoja ni nyingi, basi naomba nijibu hizo na mengine yale Waheshimiwa Wabunge tutawaandikia.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashidi atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo na Mheshimiwa Makalla ajiandae.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, nami nachukua fursa hii kushukuru kupata nafasi ya kuchangia, lakini kabla sijaendelea na mchango niunge mkono hoja na katika kuchangia nikijaribu kugusa kwenye maeneo yote ambayo kwa ujumla yameguswa na Waheshimiwa Wabunge. Sitaweza kuyapitia yote, lakini angalau nitayazungumza yale makubwa ambayo kwa ujumla yanahusu karibu kila sehemu yanazungumziwa. Sehemu moja kubwa katika Wizara yangu ni kuhusu eneo la dawa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tukizungumza katika eneo la dawa tuna changamoto nyingi na ni lazima tuseme tunafanya nini katika kuhakikisha kwamba eneo hili linapatiwa dawa kwa kuhakikisha dawa zinapatikana katika vituo vyetu, lakini tunapunguza kiwango ambacho dawa zitakuwa zinakosekana katika vituo. Vilevile tutafute namna ambavyo bajeti yetu inaweza ikatumika vizuri katika kutosheleza katika eneo hili la upatikanaji wa dawa katika vituo.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo moja ni katika kuboresha eneo la Bohari ya Dawa *(MSD)*, katika kuboresha eneo hili mambo mengi ambayo tayari tulishayafanya. Tulishapata washauri wakapitia kitaalam, wakaweza kutushauri maeneo ambayo tulitakiwa tuboreshe, tumebadilisha mfumo wa usimamizi wa kufanya ukaribu, karibu kila kitu chake sasa hivi kinafanyika kwa kutumia mifumo wa kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, vilevile inatuwezesha kufahamu kiwango cha dawa ambazo zinapelekwa hadi katika kituo husika. Tatizo tulilonalo kwamba baada ya dawa kufika katika kituo sasa dawa pale inatumika vipi, je inatumika kwa mgonjwa ambaye kweli amefika kwenye kituo na ameonwa na daktari na kuandikiwa hiyo dawa au imetumika kwa njia nyingine.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye eneo hili tunaboresha kwa kutengeneza mfumo mwingine wa kielektroniki ambao utakuwa unatupa taarifa za idadi na kiwango ambacho Daktari atakuwa anafanya kazi, wagonjwa wanavyofika kwenye kituo, ugonjwa ambao mgonjwa amethibitishwa kuwa anaugua na dawa ambazo ameandikiwa na dawa ambazo kusema kweli zimetoka kwenye kile kituo husika na kwa namna hiyo tutaweza kuboresha eneo hili la usimamizi wa dawa.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumeweka na baadhi ya dawa zimeshaanza kuwekwa alama yaani nembo, kila kidonge kinachoingia katika mfumo huu kimewekewa nembo ya *GOT* ili kuweza kudhibiti na dawa za namna hiyo zitatakiwa zionekane tu katika vituo vya Serikali na kwamba zikionekana katika duka la mtu binafsi basi huyo mtu atakuwa ni mwizi na itabidi awajibike kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine ni kwamba tunadhibiti na kuweza kuona namna bora tunavyoweza kutumia zile rasilimali chache tulizokuwa nazo katika vituo vyote nchi nzima. Katika eneo hili ni lazima tuweze kusimamia matumizi yetu, kusimamia namna ambavyo dawa zitakuwa zinatolewa kwa maana ya Daktari kuandika dawa kwa mujibu wa kanuni za kutoa dawa kwa mgonjwa, badala ya kuandika dawa ambazo nyingine hazihitaji, basi lazima kuwe na namna ambavyo Daktari atafuata ile miongozo ya tiba kutegemea na miongozo na ugonjwa ambao mgonjwa anaugua.

Mheshimiwa Spika, kingine tunaangalia eneo hili la mapato. Kusema kweli tunapozungumzia mapato tunazungumzia mapato kwa ujumla wake. Sasa kutokana na ukweli kwamba tuna mfumo wa Bima ambao unamwezesha mwananchi kuwa mwanachama katika Bima na hivyo hivyo anavyofika kwenye kituo chetu, Bima yake inatakiwa ilipe kwenye kituo.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru mpaka sasa eneo hili la Bima pamoja na kwamba bado hatujafanya vizuri na tunatakiwa tufanye vizuri zaidi, nikisema tu kwa wastani Bima kwa kipindi cha mwaka jana, tuseme mwaka 2012/2013, iliweza kulipa yaani kama mchango wote wa kuwalipa kwa ajili ya huduma ambazo wateja wa Bima wamepata nchi nzima, waliweza kutoa jumla ya shilingi bilioni 82 mwaka 2012/2013 na mwaka 2013/2014 wameweza kutoa jumla ya shilingi bilioni 77.

Mheshimiwa Spika, hizi fedha ni mapato kwenye vituo vyote vya tiba nchi nzima na kama zikisimamiwa vizuri na zikaweza kuainishwa kwamba sehemu kubwa ya hizi fedha zinaingia moja kwa moja *MSD* ili ziweze kutumika kwa kuhakikisha kwamba dawa zinapatikana kwenye vituo na hizo fedha zote zinatumika kwa kupeleka dawa kwenye vituo pamoja na kuwapelekea vitendea kazi, naamini sehemu kubwa ya changamoto tulizokuwa nazo kwenye vituo zitapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba tunaboresha eneo hili. Kwanza wananchi wengi zaidi wajiunge na Mifuko hii ya Bima ili wananchi wengi wanapokuwa wanachama wakifika kwenye vituo hivi watapata huduma na vituo hivi vitakuwa vinaidai Bima kwa huduma ambazo wametoa kwa wananchi ambao ni wanachama wa Mifuko hii.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili tumo katika hatua za mwisho za kuweza kufanya mabadiliko na kuweza kuamua njia ipi nzuri tuweze kuifanya ili angalau wananchi wengi zaidi waweze kujiunga na Mifuko hii ya Bima. Nafikiri Kamati ya Huduma ya Jamii, baada ya kipindi hiki tutapata fursa ya kukaa nao ili angalau waweze kupitia na kuishauri vizuri Serikali katika kukamilisha eneo hili la kuwafanya wananchi wengi zaidi wawe ni wanachama wa Bima na kutuwezesha kuongeza mapato katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine katika kusimamia, ni lazima tuweze kuboresha mifumo ya kieletroniki katika kuhakikisha kwamba mapato kwenye vituo hivi hayavuji. Mapato yanapoingia kwenye vituo lazima yasimamiwe vizuri, inajulikana kwamba katika kila kituo kiasi gani kimepatikana na kile kiasi kilichopatikana kule kinapokwenda.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka nizungumzie eneo la watumishi. Ni kweli tuna changamoto ya watumishi na kwa hakika tulivyokuwa miaka sita iliyopita tulikuwa katika hali mbaya zaidi. Tulikuwa na uhaba wa karibu asilimia 67 ya mahitaji ya watumishi katika vituo vyote nchi nzima. Katika kipindi hiki hiki ambacho tumekuwa na uhaba, bado tuliongeza vituo vipya kwa ajili ya kutoa huduma na vingine vilipanuliwa kuwa vyenye ubora zaidi au kuwa na uwezo mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, Vituo vya Mikoa vilipandishwa hadhi na vituo vingine ambavyo vilikuwa katika ngazi za Wilaya na vyenyewe vilipandishwa hadhi na huduma nyingine ambazo zilikuwa hazitolewi katika vituo zikawa zinatolewa na kwa namna hiyo idadi ya mahitaji ya wahudumu na watoa huduma kwenye vituo vyote nchi nzima iliongezeka karibu mara mbili zaidi kuliko ilivyokuwa miaka mitano au sita iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya juhudi za Serikali kwanza katika kuwafanya wataalam hao waanze kuingia vyuoni na kuweza kuzalisha wataalam wengi zaidi, hivi sasa upungufu huo umepungua na upungufu huo umo katika kiwango cha asilimia tuseme 50. Kwa hiyo, tuna upungufu karibu asilimia 50 baada ya kutoka kwenye upungufu wa karibu asilimia 67. Katika hilo juhudi kubwa zimefanywa na Serikali na hapo ni kwamba tumeongeza vituo zaidi ya 1,200 vipya ambavyo pia vimejazwa na watumishi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tuna jumla ya watumishi karibu 11,000 ambao wamo katika kukamilisha eneo hili la kuajiri na pale tutakapokuwa tumekamilisha kabla ya mwisho wa mwezi

huu, naamini katika vituo vingi na Halmashauri nyingi zitaweza kupata watumishi. Tuna changamoto bado ya uzalishaji na tunaendelea kuboresha eneo hili.

Mheshimiwa Spika, tutabadilisha namna ambavyo tunaviendesha Vyuo vyetu vya Wizara ya Afya ili angalau tuweze kushirikisha sekta binafsi na kuhakikisha kwamba vyuo vingi vinakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi wengi zaidi na kwa hiyo kuzalisha wataalam wengi zaidi na kuweza kuhakikisha tunaondoka na pungufu hili la wataalam na ikiwezekana kuzalisha wataalam ambao wanaweza wakaenda wakafanya kazi hata nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nikamilishe kwa kusema kwamba naunga mkono hoja na Wizara yangu tutajitahidi kwa kiwango ambacho itawezekana kushirikiana na Halmashauri zote...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante. Muda umekwisha.
WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Profesa Muhongo atafuatiwa na Mheshimiwa Makalla na Mheshimiwa Mwakyembe!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa kujibu hoja za Wabunge wote, lakini muda ni mfupi, lakini jibu moja ambalo ni la msingi sana ni la lile suala la Mheshimiwa Lissu. Alisema kwamba, nimedanganya dhahabu inayopelekwa nje sio dhahabu yetu. Katika hizi dakika 10 nisingependa kuzitumia kumfundisha Mheshimiwa Lissu, maana ya pato la Taifa ni nini. Kwa hiyo, popote alipo aende kwenye kompyuta a-*google* atafute maana ya neno pato la Taifa, yaani ile *Growth Domestic Product (GDP)* au *(GNI)*. Sasa akiitafuta hiyo *definition* atajua maana ya pato la Taifa ni nini na nadhani hili Bunge lisipoteze muda kwa kitu ambacho ni cha *Form One* na *Form Two*. *(Makofi/Kicheko)*

WABUNGE FULANI: Aaaaa!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, wengi sana wameongelea hapa mambo ya mafuta na mambo ya ajira. Sasa napenda niseme kwamba, ajira ambayo Mheshimiwa Kabaka ameiongea na Taifa hili lazima tujitayarishe, tunaingia kwenye uchumi wa gesi *(gas economy)*. Hii ndiyo itahakikisha kwamba tunapata ajira mpya na ajira nyingi na ajira za uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kwamba, tunaendelea kutafuta gesi na mafuta. Hadi leo hii tumeshagundua kiasi cha futi za ujazo trilioni 50.5, ukitaka kuweka kwenye mapipa ya mafuta ni karibu mapipa bilioni 9.6. Kwa hiyo, hii gesi ndiyo inakuja kufanya mapinduzi makubwa sana ya uchumi nchini hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine wameongelea kwamba hatupati chochote, lakini niwaeleze Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote wanaonisikia ni kwamba, kuwekeza anayetafuta sisi hatuwekezi senti hata moja, lakini huyu mtu anayewekeza ni lazima arudishe fedha zake. Hii Watanzania lazima tukubali, mtu hawezi kuja akawekeza asipate faida kwa uwekezaji wake. Ndiyo maana nimekuwa nasema uwekezaji wa baharini kwa siku mtu anatumia Dola za Marekani milioni moja, kwa siku mtu anatumia shilingi trilioni 1.6.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo huyu mtu au hii Kampuni lazima irudishe fedha zake. Wakisharudisha au wakati wanarudisha ndiyo mapato yetu ya Serikali sio kwamba hatupati chochote, tunapata kati ya asilimia 62.95 mpaka 82.3. Sasa kuna watalam, watu wanakwenda kozi ya wiki moja, ya wiki mbili wanageuka kuwa wataalam wa mafuta, wanasema hatujui, nadhani hapa itabidi hizi kozi nazo tuanze kuzipiga marufuku, zinakuja kupotosha watu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mambo yaliongelewa kwa kirefu sana ni umeme vijijini. Waheshimiwa Wabunge wote nadhani wengi tumeshawasiliana, nimewasihi na nyie msaidie Wizara ya Nishati na Madini kufuatilia wakandarasi, wakandarasi kila Wilaya Tanzania hii hata Wilaya za hawa Wapinzani wanapewa umeme. Serikali ya CCM haina ubaguzi, inaleta maendeleo kwa wananchi wote. Hatujui wenzetu wakichukua madaraka kitu ambacho hakiwezekani labda kwenye sayari nyingine, kwenye sayari hii haiwezekani, hamuwezi kutengeneza bajeti. *Definition* ya *GDP* hamjui, kwa hiyo, hamuwezi, labda mtaongoza Serikali kwenye sayari nyingine, sio sayari hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, umeme vijijini ni kwamba, wakandarasi wako kazini na napenda kutoa agizo kupitia hili Bunge kwamba, Mkandarasi ambaye atakuwa hajaanza kazi ikifika tarehe 1 Julai, *REA* lazima wamtoe huyo Mkandarasi waweke Mkandarasi mwingine. Narudia tena, ikifika tarehe 1 Julai Mkandarasi wa umeme vijijini hajaanza kazi ananyang'anywa hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini kingine ambacho ni muhimu sana ni kwamba, kuna vile vijiji vilivyoko pembezoni mwa mji, nawakumbusha Mameneja wa *TANESCO* narudia tena na tena wale ni wanavijiji msiwahesabu kama ni watu wa mjini, vijiji ambavyo viko pembezoni wale watu wana mazizi ya ng'ombe, wale watu wana makaburi ya wajomba zao, hawawezi kuwa ni mji ule. Kwa hiyo, vijiji ambavyo viko pembezoni mwa miji ya Tanzania nzima wale ni wanavijiji na wao wapewe umeme kwa gharama za wanavijiji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote mnaonisikiliza, *REA* awamu ya pili kuwekewa umeme ni sh. 27,000/= peke yake. Halafu na fomu ya kujazia ni sh. 5,000 ya *TANESCO,* hakuna rushwa, hakuna hongo, hakuna magendo. Kampuni itakayoletwa Wizarani kwamba wafanyakazi wake wameomba rushwa kwa wananchi vijijini, hiyo Kampuni inanyang'wanywa kazi, tumekubaliana hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mambo ya umeme nadhani wananchi wote wamesikia na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge ni kwamba *TANESCO* tunaisuka upya, lakini kusuka kwetu *TANESCO* mpya tunakaribisha ushindani, tunakaribisha na wawekezaji binafsi. Kwa hiyo mtu anayesema kwamba na tukitaka Taifa hili kwenda mbele, ni lazima tukubali wawekezaji binafsi. Ili mradi wawe wawekezaji, sio wababaishaji, sio wezi na wale ambao rekodi zao ni za kidalali dalali hawa hawatakiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo. Nimesema ajira zetu mpya zinakuja kwenye uchumi wa gesi na ajira mpya nazo zinakuja kupitia uchimbaji mdogo. Serikali imeamua kuwasaidia na kuwawezesha wachimbaji wadogo na Wabunge wengi sana hapa wameongelea. Napenda kumshukuru sana Mbunge wa Geita Mheshimiwa Vicky Kamata yeye amefuatilia kweli kweli watu wa Geita na uchimbaji wa Geita. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Vicky Kamata na Wabunge wengine, nendeni huko mkawaeleze wachimbaji wadogo kwamba, muda wa neema ni sasa. Wao tunawapatia ruzuku ya Dola

50,000 karibu sh. 80,000,000, tunampatia bure harudishi, lakini tunataka aboreshe uchimbaji wake. Kwa hiyo, wachimbaji wadogo tunaomba…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa muda umekwisha.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Naunga mkono hoja, mwingine hayupo labda niendelee. *(Kicheko)*

SPIKA: Hapana. Mheshimiwa Makalla, umesahau na wewe. Mheshimiwa Makala atafuatiwa na Mheshimiwa Mwakyembe. Tuna tatizo la muda na Mawaziri wote lazima waseme sasa hivi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa niaba ya Waziri wa Maji, amenipa maelekezo na nitakayoyasema ni kwa niaba yake na naamini kwamba nitafikisha ujumbe ambao amenituma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nianze tu kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kwamba mimi sio miongoni mwa wale wanafiki, nasema hivyo kwa sababu; moja, lengo lolote la Chama cha Siasa ni kushika dola, hakuna chama kilichoanzishwa duniani kuwahubiria watu kwenda mbinguni, ni kushika dola na ukishika dola unapewa nafasi ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi. Sisi ndiyo tumepewa nafasi hiyo ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi na lazima itekelezwe kwa maana ya bajeti kupitishwa na kuwapelekea huduma mbalimbali wananchi wa Tanzania, kwa hiyo ninayo sababu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, mimi kama mwana-CCM ahadi za mwanachama zinasema, nitasema kweli daima, fitina kwangu ni mwiko. Kwa hiyo, naamini kwamba kilichowasilishwa ni sahihi na nakiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wale ambao ni wanafiki maana yake ni kutokupitisha bajeti, halafu mwaka kesho tukija unasema mwaka jana tulipitisha hiki hamkutekeleza, ulipitisha na nani wakati ulikataa kupitisha bajeti? Kwa hiyo, unaanza kuwa mtaalam wa kufuatilia Randama, unasema mwaka jana tulitenga kiasi fulani kwa nini hamkutekeleza, wakati hukuwepo na ulikataa kupitisha bajeti. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, ni pale ambapo utataka huduma ya maji, barabara na zahanati, lakini wakati huo huo bajeti umeikataa. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba wananchi wenyewe wataamini na message *imefika.*

Mheshimiwa Spika, nilishukuru Bunge kwamba, walitupigania sana Wizara ya Maji kuiomba Serikali kutenga shilingi bilioni themanini waipatie Wizara ya Maji. Nitumie fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwamba Wizara yetu imepokea shilingi bilioni themanini mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo tayari zimeshaanza kupelekwa katika miradi mbalimbali ambayo ilikuwa imesimama, Wakandarasi walikuwa wanaendelea na kazi, walikuwa bado wanadai malipo. Kwa hiyo, malipo hayo sasa yanafanyika na miradi mbalimbali ambayo ilikuwa ikiendelea, itaendelea kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, kubwa ni kwamba Waziri wa Maji amenieleza kwamba amefanya mazungumzo majuzi na wenzetu wa *World Bank,* nao wameonesha nia ya kukamilisha ahadi zao kabla ya mwaka wa fedha huu haujakwisha. Kwa hiyo, hiyo nayo ni habari njema katika Wizara ya Maji kuona kwamba, mambo yale ambayo tulikuwa tumepanga tunaweza kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, nimesimama pia hapa kutoa ufafanuzi, wapo Waheshimiwa ambao walifika hapa wakasema kwamba takwimu tunazozitoa kuhusu maji ni takwimu ambazo zimepikwa, zinawahadaa Watanzania na hazina uhalisia wowote. Nataka niseme kwamba jambo hilo siyo kweli na kwamba nataka kusema takwimu zinazotolewa na hotuba mbalimbali zinazotolewa hapa ni za uhakika kabisa.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango kwa hotuba yake nzuri ambayo alieleza kuwa mipango ya Serikali imekuwa ikihudumia wananchi toka uhuru kwa kila mwaka kati ya wananchi laki tatu mpaka laki tano, ni sahihi kabisa na siyo kwamba wananchi laki tano mpaka sasa wamehudumiwa maji vijijini. Nataka kusema kwamba, takwimu tunazozitoa hapa zimetokana na kuingia katika miradi ya matokeo ya haraka sasa ambayo tulikuwa tumelenga kuwafikia Watanzania milioni nane na katika vijiji elfu moja mia tano na hamsini na tano.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo ya *BRN* na baada ya kupunguza ule mlolongo wa utekelezaji wa Vijiji Kumi mambo ya *no objection,* sasa ni kwamba, miradi iliyokamilika ni miradi mia mbili arobaini na nane na katika vijiji mia mbili arobaini na saba na tumewafikia watu milioni mbili, laki tatu tisini na nane na mia tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaona katika kipindi cha kutekeleza miradi hii ya *BRN,* kutoka Watanzania milioni kumi na tano vijijini, mpaka sasa tumewafikia milioni kumi na saba, lakini ipo miradi inayoendelea ambayo hela mlizozipitisha sasa na hizi Serikali ilizozitoa miradi inayoendelea katika vijiji mia tano themanini na tatu itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba wakati huo huo ipo miradi katika vijiji mia saba ishirini na tano imeshasainiwa tayari na pesa hizi tulizozipitisha zitakwenda kutekeleza miradi hiyo. Kwa hiyo, tunaposema haya mambo ni kwamba, tumeyafanyia kazi na kwamba ni ya uhalisia kabisa.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo ambalo limeongelewa hapa kuhusu tatizo kubwa la maji kwa Jiji la Dar es Salaam. Niseme tu kwamba, tulishaeleza wakati wa bajeti yetu kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la maji kwa Mji wa Dar es Salaam na ndiyo maana upo mradi wa Ruvu Chini ambao utakamilika Agosti na wa Ruvu Juu mwezi Septemba na visima vyote vya Mpiji na Mpera Novemba mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema tu kwamba, kazi zinaendelea na niwaalike Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam wote kwa pamoja tushuhudie tarehe 14 tunafanya ziara, tunakwenda Ruvu Juu, kukagua kazi zinazoendelea pale, katika kutanua kile chanzo, lakini pia na kazi ya kulaza bomba, kuna Wakandarasi wawili wako pale. Kwa hiyo, niwaalike akina Mheshimiwa Mnyika, akina Mheshimiwa Halima Mdee tuungane kwa tarehe hizo, tuwepo pale bila visingizio vyovyote na ratiba nimeshaitoa.

Mheshimiwa Spika, pia tutakwenda Tegeta pia kwa Mheshimiwa Halima kule tuangalie hali ya ulazaji bomba inaendeleaje katika Ruvu Chini. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba, tatizo la maji kwa Mkoa wa Dar es Salaam tunalimaliza. Kwa hiyo, sitatoa taarifa nyingine; tarehe 14 tuko Ruvu Juu na tarehe 16 tuko Tegeta na maeneo yote hayo tutakwenda mpaka Makongo na maeneo yote tutaongea na wananchi, kuwapa matumaini juu ya Serikali ya CCM inavyofanya kazi katika kuhakikisha kwamba tatizo la maji tunalimaliza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana muwepo tarehe hiyo, tuungane kwa pamoja na wananchi watajua ni nani anayefanya kazi hii kama siyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo pia kwa maeneo ambayo yalikuwa hayapati maji. Kuna mabomba ya Mchina tunaangalia namna ambavyo tunaweza kufanya baada ya kupatikana haya maji, matenki hayo tutayaimarisha, tutayajenga upya lakini pia tunataka kujenga pale Salasala kwako, kuhakikisha kuwa maji sasa maeneo ya Goba, Mbezi Juu yasiwe na tatizo na Makongo Juu watu waweze kupata maji. Kwa hiyo, nataka kuweka sawa jambo hilo ili watu waelewe tu kwamba kuna kazi zinafanyika na yote haya ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2010/2015.

Mheshimiwa Spika, pia kuna jambo ambalo liliongelewa kwa hisia kali na Mheshimiwa Badwel kuhusu Bwawa la Farkwa ambalo lengo letu ni kuhakikisha kuwa Mji wa Dodoma unakuwa na maji ya kutosha. Nataka kusema kwamba, Serikali iko katika hatua mbalimbali, mtu wa tathimini ya mazingira amefanya kazi hiyo, amewashirikisha viongozi mbalimbali wa Bahi, lakini pia vijiji ambavyo Bwawa hili liko katika Wilaya Chemba, vijiji vya karibu vitapata maji.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni kwamba, tutaendelea kutoa elimu kwa watu wa Bahi na huko Chemba, kuona kwamba ile nia nzuri ya Serikali inatimia. Pia niwahakikishie kuwa tumepanga mwezi wa Saba tutakutana tena na wadau mbalimbali na asasi zingine ambazo wamekuwa wakipiga kelele juu ya suala la mazingira na kuathiri wananchi. Hilo niwahakikishie kuwa tutalifanya mwezi Julai.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja tena. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Harrison Mwakyembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka na baadaye Mheshimiwa Mary Nagu.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia. Nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia sekta ya uchukuzi kwa njia ya reli na kwa njia ya anga. Kwa kweli siyo rahisi kama walivyosema Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, kwa dakika kumi nilizopewa kumwongelea kila Mbunge na hoja zake. Kwa hiyo, tutakachofanya ni kutoa tu kwa maandishi majibu yetu na maelezo yetu ili kila Mbunge awe na kumbukumbu ya yaliyojiri katika Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea sekta ya uchukuzi kwa njia ya reli na kwa njia ya anga kwa hisia kali sana, ni kama ilivyokuwa kwenye mkutano wa bajeti ya mwaka jana na kujenga hisia kana kwamba Serikali pengine haijali, haijafanya lolote toka mwaka jana, kitu ambacho siyo sahihi hata kidogo na naamini hata Waheshimiwa Wabunge wanajua hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kidogo kwa sekunde chache nieleze kuwa mijadala inavyokwenda ndani ya Bunge letu mara nyingine inachukua mkondo wa kisa cha chui na

mtoto wa swala, waliokutana mtoni. Chui anamwambia mtoto wa swala mbona unachafua maji ninayokunywa. Mtoto wa swala anasema lakini mzee wewe umekaa sehemu ambayo mto unatokea, mimi niko huku chini. Akasema lakini wewe mtoto una tabia mbaya hata jana ulinipita bila kuniamkia, adabu huna, akasema Mzee sikuwa mimi akasema ni wewe. Akamwambia Mzee mimi nimezaliwa leo asubuhi, akamwambia hata wazazi wako wote ni wa hovyo sana! Kwa hiyo, ni kwamba hakuna zuri upande wa Serikali, lakini faraja yetu sisi upande wa Serikali ni kwamba, Watanzania ni makini, wanatambua juhudi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitegemea sana kwenye mkutano huu, Waziri wa Fedha na Manaibu wake wapongezwe kwelikweli kwa kufanikisha bajeti ya Uchukuzi kwa miradi yote ya *BRN* ambayo kwa kweli ambayo imekwenda kwa asilimia zaidi ya 95%. Wamefanya hivyo siyo kwa ajili ya kunipendelea, ni kwa sababu ya kujua tu kwamba sekta ya uchukuzi ndiyo ufunguo wa kuweza kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudie tu kwamba Hazina hawa ambao tunawatilia shaka, tuliwaomba fedha ya kununulia vichwa vipya vya treni kumi na tatu, shilingi bilioni sabini nukta tisa wametupa zote, vichwa vinaingia Disemba hapa, tuliwaomba pesa za mabehewa mia mbili sabini na nne ya mizigo wametupa shilingi bilioni arobaini na tano nukta tano nne, pesa imekwenda, mabehewa yametengenezwa na Septemba yanaanza kuja nchini, tutamalizia milioni tisa ambazo Waziri amesema atanipa muda wowote ule yakimalizika.

Mheshimiwa Spika, tuliomba pesa za mabehewa ya abiria ishirini na mbili ametupa shilingi bilioni ishirini na nane nukta moja tano mabehewa yanaingia Septemba. Tuliomba mabehewa ta breki thelathini na nne Mheshimiwa Saada kwa kweli hakuchelewa, akatupa shilingi bilioni sita nukta tisa na mabehewa yanaingia mwezi Agosti, miezi miwili tu ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tuliomba mabehewa ishirini na tano kwa ajili ya kubebea kokoto kwa ajili ya ukarabati, tumepewa shilingi bilioni nne na mabehewa yanaingia katika miezi miwili ijayo. Tumeomba shilingi bilioni saba nukta sita tununulie mashine ya kushindilia kokoto, tumepata hiyo fedha na vile vile tumepata mpaka mashine ya kunyayulia mabehewa ambayo inangia Disemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiishi tu hapo, tumekaa na wenzetu wa Benki ya Dunia tukawaambia tunataka kufanya mapinduzi kwenye uchukuzi, wenzetu nao wameamua kununua vichwa vitatu vipya vya treni pamoja na mabehewa arobaini na nne kwa ajili ya kuanzisha *block trails* kutoka Dar es Salaam kwenda Isaka kwa shilingi bilioni thelathini na moja nukta nane tano.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Bandari ikasema hapana haiwezekani tukawaachia *World Bank* peke yake tunataka mapinduzi ya Uchukuzi hapa na wao wametoa bilioni kumi na saba nukta tano kufanya *manufacturing* ya vichwa vya treni vitano.

Mheshimiwa Spika hii ina maana? Ina maana kwamba, uchukuzi reli ya kati unafufuka, pengine Waheshimiwa Wabunge walishasahau kuwa *TRL* ilibinafsishwa kwa nia njema tu, kama mashirika yetu mengine kama *NBC, TBL*, SIGARA na kadhalika ambayo yanafanya vizuri sana mpaka leo, lakini tofauti na mashirika hayo ufanisi *TRL* ulikwenda chini sana, tena sana, mpaka Serikali ikaamua miaka miwili na nusu kuichukua tena *TRL* tuweze sisi wenyewe kuipandisha na tulichukua ikiwa hoi bin taabani, ilikuwa na vichwa vinane tu vinavyofanya kazi ambavyo vipo mpaka leo badala ya vichwa hamsini na nne vilivyokuwepo mwaka 2002 ikiwa chini ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali tumeichukua *TRL* ikiwa na mabehewa mia sita tu ya mizigo badala ya mabehewa elfu mbili mia mbili tuliyokuwa nayo mwaka 2002, ndiyo maana kipindi cha 2002 tumeweza kusafirisha tani milioni moja nukta tano ya mizigo. Leo hii kutokana na mchakato uliopita huo ambao tumeamua kuurejesha, tunasafirisha kati ya tani laki moja na hamsini na tano mpaka laki mbili ambayo inaua barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunakoelekea ni kuzuri na uwezeshwaji ambao tumeupata kwenye bajeti, unaturejesha kwenye nguvu tuliyokuwa nayo zamani. Hayo ni mabadiliko mazuri tuyatambue, tusiwe kama chui, tuyatambue ni mazuri hata kama ni ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, wapo wanaoongelea *standard gauge railway* kwamba sasa na sisi tujenge *standard gauge railway* ni sawa tunakubali, tuna miradi mikubwa miwili; kuna miradi ambayo ni ya kwetu sisi wenyewe, lakini kuna mradi mwingine ambao tumeungana na wenzetu wa Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Spika, *final study* imekamilika na *Cana Rail* mwezi wa Nne mwaka huu, tusingeweza kufanya kingine cha ajabu nje ya hiyo *study* na sasa hivi kwa usajili wa Benki ya Afrika *(ADB),* tunatafuta *transaction Adviser* kutusaidia huu mradi tuweze kujenga kwa njia ya *PPP*. Sasa hiyo ni mipango ya nchi tatu, lakini sisi wenyewe hatujakaa kusubiri nchi tatu zifanye hiyo kazi, sisi wenyewe tumeanza kutafuta *partiners* katika kujenga. Tuna mtandao mrefu sana wa *rail* hapa, elfu mbili mia saba na saba ndiyo mtandao wa reli na wote nia yetu ni kuweka katika *standard gauge*.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie kwamba tumefanya kazi nzuri sana kama Serikali kufikia huko na ndiyo maana tumepata mafanikio makubwa sana juzi Davos kwenye mkutano wa *World Economic Forum* tukiwa na Mheshimiwa Rais. *Transport corridors* hamsini na moja za Afrika zilishindanishwa, lakini imeweza kuwa *picked Central Transport Corridor* kutoka Dar es Salaam kwenda Magharibi, tumechaguliwa sisi *the only transport Corridor* ambayo sasa imekuwa *adopted in the World Economic Forum* na wafadhili na wawekezaji wengi wameanza kutufuata na nina uhakika tutafika mbali.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa *standard gauge* usitufanye sasa tusimamishe kukarabati reli ya kati, *we shall bring our economic to a stand still,* hatuwezi kufanya hivyo, *nobody is doing that*. Wakenya wenyewe na wao wanajenga *standard gauge* ingawaje kwa gharama maana wao ni *build and design*. Kwa hiyo, *at the mercy* ya huyo anayejenga wenzetu kilomita moja inajengwa kwa Dola milioni tano nukta nane, ndiyo hivyo, ukienda namna hiyo, lakini sisi tumefanya study zote. Kwa hiyo, ninachosema tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kuhusu *ATCL,* tumeeleza mengi kuhusu *ATCL,* mwaka jana ilikuwa ni malalamiko, ilikuwa ni kwamba Serikali inafanya nini watu walioifikisha *ATCL* hapo. Tukawaeleza jamani tunachukua hatua na leo Waheshimiwa Wabunge wote mnajua kuwa kuna kesi Mahakamani dhidi ya watu ambao wametufikisha hapa, nisingependa tuongee zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile tumechukua hatua kuisafisha *ATCL* and *ATCL is doing very well now* pamoja na ndege mbili ambapo mwaka jana ilikuwa inakwenda Tabora na

Kigoma na Mtwara, leo ina kwenda Mbeya, inakwenda Arusha, inakwenda Mwanza na ina kwenda Zanzibar, lakini *we dont appreciate,* tunawakatisha tamaa hawa vijana.

Leo wameanza kwenda Bujumbura, wana kwenda Moroni wanakwenda sasa Anjuan na kuanzia tarehe 29 ATCL wanaanza kwenda Johanesburg kwa kukodi *share* na Shirika la *Inter Air* la Afrika ya Kusini, sasa badala ya kuwakatisha tama, hebu tuwasaidie *ATCL* waweze kuboresha huduma zao.

Mheshimiwa Spika, nakuhakikishia, *once* tunasafisha *balance sheet* ya *ATCL* tutapaa na hakuna mtu atakayeweza kuturudisha chini tena kwa sababu *once bitten, twice shy* na kufanya kosa mara moja siyo mbaya, lakini kurudia kosa hayo ndiyo majuto.

Mheshimiwa Spika, najua kuwa kengele ya pili inanifuatia na mimi siwezi kukubali mtu wa uchukuzi kupigiwa kengele. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, atafutiwa na Dkt. Mary Nagu na Profesa Mwandosya! Dakika ni kumi, siyo nyingi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, naomba kabisa niunge mkono hoja kwa nguvu zangu zote na niwapongeze kabisa Mawaziri wetu wa Fedha, Mheshimiwa Waziri Saada Mkuya na Wasaidizi wake Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Malima. Niseme tu kwamba ukiangalia timu hii na ukaangalia kazi nzuri waliyoifanya ya ku-*balance* bajeti, haikuwa kazi ndogo ni kitu kigumu, lakini kinaonekana kwamba kiko kwenye mikono salama kabisa.

Mheshimiwa Spika, hapa tunashuhudia mpangilio wa *generations* wa vizazi, sasa sisi *BBC* tumeondoka, wameingia *Dotcom*, *BBC* ni *Born Before Computers* na *Dotcom* mliona Mheshimiwa Saada alipokuwa anawasilisha kwa kutumia *Ipad* hotuba ndefu na hakutetereka. Rafiki yangu mmoja akaniletea meseji akasema tunamwangalia pia Mheshimiwa Waziri wa nchi jirani, yeye alikuwa anahangaika na makaratasi kama mimi. Kwa hiyo, haya ni mambo mazuri, ni lazima tuyatambue.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba pia nijielekeze kwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa ufasaha kabisa. Bajeti hii nimeifuatilia, kwa upande wangu wengi wamezungumzia mambo ya ardhi, masuala ya nyumba yalijitokeza na hata bughudha za mjini na mipango miji, maendeleo ya makazi nayo niliyasikia.

Mheshimiwa Spika, siyo rahisi kujibu kila kitu kilichosemwa, lakini niseme kwamba, katika bajeti hii Wizara yangu imepangiwa fedha kiasi tu cha kufanya kazi yetu, lakini uzuri ni kwamba tunafanya kazi na wadau wetu, sekta nyingi ambazo ni wadau wetu hususani wenzetu wa kilimo ambao wana kazi kubwa sana ya kusukuma maendeleo katika *Big Results Now,* wamepewa fedha za kusaidia kusukuma kazi zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema kwamba matatizo ya ardhi yaliyokuwa yanajadiliwa hasa nilisikia, kwa mfano, Mheshimiwa Waziri Mstaafu wa Ardhi, Mheshimiwa Chiligati alizungumza kwa ufasaha kabisa tatizo la kuwa na ardhi kama mtaji mfu, yaani *dead capital* ambayo haitumiki kwa sababu ya kukosa upangaji na upimaji.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nichukue nafasi hii niseme kwamba, kwa wale wadau wakubwa hasa Sekta ya Kilimo, Sekta ya Misitu, Sekta ya Hifadhi zetu, Sekta ya Mifugo wanapopanga matumizi ya ardhi, basi watakuwa tayari na wataweza kutoa kipaumbele katika kutafuta bajeti za kupima ardhi zetu.

Mheshimiwa Spika, suala hili la kupima ardhi ni changamoto ya nchi hii, kwa sababu asilimia kumi tu ya ardhi ndiyo imepimwa na katika Vijiji 13,000 vya nchi hii, ni Vijiji 1000 tu ambavyo vina matumizi bora ya ardhi. Kama huna mpango wa matumizi bora ya ardhi, kimsingi huwezi kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji, Sheria zinakuwa haziruhusu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unakuta kwamba, katika gurudumu zima la kujaribu kusukuma wawekezaji na ninapozungumza wawekezaji hapa kwa sisi Sekta ya Ardhi wawekezaji wanaweza wakawa wa nje ama wa ndani. Mwekezaji ni mtu yeyote ambaye atakwenda kuboresha ile ardhi iweze sasa kutumika kwa tija zaidi. Kwa hiyo, nafikiria kwamba hili nalo linahitaji ufafanuzi, hivyo, wawekezaji wawezeshe wa ndani na wa nje kupata ardhi zao.

Mheshimiwa Spika, yameongelewa masuala kadhaa ya kuhusu hati miliki hasa za kimila. Nifafanue kwamba hati miliki za kimila ambazo ni chombo kitakachotusaidia katika kurasimisha ardhi yetu, katika kupima na kuweza kuitumia kwa manufaa ya wale wenye ardhi hiyo kwa namna ya kupata mikopo ya uzalishaji, lakini pia kwa manufaa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Bajeti yetu hapa, kupanua wigo wa mapato. Ardhi Tanzania sasa hivi haijachangia vya kutosha katika mapato ya Taifa kwa sababu haijapimwa na haijamilikishwa. Kama haijapimwa inamaanisha kwamba haichangiwi, kutozwa kodi na kuwa pango la ardhi halilipwi. Hakuna kitu ambacho kitaweza kutoa fedha nchi hii kama ardhi ingekuwa inatozwa kidogo tu lakini inachangia.

Kwa hiyo, unakuta kwamba wenye ardhi sasa hivi walio wengi hawachangii. Mpaka sasa hivi hati miliki za kimila, Serikali haijaziwekea tuzo lolote au kodi yoyote. Sasa niseme tu kwamba kwa kuboresha Bajeti yetu hii, nijielekeze kwa mara nyingine tena kwa ngazi ya Halmashauri na ngazi za Vijiji ambazo ardhi hizi zipo.

Ardhi Tanzania asilimia 70, ni mali ya Vijiji. Sasa katika Serikali zetu za Vijiji tunaweza pia tukapanua mapato yetu katika Halmashauri ili mradi tunawekeza kidogo katika upangaji na upimaji wa ardhi. Narudia tena kwamba, Bajeti hii mbele yetu imewezesha, lakini peke yake haitaweza kulikamalimisha hilo.

Mheshimiwa Spika, kitu cha pili ambacho nimekisikia sana, wachangiaji wengi wamezungumzia jambo la fidia. Kwa kweli eneo la fidia katika Bajeti yangu, nimesema kwamba limekuwa ni eneo la kuzua migogoro ya ardhi, hapa Bajeti yetu inatuwezesha kwamba mwenye mradi lazima atoe fidia. Sheria ya ardhi ipo wazi, ardhi yako haiwezi kutwaliwa kabla haijatolewa fidia stahiki.

Mheshimiwa Spika, sasa kitu cha kwanza wewe mwenye ardhi ujue haki yako. Lakini wewe mwenye mradi lazima pia ujue kwamba, kama huna fidia hutaweza kuifikia ile ardhi. Jambo hili nalo mmelisikia, halitakiwi kuwa kero, wala kutugawa. Fidia inayotolewa ni lazima kama imechelewa zaidi ya miezi sita, inalipiwa riba. Kwa hiyo, hapo ni wenye ardhi kuwa macho kuhakikisha kwamba, wanadai riba zao na ewe nimeshaagiza kwamba kama umefanya fidia miaka minne imepita, hiyo fidia imekuwa imefutwa *automatically* kwa kanuni mlizoweka kwa sababu inakuwa kwamba ni lazima upate vigezo vipya.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, nizungumzie sasa suala la upangaji miji. Miji yetu inaendelea kukua kama uyoga na kwa wale ambao mna kero za ukaaji holela, muarubaini ni kupima Miji yetu kuwa na mipango kabambe yaani *master plan.* Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kutoa rai kwa Halmashauri zote ambazo hazina *master plan* ya Miji yao kwamba tuanzie pale. Uzuri ni kwamba, zoezi hili na lenyewe linalipika siyo tu kwa kuitegemea Serikali kuu, lakini linalipika pia kwa sisi mapato yetu madogo ya ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nichukue nafasi hii, Halmashauri ya kwanza ninayoiweka mbele ni Halmashauri yangu ya Muleba Kusini, nachukua nafasi hii kuhamasisha kule Muleba Kusini mnaonisikiliza na sisi tuwe na mipango ili tuwe mfano wa kuigwa, wenzetu watuige.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii, kusema kwamba kuna *trading stations*. Kuna Vituo vingi vya maduka vinakuwa haraka haraka. Sasa kusudi tuviokoe hivi kabla hatujachelewa, hivi navyo venyewe vitangazwe kama maeneo ya upangaji kusudi tuondokane na ukuaji wa miji kiholela. Kinaanza Kituo kidogo kinakua, kinakua, baada ya hapo inakuwa vurugu.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo mchango ambao naweza kutoa na kwa mara nyingine tena nawapongeza Mawaziri wetu wamefanya kazi nzuri na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mary Nagu!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuchangia hoja ya Waziri wa Fedha kuhusu Bajeti ya Serikali kwa Mwaka huu 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Fedha kwa umahiri wake pamoja na Naibu Mawaziri wake. Naomba sasa nitoe mchango wangu kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri hususan katika eneo la uwekezaji na maendeleo ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa maoni na ushauri mzuri sana kwa Serikali kuhusu mikakati ya kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Serikali itazingatia ushauri huo kwa dhati kabisa na utautumia kwa kuweza kuimarisha uwekezaji kwa sababu uwekezaji unaleta manufaa makubwa sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Wabunge yanadhihirisha kwamba Serikali tunakubaliana kwamba Wabunge sasa wanaona umuhimu na uzuri wa wawekezaji katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Hii inatokana na ukweli kwamba, kukuza uwekezaji ndiyo njia ya uhakika ya kuongeza fursa ya ajira kwa vijana wetu, ndiyo upatikanaji wa bidhaa na huduma, teknolojia mpya na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, usipopanda shamba lako hutavuna. Uwekezaji ni sawa na kupanda shamba na hatimaye unavuna. Vile vile uwekezaji ndiyo njia ya uhakika ya kuongeza thamani ya mazao yetu. Kama uwekezaji kwenye viwanda utaongeza thamani ya mazao na bidhaa zetu? Ukiuza nje utauza kwa thamani kubwa kuliko ukiuza malighafi nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo ya kujenga uchumi imara, jukumu la msingi la Serikali ni kujenga mazingira wezeshi ya uwekezaji. Tusipofanya hivi wawekezaji wa ndani na wa nje hawatawekeza. Tumesikia hoja nyingi sana kuhusu misamaha ya kodi inayotolewa na Serikali ikiwa ni pamoja na unafuu wa kodi unaotolewa kwa wawekezaji kwenye hatua za awali za kuanzisha miradi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi waelewe kwamba Serikali zote duniani zinatoa kodi siyo tu kwa madhumuni ya uwekezaji au ya kuongeza mapato. Inatoa kwa madhumuni mengi mbalimbali kwa sababu muda hautoshi, nitatoa maelezo yangu kwenye *Hansard* na naomba niende sasa kutoa takwimu.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi hutolewa na Serikali kupitia mitaji ya sekta binafsi kama nilivyoeleza hapo awali. Kuna dhana imejengeka kuwa miongoni mwa Watanzania wengi kwamba wawekezaji hususan wawekezaji wakubwa, hawatozwi kodi yoyote au wamesamehewa kulipa kodi zote. Hii si kweli! Dhana hii si sahihi kabisa kwani wawekezaji wote hulipa kodi mbalimbali kwa bidhaa zote ambazo hazijaorodheshwa kuwa ni bidhaa za mtaji.

Mheshimiwa Spika, Wawekezaji hulipa kodi hizi hata katika kipindi cha uanzishwaji wa miradi. Kwa mujibu wa taarifa ya fedha za Mamlaka ya Mapato Tanzania zilizokaguliwa na kwa utafiti wa *TIC* katika Mwaka wa Fedha 2013, jumla ya misamaha ya kodi iliyotolewa na Serikali ilikuwa ni shilingi trilioni 1.4 na hata Waziri alisema. Kati ya misamaha hiyo, iliyoelekezwa kwenye miradi ya uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji ni shilingi bilioni 290.7, sawa na asilimia 19 ya misamaha yote iliyotolewa. Serikali imeweka utaratibu wa kufuatilia wale wote waliopewa misaada.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa kueleza kwamba pamoja na misamaha hiyo iliyotolewa, tathmini iliyofanywa na Serikali kuhusu misamaha iliyotolewa na Serikali kwenye bidhaa za mtaji kama makampuni hamsini makubwa kwa kipindi cha miaka mitano toka 2005 mpaka 2010 imeonesha kwamba, makampuni hayo yaliwekeza mtaji wenye thamani ya shilingi trilioni 1.7.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, misamaha iliyotolewa ina thamani ya shilingi bilioni 88.8, sawa na asilimia tano tu ya mitaji iliyowekezwa. Naomba Waheshimiwa Wabunge waone kwamba, katika kipindi hicho hicho kiasi cha kodi mbalimbali kilicholipwa na makampuni haya kwa Serikali ni shilingi trilioni 1.1. Misamaha ni trilioni 1.7, kodi iliyolipwa ni trilioni 1.1, sawa na asilimia 66 na kodi iliyosamahewa ni sawa na asilimia tano.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hivyo tu! Ajira zilizopatikana kutokana na Makampuni haya 50 ni sawasawa na 121,951. Sasa tathmini hiyo inaonesha pia kwamba tusingetoa misamaha hiyo, Makampuni hayo yasingewekeza. Kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu na wananchi waone kwamba tunatoa misamaha ili kuleta manufaa makubwa zaidi ya uchumi ndani ya nchi yetu na tusione kwamba wawekezaji wote ni wezi au ni matapeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lililo muhimu na ambalo nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, lazima tusimamie misamaha hiyo tuliyotoa, ili tupate manufaa yaliyolengwa na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kutokana na utafiti wa *INTAD,* mitaji kutoka nje ya Tanzania iliyopatikana mwaka 2005 ni dola za Marekani milioni 520. Mwaka 2012 mitaji iliyoletwa Tanzania ni sawa na dola za Marekani, bilioni 1.1. Kama tusingewezesha wawekezaji, tusingewavutia, wasingelikuja! Nawaambia kwamba kutokana na mitaji ya dunia, mitaji ambayo inakwenda Marekani ni asilimia 30, inayokuja Afrika ni asilimia tatu. Inayokuja Tanzania ni asilimia 0.03 na sisi ndiyo maskini kuliko Marekani. Kwa hiyo, lazima tuendelee kujenga mazingira mazuri ya sekta binafsi, kufanya kazi yake na wawekaji kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, mikakati ya kuvutia wawekezaji haijaanza leo. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alisisitiza suala hili

kwenye hotuba aliyoitoa kwenye Bunge la Afrika kusini tarehe 16 Oktoba, 1997 na nanukuu kwa lugha ya Kiingereza:

"Africa South of Sahara is an isolated region of the world." Na Tanzania ndiyo zaidi. *"I have been many times to Latin America, many times to Asia, many times to many parts of Africa before coming here. Many times to a large number of countries in Europe, Logic of Geography means that if you have problems of unemployment in Eastern Europe, East Europeans will want to move to West Europe. The economy of the US pulls people from Mexico in the United States. Now they are working together to create jobs in Mexico to prevent poor Mexicans from looking for jobs in the United States."*

Mheshimiwa Spika, ili Marekani izuie *Mexicans* inabidi sasa iende ikafanye kazi Mexico. *So the US is not fighten of unemployment in Africa South of Sahara.* Kwa hiyo, tujue Marekani na Europe hawavutiwi kuja Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Kwa hiyo, sisi lazima tujifanyie kazi wenyewe kuwavutia wawekezaji kwa sababu wawekezaji hawana sababu ya kuja, wana maeneo mengi sana ya kwenda kwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tafsiri hii kwa Kiswahili, naomba niseme tu kwa muda mfupi, tafsiri isiyo rasmi ya maneno haya ya Baba wa Taifa ni kwamba nchi za Afrika Kusini mwa jangwa la Sahara ni eneo lililojitenga na lisilo la kipaumbele kwa nchi zilizoendelea za Marekani, Ulaya na Asia kwa sababu za kijiografia.

Vipaumbele katika sera za nchi hizo tajiri ni kutafuta ufumbuzi wa changamoto za ukosefu wa ajira kwenye nchi maskini ambazo kijiografia zimepakana nazo kama vile Mexico kwa Marekani na Egypt pamoja na nchi zingine Afrika ya Kaskazini. Kwa hiyo, sisi lazima tufanye jitihada za ziada, namshukuru sana Profesa Muhongo, Mama Kabaka, Mama Anna Tibaijuka na wote waliongea Mawaziri waliosimama wameongea juu ya umuhimu wa uwekezaji.

Naomba na ninyi Waheshimiwa Wabunge mjue umuhimu wa uwekezaji…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Haya ahsante. *I am running out of time*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Profesa Mwandosya! Nitampa dakika 15, dakika tano atazichukua kwa Mheshimiwa Wassira.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili nitoe pongezi kwa Mawaziri Mheshimiwa Saada Mkuya Salum na vile vile Mheshimiwa Wassira na Manaibu Waziri pamoja na Watendaji katika maeneo yao. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa katika sehemu mbili. La kwanza ni lile eneo ambalo Waingereza wanasema hata malaika wanaogopa kulizungumzia au kutembea juu yake, nalo ni la ajira. La pili ni jinsi wengine wanavyotuona sisi Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze na ajira. Wengi wetu na nina hakika kwa nia njema kabisa, wamezungumzia kuhusu ajira kama vile bomu ambalo linangoja kulipuka, ni kweli, lakini labda sasa ni wakati ambapo mjadala uondoke kutoka kwenye bomu, twende kwenye jinsi gani tunaweza kulitengua hilo bomu na vilevile ni jinsi gani tunaweza kupunguza athari za hilo bomu kama litalipuka. Nadhani mjadala huu utakuwa na tija zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ajira ina pande mbili. Upande mmoja ni wanaoajiri, mwingine ni wanaoajiriwa. Sasa sehemu ya wigo wa ajira ongezeko lake umezungumzwa kwa ufasaha sana na Mheshimiwa Waziri wa Kazi na naamini kabisa Mheshimiwa Wassira atakapokuja kuelezea suala hili atazungumzia kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Spika, nataka kujielekeza katika mchango wangu kwenye waajiriwa, waajiriwa watarajiwa, huu ndiyo upande mwingine wa sarafu la ajira. Nasema hivyo kwa sababu ni Mwalimu na nimehusika sana katika kutaarisha hawa waajiriwa watarajiwa na hawa ndiyo nataka kuzungumza nao kupitia kwako.

Mheshimiwa Spika, nina mambo kumi ambayo ningependa wazingatie. Jambo la kwanza kwa ushauri wachague fani ambazo wakimaliza wanaajirika na fani muhimu sana kwa dunia ya sasa ni fani ya sayansi, teknolojia na uhandisi. Kwa hiyo, mnapokwenda Vyuo Vikuu hizi ni baadhi ya fani ambazo mzichague.

Mheshimiwa Spika, lakini namba mbili, wale ambao mtasomea sayansi na mnasomea Uhandisi, hakikisheni kwa ulimwengu wa sasa vile vile mnachukua fani ya usimamizi wa biashara mnakuwa na shahada ya Uhandisi na *MBA*. Hapo mtaajirika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, la tatu mnaochukua fani za sanaa, vilevile mjiendeleze katika fani ya usimamizi.

Nne, msidharau lugha ya Kiswahili na vilevile Kiingereza. Muwe na uelewa wa kutosha na mzungumze hizi lugha mbili kwa ufasaha; Kiswahili na kiingereza.

Tano, jifunzeni vilevile lugha angalau moja kati ya lugha zifuatazo:- Kifaransa, Kispaniola, Kireno na Kichina kwa sababu ya ushindani wa ajira Kimataifa. Itawasaidia sana.

Sita, msiwe waoga katika kushindana katika soko la ajira ya nchi za nje. Afrika Mashariki, Mashariki ya Kati na sehemu nyingine. Utakuta waliojaa katika soko hilo la ajira kutoka Afrika ni Wakenya, Waganda, Ghana na Wanigeria, na sisi ni lazima tuingie huko, tusiogope ushindani, hata kidogo!

Mheshimiwa Spika, narudia tena kuhusu Kiswahili. Walimu wa Kiswahili wanahitajika sana katika nchi kama Burundi, *DRC*, Gabon, China, Ghana na Nigeria, lakini ni lazima uzitafute hizo nafasi, haziji tu.

Juzi nilikuwa Burundi, Mheshimiwa Waziri wa Elimu ananiambia tunahitaji sana Walimu wa kufundisha Kiswahili; tunahitaji sana Walimu wa kufundisha katika shule zao za *VETA*. Sasa hizo ni ajira ambazo lazima mzitafute, haziji hivi hivi. Kwa hiyo, ushindani utakuwepo lakini maeneo mengi ya ajira pia yapo.

Mheshimiwa Spika, lingine naomba sana waajiriwa watarajiwa; kujiajiri ni jambo zuri sana, msingoje wakati wote Serikali itoe ajira. *(Makofi)*

Nilikuwa nazungumza na Wanafunzi wangu waliokuwa wanamaliza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nilipokuwa nafundisha, nikawaambia siyo lazima mwajiriwe. Tukaongea kwa muda mrefu, tukabishana. Miaka minne, mitano baadaye mwanafunzi mmoja akanijia akaniambia lile somo ulilonipa kuhusu kujiajiri, nakushukuru sana. Sikwenda kutafuta ajira. Nilijiajiri mwenyewe, nikaanzisha Kampuni yangu, sasa ninaajiri wafanyakazi 40. Nikasema kumbe somo liliingia.

Kwa hiyo, inawezekana, msiogope sana kujiajiri. Serikali imewapa elimu, na elimu ni nyenzo. Sasa hiyo nyenzo itumieni. Serikali inachongojea ni mrejesho wa hiyo kazi mtakayoifanya kwa maana ya kulisaidia Taifa. Kwa hiyo, naomba hili nalo mlizingatie.

Mheshimiwa Spika, tisa ni kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Kabaka, wasomi wenzangu kwa kweli msichague kazi wala ngazi ya kuanzia kazi. Mnaweza mkaanzia ngazi ya chini, lakini mkapanda haraka sana.

Kwa hiyo, Mhandisi unaweza ukaanzia na ngazi ya Fundi Mchundo, lakini ukapanda haraka sana. Lakini usipite tu Mitaani tu miaka miwili inapita, eti kwa sababu unangoja kazi ya Uhandisi ambayo haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kumi na la mwisho, naomba mjiamini, muwe wabunifu, jiungeni katika vikundi na mtumie uelewa wa pamoja ili muweze kutumia nafasi zilizopo za kibenki, za kifedha ili kujiendeleza. Kwa hiyo, mchango wangu nimeelekeza zaidi kwa waajiriwa watarajiwa zaidi kuliko Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya mchango wangu. Ukisikiliza labda mtu aliyetoka sayari nyingine, sayari ya *Mars* anakuja hapa ghafla, anasikiliza mjadala; akisikiliza mchango wa baadhi yetu na hasa kutoka Upinzani, anaweza kusema hii nchi karibu inasambaratika. Sasa mimi nitajibu kusema kwa jinsi wanavyotusema wengine toka humu humu duniani; wanasema nini kuhusu maendeleo ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika, kuna jarida la *Business Insider* ambalo linainukuu Benki ya Dunia na kusema, nchi ambazo uchumi wake unakua kwa kasi sana duniani ni pamoja na Tanzania. *(Makofi)*

Shirika moja la *Ventures Africa,* linasema Tanzania ni moja ya nchi kumi katika Bara la Afrika ambao uchumi wake umekua sana katika mwaka 2013. Haya siyo ya Mheshimiwa Wasira wala siyo ya Mheshimiwa Mkuya.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ujasusi la Marekani linatufuatilia sana, lakini nalo linatoa taarifa zake. Linasema Tanzania ni nchi ya 22 duniani kati ya nchi zaidi ya 200 katika kasi ya kukua kwa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa siyo kwangu haya, mimi nasema wanavyosema wengine. Maana yake ningesema ni sisi tumesema, aah basi najua kabisa kwamba ingekuwa balaa hapa!

Halafu jarida la *Wall Street Journal* la Marekani ambalo ni jarida maarufu sana, linasema, Waamerika hawajui sana mambo ya Afrika na sehemu nyingine za dunia; lakini sasa wafanyabiashara wa Marekani wanasema, Tanzania ni nchi ya 13 kati ya 20 zinazosema Marekani wanawashawishi Wamarekani waende wakawekeze. Hii ni *Wall Street Journal;* hii siyo mimi wala siyo Mheshimiwa Saada Mkuya, wala siyo Mheshimiwa Wasira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nimesema haya yote wengine wanavyotusema ili Watanzania tujue kwamba kwa kweli tumefanya kazi kubwa, bado hatujamaliza lakini tuna mwelekeo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka tu kwa kumalizia, Umoja wa Mataifa wanasema nini? Unasema Tanzania imepunguza vifo vya akina mama wakati wa uzazi kutoka 770 kati ya laki 100,000 mpaka 450 mwaka 2013. Vifo vya watoto vimepungua kutoka 160 kwa watoto 1,000, mpaka sasa tumefikia 54, tumeshavuka hata lengo la milenia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika tiba ya *TB*, tumeweza hata kuzidi lengo, kwamba sasa tunaweza kutibu asilimia 87 ambapo lengo la milenia ni asilimia 85. Uandikishwaji wa wanafunzi, tulishavuka lengo kabisa siku nyingi sana! Wanafunzi wanaomaliza Elimu ya Msingi lengo karibu tutalifikia la milenia. Watumiaji wa simu za mkononi, tumeshafika asilimia 57 ya Watanzania. Watumiaji wa *internet,* sasa ni milioni 13. Tupo mbali sana.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi, ninachosema ni kwamba tusiwe wanyonge, tuongeze kasi, tutafikia malengo ya dira ya 2025. Tutayafikia kwa hakika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa. Wale Mawaziri wachache waliotakiwa kusema wamemaliza, sasa nitamwita mtoa hoja wa shughuli ya mipango na kwa mujibu wa Kanuni ya 28 Kanuni ndogo ya tano, nitaongeza muda wa nusu saa.

Mheshimiwa Mtoa hoja Wassira.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana wewe pamoja na wasaidizi wako, Naibu Spika na Wenyeviti kwa kazi yenu mnayofanya nzuri sana ya kuliongoza Bunge letu. Zaidi, natoa shukrani kwa kunipa nafasi hii tena ili nihitimishe hoja yangu ya hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/2015.

Aidha, natoa shukrani pia na kutambua mchango wa Kamati ya Bunge chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi kwa ushauri na ushirikiano tulioendelea kuupata tangu tulipoanza mchakato wa Mpango wa mwaka huu Novemba mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, niruhusu niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kusema na kwa maandishi. Nawashukuru sana. Labda niseme kwamba Bunge hili limetimiza wajibu wake wa kuishauri Serikali na vile vile kuisimamia kwa mujibu wa Katiba.

Nawashukuru Mawaziri wote wa Sekta zinazohusika na Mpango huu wa Maendeleo kwa ufafanuzi ambao wameutoa na kwa maelezo yote ambayo yamesaidia sana kuhitimisha sekta hii au Mpango huu wa Maendeleo na hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaeleza mambo ambayo nataka kuyazungumzia, mambo ya jumla kwanza, nataka niseme neno moja tu. Mpango wa Maendeleo na utekelezaji wake unatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010 na 2015. Hili halina mjadala, kwa sababu Chama hiki ndiyo kilishinda na kikaamua kutengenza Mpango ukaidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukikaa hapa tena tukawa tunashauriana namna ya kukataa, maana yake tunashauriana namna ya kukataa kutekeleza Mpango ambao sisi wenyewe tumeuweka. Kwa hiyo, ushawishi wa kukataa, unakataliwa na wote nafikiri wenye nia njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema huu Mpango unafanana na Ilani yenyewe. Niliulizwa juzi katika mjadala kwamba Ilani ya CCM ilisema itaboresha na kujenga uchumi wa kisasa. Lakini Ilani ya CCM ilisema hivi, uchumi wetu bado uko nyuma, lazima tuchukue hatua za kupiga hatua kuelekea mbele katika kuufanya uwe wa kisasa.

Mimi sijui kama Wachumi watasemaje, lakini uchumi unaweza ukasaidiwa sana kama kuna miundombinu katika nchi. Mtu anayelima mahindi Rukwa na ambaye hana soko kwa sababu hana barabara, huwezi kuzungumza kwamba ana uchumi wa kisasa. Ni lazima umjengee barabara ili umpe fursa halafu fursa zile ndiyo zijenge uchumi wa kisasa. Hii ndiyo kazi tunayoifanya kupitia Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, hoja kubwa sana ya kwanza ambayo imezungumzwa sana hapa, ilikuwa ni kwanini uchumi unakua lakini umasikini haupungui kwa kasi ya kuridhisha? Hoja hii imeongelewa na Waheshimiwa Wabunge 19 na wamejadili wawili kwa maandishi.

Kwanza, ni kweli kwamba uchumi wa Tanzania umekuwa unakua kwa wastani wa asilimia sita mpaka saba katika kipindi cha mwongo uliopita. Hili la hali ya umasikini ni kweli imekuwa inapungua lakini kwa kasi ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitano iliyopita 2007 mpaka 2013 umasikini umepungua kwa asilimia 5.4 kutoka asilimia 33.6 mwaka 2007 mpaka asilimia 28.2 ambao bado ni kiwango kikubwa sana cha umasikini katika nchini yetu, maana hii ni karibu theluthi nzima ya Watanzania. Ni lazima tukiri kwa sababu ukikiri unajipa nguvu ya kwenda kupambana zaidi na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, pengine ni vizuri tufafanue vizuri jambo hili la ukuaji wa uchumi na uhusiano wake na umasikini ili tuweze kuelewana, kwa sababu tunazungumza hapa na Wabunge ambao nadhani wanaelewa, lakini Watanzania wote wanahitaji majibu maana tunazungumza na Waheshimiwa Wabunge lakini tunazungumza na Watanzania vilevile.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme, kwanza Pato la Taifa ni kitu gani? Kwa lugha rahisi kabisa, pato la Taifa ni thamani ya shughuli zote za uzalishaji mali na utoaji wa huduma. Kwa kipindi cha miezi 12 mnatoa huduma, mnazalisha katika sekta mbalimbali halafu mnatoa thamani ya kile mlichokizalisha kwa miezi 12 ndiyo kinaitwa Pato la Taifa.

Kwa maana hiyo Pato la Taifa kwa mwaka 2013 linaitwa *nominal,* lilikuwa Shilingi trilioni 53.1. Lakini pato hilo likilinganishwa na bei za mwaka 2001 ambalo huitwa pato halisi, ni Shilingi trilioni 20.5, ukilinganisha na pato la mwaka 2012 la trilioni 19,000.1 halisi unaona tofauti ya trilioni 1.3 ambayo ni sawa na ongezeko la 7%.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukisema uchumi umekua kwa asilimia saba, maana yake ni kwamba pato la mwaka jana lilikuwa dogo zaidi kuliko mwaka ambao unaufanyia mahesabu. Unafanya kwa mahesabu hayo unapata asilimia ngapi ya mafanikio yaliyopatikana.

Pato la Taifa hupanda na kushuka kutegemeana na hali ya uzalishaji na utoaji wa huduma. Kwa hiyo, mwaka mmoja inaweza kwenda juu na mwaka mwingine ukakuta liko chini. Ni jambo la kawaida.

Mheshimiwa Spika, lakini shughuli zinazochangia pato la Taifa, kubwa zaidi ni mawasiliano, asilimia 22.8, nimesema kwenye hotuba yangu; fedha asilimia 12.2; ujenzi asilimia 8.6; biashara ya jumla na rejareja asilimia 8.3; hoteli na migahawa asilimia 6.3; lakini kilimo kinakua kwa asilimia 4.3 kwa muda wa miaka miwili mfululizo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu jamii kubwa ya Watanzania wanategemea kilimo ambacho kimekua kwa asilimia 4.3, maana yake nini? Maana yake ni kwamba ukuaji mdogo katika Sekta ya Kilimo unachangia katika kuendeleza au kuwepo kwa umasikini. Kwa maneno mengine tija ndogo katika sekta mama ya kilimo ambayo inaajiri watu wengi, inapokuwa inakua kidogo zaidi na kuchangia kidogo katika uchumi, lakini inabeba watu wengi zaidi, ndiyo tatizo hapo unapolikuta. Utafiti wote uliofanyika, unaonesha kwamba umasikini umejikita zaidi katika Sekta ya Kilimo na hasa katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, tunafanya nini katika kupambana na hali hiyo? Kwanza, ni lazima kuongeza bajeti ya Serikali na nadhani tumekuwa tunaongeza na tutaendelea kuongeza bajeti ya Serikali inayoenda kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ina mambo maalum inafanya. Inashughulika na utafiti, ugani, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, uzalishaji mbegu na uratibu wa shughuli za masoko na mikopo. Ili kuharakisha ukuaji wa Sekta ya Kilimo na Uwekezai, Serikali imekamilisha sasa kazi ya uanzishaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(Tanzania Agricultural Development Bank)* ambayo itaanza kutoa mikopo kupitia *SACCOS* ili kuweza kuwafikia wakulima wadogo. Hiyo itakuwa mojawapo ya hatua ambazo kwa kweli zitasaidia katika siku za usoni katika kupambana na umasikini katika Sekta hii inayoajiri watu wengi.

Mheshimiwa Spika, kilimo kama biashara nyingine, ni lazima ikope, lazima ikue na mitaji ni lazima ipatikane. Uanzishwaji wa Benki hii ni hatua ya kusaidia Sekta ya Kilimo. Vilevile kuwatia moyo wawekezaji wa ndani kuwekeza katika viwanda vidogo vidogo au vya kati ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Hili ni jambo moja ambalo bado tupo nyuma kusema kweli.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutumia nafasi hii kuwataka Wawekezaji wa ndani ili waweze kuchukua na wao nafasi yao. Tusitegemee wa nje peke yake, na wawekezaji wa ndani wawekeze mitaji yao hapa katika viwanda vya kati, viwanda vikubwa ili tuweze kuongeza thamani ya mazao yetu; basi hiyo itatusaidia sana katika kuongeza uzalishaji katika Sekta ya Kilimo maana kilimo na viwanda vinakwenda pamoja.

Mheshimiwa Spika, vilevile hivi karibuni Serikali inakusudia kuanzisha soko la mazao ya kilimo linaitwa *Agricultural Commodity Exchange* ambalo litakuwa ni soko linalounganisha wazalishaji wa ndani na wanunuzi wa nje katika mtandao. Kazi hiyo itafanyika kwa kusimamiwa na Soko la Mitaji la Dar es Salaam. Uzoefu uliopo kwenye Soko la Mitaji la Dar es Salaam utatumika kukuza soko hili. Hiyo nayo itakuwa hatua nyingine ya kusaidia na hatua hizi zote zitakuwa zinasaidia kumpa kipato zaidi mkulima na kwa hiyo kupambana na umasikini.

Mheshimiwa Spika, umasikini ni tatizo, lakini siyo tatizo la Tanzania peke yake. Maana wapo watu wanafikiri umasikini upo Tanzania, kwa hiyo umasikini unakuwa ajenda.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013 nilikwenda China. China kwa muda wa miaka 20 ilikuwa inakua kwa wastani wa asilimia 10, lakini nilipokwenda China sikwenda kwenye Miji mikubwa peke yake, nilitaka kwenda kijijini na niliwaambia kabisa Wachina, mnionyeshe kule ambako Wachina masikini wanaishi. Walinipeleka kwenye kijiji cha masikini wa Kichina. Kuna masikini milioni 100 China, pamoja na kwamba duniani uchumi wa China ni wa pili, lakini bado una masikini milioni 100 ambao ni 8% ya *population* ya China.

Mheshimia Spika, nikaenda nikakuta umasikini kweli kweli, hata huku kwetu sijauona. Maana kuna Kijiji ambacho wanawake wote wamehama, wamebaki kijiji cha wanaume tu peke yao. Wameukimbia ndiyo! Ni *problem!* Kwa hiyo, nadhani la maana hapa ni kujadili *way*

forward, namna gani tunaweza ku-*deal* na hii *problem.* Kulalamika hakuwezi kuondoa umasikini, ni lazima tujibu jambo hili kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pato la Taifa linapogawanywa kwa idadi ya watu ndiyo tunapata kitu kinaitwa pato la wastani. Lakini ni hesabu, ni *arithmetic,* kwamba una *population* ya watu milioni 48, pato lako ni trilioni kadhaa. Ukigawanya zile trilioni kwa idadi ya watu, unapata *average*. Ni sawasawa na mtu kukwambia Tanzania ina watu milioni 50, ina ng'ombe milioni 25. Kwa hiyo, kwa wastani kila watu wawili wana ng'ombe mmoja. Lakini mwingine hata ng'ombe hajaona. *It is just an arithmetic*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *arithmetic* inayotumiwa na dunia nzima katika kupima ukuaji wa uchumi, huwezi kuukwepa. Ndiyo dunia ilivyo na hesabu zile na vitabu vyote vya Wachumi hata waliomo humu, ndiyo kazi waliyosoma. Naona hata *Attorney General* anatikisa kichwa pale, ina maana naye aliusoma hivyo hivyo! Eh, huo huo! *(Kicheko)*

Jambo la pili ambalo limezunguzwa sana linahusu ajira. Namshukuru sana Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Waziri wa Kazi na Mheshimiwa Mwandosya vile vile amesaidia sana katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba hili jambo limechangiwa kwa hisia kali sana. Wanaojadili suala hili wameeleza tatizo na ukubwa wake, lakini vile vile nilisikitika kidogo kwa sababu hawakutoa mawazo namna ya kupunguza hii *problem.* Sasa kusema ni kubwa, ni kubwa; nataka niseme kwamba hata Serikali kama wote walivyosema, nasi tunakubali kwamba hili jambo ni *problem,* na tunajali.

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba hatujui kwamba tuna ajira, tunajua. Lakini tunajaribu kujifunza kitu gani kinafanya hali inakuwa hivyo na tunafanya nini. Ndiyo hasa mambo ya maana zaidi, kwanza ujue ugonjwa ni nini? Maradhi hayo yanatokana na nini? Halafu upate dawa! Lakini kusema ugonjwa huu ni mkubwa; sasa ni mkubwa sawa, sasa tufanyeje? Tusaidie kupata jibu basi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulimwenguni hapa wanasema dunia nzima, tatizo la ajira; yaani *unemployment* iko kwa asilimia 12.7. Afrika ya Kusini chini ya Jangwa la Sahara ni asimilia 12. Hii ni *ADB* ndiyo iliyofanya hiyo *study*. Lakini Taarifa ya Ofisi ya Takwimu ya Taifa letu, inaonyesha mwaka 2012 kulikuwa na watu milioni 2.4 ambao walikuwa hawana ajira za uhakika na wengi wao ni vijana.

Kwa hiyo, huwezi ukawa na hali hii halafu ukasema hamna *problem*. Utakuwa wewe *laissez-faire* kweli kweli! Sasa tumejaribu kufanya tathmini, vijana ambao hawana elimu ambao hawana kazi na hata elimu hawana, ni asilimia 2.3. Wenye Elimu ya Msingi ambao hawana kazi ni asilimia 8.1 ya hao ambao hawana. Vijana walio na Elimu ya Sekondari ni asilimia 32. Unaweza ukaona, kadri elimu inavyokwenda juu, ndiyo u*nemployment* inakuwa kubwa zaidi.

Vijana walio na elimu ya ufundi ni asilimia 23. Vijana walio na elimu ya kati na ya juu, ni asilimia 23.4. Tatizo la ukosefu wa ajira katika nchi nyingi za Afrika ikiwemo Tanzania, linatokana na uwezo wa soko la ajira, amelieleza vizuri ndugu yangu Mheshimiwa Mwandosya na Mheshimiwa Waziri wa Ajira, kwamba unasomesha watu wangapi wanatoka kwa mwaka? Ajira zinazozalishwa na uchumi wako ni kiasi gani? Pengo lile linakua, lina-*create unemployment*. Kwa hiyo jambo la ajabu sana kwamba limetokea Tanzania peke yake, hapana! Liko kila mahali. *(Makofi)*

Sasa uzoefu wetu unaonyesha kwamba tungeweza kuwaajiri vijana hawa katika sekta mbalimbali, lakini viko vikwazo. Kwa mfano, tija ndogo ya kilimo, uvuvi na ufugaji ambao unategemea zana duni na teknolojia duni haziwavutii vijana kwenda katika ajira hizi. Kwa hiyo, lazima tufanye *something* ili wavutike kwenda kule. Udogo wa Sekta ya Viwanda ambayo ni tegemeo katika ajira, nalo ni tatizo, nimelizungumza. Lazima tuanzishe viwanda, lazima tuwekeze na wawekezaji wa ndani wachangie na wawekezaji wa ndani wengine wako humu humu na wengine nawaona hapa. Kawekezeni kwenye viwanda tuajiri vijana hawa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya mimi sio mwekezaji. Ongezeko kubwa la vijana wanaohitimu katika Vyuo Vikuu nimelieleza na lenyewe ni moja katika kuchangia tatizo hilo. Uchache wa Taasisi zinazotoa elimu ya ufundi nayo ni *problem*. Kukosekana kwa mikopo na mitaji nafuu kwa vijana hawa kunachangia. Hali ya ajira ya mwaka 2013/2014, Serikalini fursa zilizopatikana zilikuwa 630,616 ya ajira zilizozalishwa. Mwaka unaokuja wa fedha tunaouzungumza, tunakusudia zitakuwa ajira 700,000. Lakini watu wanaoingia kwenye ajira kwa mwaka ni wengi zaidi kuliko hizi. Kwa hiyo, hizi ajira hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya jitihada ambazo Serikali inataka kufanya, kwanza nimesema tumeanzisha Benki ya Kilimo na inaanza. Tunadhani vijana hawa wanaweza kuwa wateja wa Benki hii. Maana kama wanaingia kwenye kilimo, lazima waingie na teknolojia ya kisasa ambayo inauzwa. Lazima wapate mitaji ya kununua teknolojia hiyo. Kwa hiyo, nadhani Benki hii inaweza ikafanya, na vijana wa Tanzania ndio wengi, sasa wakulima wa Tanzania watakuwa vijana. Hata ukisoma takwimu zilizopo sasa hivi, asilimia karibu 90 ni vijana wenyewe. Sasa hii Benki itamkopesha nani? Lazima iwakopeshe hao wanaokwenda kufanya kazi hiyo.

Kwa vile vijana wanapendelea shughuli zinazowaingizia pesa haraka, hawataki hii mitulinga hii ya kungoja miezi sita, biashara ndiyo inawavutia zaidi, ufugaji wa kuku, ufugaji wa samaki na nyuki na kilimo chenye mazao ambayo yanaitwa *high value,* matunda na mboga mboga.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali tunataka kutoa kipaumbele kwa vijana katika maeneo haya ambayo wakiwekeza na wakakopesheka, wanaweza kuzalisha zaidi na wakaongeza uchumi wa nchi yao. Kutekeleza *program* ya vijana ambayo ameieleza Mama Kabaka, ya miaka mitatu ikiwemo mafunzo kwa wajasiriamali na utoaji wa mikopo, nataka niseme huko nyuma tulikuwa na Mfuko unaitwa Mabilioni ya JK. Sasa hivi mabilioni yale yanafanyiwa tathmini na Baraza la Uwezeshaji. Lakini tumekubaliana na mwenye mabilioni yake, fedha hizi sasa tuziingize zisaidie katika kutoa mikopo kwa vijana ili vijana hawa wanapotaka kujiajiri, tuweze kuwakopesha kupitia hii pesa.

Wengine wanaweza kukopa kupitia Benki, wengine wanaweza kukopa kupitia mifuko mingine. Huu Mfuko na mpango huu ambao Mama Kabaka hakupata muda wa kuueleza kwa kirefu unakusudia kuzalisha ajira 10,000, itakayotoa fursa kwa vijana 840,000 na ajira 300,000 za moja kwa moja na 540,040 zisizo za moja kwa moja.

Kuimarisha Mfuko wa Vijana na Wanawake kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *TASAF* na Mfuko wa Mikopo ya Wajasiriamali *SELF* ambao tunaugeuza kuwa kampuni ili uweze kuwa wa kudumu badala ya kuwa mradi. Kuboresha mazingira ya kuwekeza na kufanya biashara nchini na kuwezesha Sekta binafsi kukua na hivyo kutengeneza fursa nyingi za ajira.

Kama nilivyosema awali, ukosefu wa ajira ni mkubwa na kusema kweli hakuna majibu ya rahisi. Panahitajika mikakati ya makusudi kukabiliana na hali hiyo. Hivyo Serikali itashirikiana na wadau mbalimbali kuendelea kuchambua tatizo hili na kubaini hatua zinazotakiwa kuchukuliwa. Pamoja na kuongeza uwezeshaji wa wananchi kuwekeza katika viwanda vidogo

na vya kati, kusaidia wananchi kuibua miradi ya kibiashara inayofungamana na masoko ambayo yana uwekezaji mkubwa.

Kuweka mfuko katika tanisia ya burudani; na yenyewe inaajiri vijana wengi sana. Mliwaona hapa juzi wakati wanatumbuiza pale. Nchi nyingi kama Nigeria, tasnia ya filamu kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Kahigi pale, inaajiri watu wengi sana na inaleta uchumi mkubwa. Kwa hiyo, vijana wale wanaweza kuwa-*encouraged* kwenda katika tanisia hiyo ili na sisi tuweze kupata uchumi unaotokana na kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo ni jambo la ajira. Limenichukulia dakika zaidi lakini bado sijamaliza.

Mheshimiwa Spika, liko suala la Machinga limesemwa hapa. Nataka wale waliolalamikia Machinga wanisikilize vizuri. Maana na Machinga nayo ni ajira, wamejiajiri vijana hawa. Wametoka vijijini kwa sababu hakuna fursa, wamekuja mijini na wameamua kuja kufanya biashara, *they are there!* Nasi hatuwezi kufikiri kuwa hawapo, haiwezekani!

Sasa kuhusu Machinga hawa, kumekuwa na migogoro mingi na mimi ningependa kutoa ushauri wa namna mbili kuhusu Machinga. Kwanza, nashauri Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji wawashirikishe Viongozi wa Machinga katika kutafuta maeneo ya kufanyia biashara, wawashirikishe, nasema. Wasiwashirikishe kwa kutumia Polisi, wawashirikishe kwa kuongea nao. Hatua hii ya ushirikishaji zitasaidia kupunguza matumizi ya nguvu zisizokuwa za lazima, maana watakuwa wameelezwa, wameelewa, wameshiriki katika kuweka maeneo yanayofaa.

Kule ambako hatua hii imechukuliwa, uhasama umepungua, na Mheshimiwa Wenje amezungumza sana jambo hili hapa na alikuwa anangojea kauli ya Serikali na bado itatolewa. Mimi na-*wind-up* sitoi kauli nyingine hapa. Mimi na-*wind-up*. Lakini nataka niseme kwamba Mwanza pale kwa Mheshimiwa Wenje, ni mahali ambapo jitihada kubwa sana zimefanyika kuwashirikisha Machinga kutafuta maeneo. *(Makofi)*

Tena nataka nimwambie Mheshimiwa Wenje, naye alishiriki. Maana wakati jambo hili linafanyika, Meya wa Mwanza alikuwa wa CHADEMA, anaitwa Manyerere. Walifanya na walitembea Mji wote wa Mwanza kuangalia namna wanaweza kupata maeneo na wakapata maeneo 12 ambapo Viongozi wote wa machinga na Viongozi wa *Council* ya Jiji la Mwanza walikubaliana kwamba ndiyo maeneo yanafaa kwa Machinga. *(Makofi)*

Sahara Stand ya zamani, *Market Street,* Sinai Mabatini, Darajani, *Pamba Road,* Mirongo, Makoroboi, Asante Moto, Mrango Mmoja, Uchochoro wa *Tanganyika Bus,* Nyegezi, Kileleni na Buzurugu. Yalitengwa maeneo hayo kwa ushirikiano na kwa kushirikisha Viongozi wa Machinga. Hayo ndiyo maeneo yaliyoruhusiwa.

Sasa eneo ambalo limeleta fujo juzi lilizuiwa lisifanyie shughuli za biashara kwa sababu ni Msikiti. Ni Msikiti! Sasa wewe wenzako wanasali ndani ya Msikiti, wewe unauza nguo kwenye ukuta wa Msikiti, aah bwana! Sisi Serikali tunalinda haki ya watu kuabudu. *(Makofi)*

Sasa pale pamezuia na maeneo haya 12 yaliyotengwa yana nafasi ya hawa kwenda, lakini wao wanakwenda pale. Tena wanaenda pale wanajikita, wale wanasema huku, wanamwita Mungu; wao wapo pale, wanauza na hawaitikii kinachosemwa ndani. Hii siyo sawa! Nasema hiyo siyo sawa! *(Makofi/Kicheko)*

Mkipewa maeneo halafu mkakubaliana halafu mkayaacha, mkaenda Msikitini kufanya biashara, Serikali ina wajibu wa kuhakikisha wale walioko Msikitini nao wanalindwa. *(Makofi)*

Ushauri wa pili ambao ni wa wanasiasa pamoja na mimi ni kwamba tushirikiane na Mamlaka zilizopo ku-*solve problem* hii kwa njia ya amani ya kuteua na kushirikisha viongozi. Maana Machinga karibu nchi nzima wana Viongozi wao, tuseme nao, tuwashirikishe, tuondokane na *problem* hii. Nami ni mwanasiasa huwa natafuta kura. Lakini usifanye kura hii ya kutafuta kwamba ukiwaambia wafanye fujo eti watakuchagua. Wale ambao wanafanyiwa, watakunyima. Sasa inategemea zipi zitatosha, ni wale wanaofanya fujo au wanaofanyiwa? *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, hii wala haisaidii sana. Huo ni ushauri wa bure, hauna gharama. Tena inatokana na *experience*. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Taarifa Mheshimiwa Spika!

SPIKA: Mheshimiwa kwa sababu tuna- *runoff time*, nitakuita baadaye.

MBUNGE FULANI: Taarifa Mheshimiwa Spika!

SPIKA: Nitakupa baadaye! Naomba ukae.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, hao waache, watasikiliza tu; mambo yakinoga watanyamaza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kutotenga asilimia 35 ya bajeti yake, tumejitahi sana. Tumejitahidi sana kwa mazingira ya uchumi wetu na kwa miaka miwili mfululizo bajeti ya maendeleo imezidi asilimia 30 na sasa 32 mwaka huu. Lakini vile vile jambo la kujivunia zaidi ni kwamba kwa mwaka huu, asilimia 66 ya bajeti ya maendeleo itatokana na mapato ya ndani badala ya kutegemea mapato ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kutambua pia kwamba sehemu ya fedha zinazotumika katika kugharamia maendeleo, bado zinakuwa katika fedha za matumizi ya kawaida kwa sababu kuna *elements* za matumizi ya kawaida kama chanjo, unaziita ni za matumizi ya kawaida lakini kwa kweli ni *development oriented*. Kwa hiyo, kwa kweli tunapiga hatua katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni ushiriki wa Sekta Binafsi. Sekta Binafsi tunaikaribisha sana wala sisi hatuna ugomvi nayo, na tumeshauri hivyo na Mheshimiwa Mtemi Chenge wakati alipokuwa anawasilisha hoja ya Kamati, nasi tunakubaliana naye kabisa kwamba Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano umesisitiza kuwa sehemu kubwa ya rasilimali fedha ya kutekeleza mpango utachangiwa na sekta binafsi. Kwa wastani, ilikadiriwa kuwa gharama ya mpango kwa mwaka ingekuwa Shilingi bilioni 8.9. Sekta ya Umma ichangie 2.9 na Sekta ya Binafsi ya ndani na nje ichangie Shilingi trilioni 6.

Pamoja na changamoto za upatikanaji wa takwimu sahihi za uwekezaji wa Sekta Binafsi, ipo mifano halisi inayodhihirisha mchango mkubwa wa Sekta Binafsi katika maendeleo ya nchi yetu. Miradi ya makaa ya mawe na chuma kule Mchuchuma na Liganga ambao utekelezaji wake sasa wawekezaji wako *site*. Ujenzi wa viwanda vikubwa vya saruji kama vile vya Dangote na kile cha Lindi kinaitwa *MEIS*. Uwekezaji kwenye miradi mikubwa ya gesi asilia na uwekezaji wote uliofanyika katika utafiti wa gesi na mafuta unafanywa na Sekta binafsi kwa gharama kubwa. Vipo Vituo vya Afya, vile vile shule ambazo zinajengwa na watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Sekta Binafsi inaendelea kuchangia katika maendeleo yetu lakini tungependa ichangie zaidi. Sehemu nyingine ni ya uwezeshaji wa Sekta Binafsi ndani, kwa maana kuwezesha ushiriki wa Sekta Binafsi ya ndani katika kutekeleza mpango.

Nimelieleza hili na ningependa kwa kweli kutoa wito kwa wawekezaji wa ndani. Tume ya Mipango itashirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda kuitisha Kongamano la wafanyabiashara hao, tuzungumze nao tusikie wao wanasema nini? Wangependa Serikali tufanye nini ili waweze kupata motisha katika kuwekeza? Kwa sababu uchumi wetu utakuwa tu ikiwa tutawekeza katika Sekta ya Viwanda na vile vile tatizo la ajira nililolizungumza litapungua.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nalo limezungumzwa hapa, linahusu utekelezaji wa miradi ya makaa ya mawe na chuma. Hili lilizungumzwa zaidi na Mheshimiwa Hilda Ngoye. Tunajua kwamba mradi huu umeshaanza, changamoto iliyokuwa pale ni kutengeneza barabara, *access road* ya kuingia mpaka kule Liganga. Sasa hivi kazi hiyo inafanyika na tunadhani baada ya kumalizika ile barabara, mitambo kwa ajili ya kujenga viwanda vya pale itaanza kuingia pale Mchuchuma.

Kwa hiyo, nadhani hili jambo ambalo tunaliendeleza na litaendelea kusimamiwa kwa sababu hii itatupa msingi mkubwa wa uchumi mkubwa katika siku zinazokuja.

Hivi ni viwanda ambavyo vitaanzisha viwanda vingine. Vitategemewa vitatoa rasilimali kwa viwanda vingine, yaani vinaitwa viwanda mama. Kwa hiyo, hapo kabisa ni kufa na kupona nchi yetu lazima iwekeze.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa nitakuwa najibu hoja zilizotolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Kama ya kwako haitafikiwa, ni kwa sababu ya muda tu, lakini nia ni njema kabisa. Kwanza kabisa ilitoka kwa Kamati. Inasema, Serikali iendelee kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya matokeo makubwa sasa ili matokeo yake yaonekane katika muda uliopangwa. Sisi tunakubaliana na suala hili kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Matokeo Makubwa Sasa ukilinganisha na umri wake, matokeo yameanza kuonekana. Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, maana mmesimama hapa mnasema umeme kwangu umewaka. Ndiyo yenyewe hayo! Matokeo makubwa. Maji, yameanza kupatikana katika baadhi ya maeneo. Wala hatukusema matokeo makubwa yatapeleka maji kila kijiji. Ukisema hivyo na wewe nawe utakuwa kichwa chako siyo kizima, maana vijiji ni vingi. Lakini unaweza kufikisha maji kwa kiwango fulani.

Matokeo makubwa kulingana na maabara, tulikubaliana kwamba tunaweza kupeleka maji kwa watu milioni saba katika muda wa miaka mitano. Tumepeleka 2.6, kazi inaendelea na watu wa maji wameshakiri hapa kwamba wameshapewa pesa ili miradi ambayo haijawa tayari iendelee. Sasa unataka matokeo makubwa ya namna gani? Si ndiyo hayo sasa! Tena pamoja na matatizo tuliyoyapata ya kibajeti ya upungufu ya rasilimali fedha, lakini matokeo yamekuwa makubwa.

Suala la *PPP* tutalizungumza Bungeni hapa, maana Muswada wake unaletwa. Ni kweli tunahitaji Sheria ile irekebishwe, ili iweze kuwa *friendly* kidogo iweze kufanya kazi ya kukaribisha Sekta Binafsi kwa jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa hoja nyingine zilizotolewa hapa zilitolewa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko. Sielewi ni kwa nini Mheshimiwa Mbowe alimweka Mheshimiwa Esther kuwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa mambo yangu, maana Mheshimiwa Esther ni shemeji yangu. Sasa hatuwezi kufanya mambo ya kishemeji-shemeji ndani ya Bunge. Lakini mradi… *(Kicheko)*

Eeeh, ni shemeji yangu, sasa wewe umeona anabisha! Si yule kule! Kwani umemsikia anabisha? Hawezi kubisha, maana akibisha hapa atapata matatizo, maana hata yule bwana anamwangalia. Kwamba, anakataa, anamkana shemeji yake Bungeni. Lakini pamoja na hayo, sasa tutaacha ushemeji, tuzungumze kazi hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hoja ya kwanza ya Mheshimiwa Esther, anasema Taarifa ya Mpango wa 2013/2014 inaonesha kuwa wananchi 70,002 tu ndio walikuwa wanaunganishiwa umeme kuanzia Julai, 2013, lakini Taarifa ya sasa inaonesha watu 138,931. Sasa anauliza imewezekanaje watu 68,000 wakaunganishiwa kwa kipindi kifupi?

Mheshimiwa Spika, jibu lake analo Mheshimiwa Muhongo. *Big Results Now!* Ndiyo *Now* yenyewe hiyo! Eeh! *That is the big results!* Maana *Big Results Now* ni *business unusual.* Ndiyo maana hata hii ni *unusual, that is it!* Sasa kama Mheshimiwa Esther alikuwa hajajua kumbe *unusual* ni ipi? Ndio hii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wa kilimo; atajifunza tu, mwisho wa yote atakuwa mtaalamu hapa. Mchango wa kilimo kwenye pato la Taifa umeendelea kudorora ambapo mchango wa kilimo ni 4%. Hapana, hapo napo kuna tatizo.

Mheshimiwa Spika, nataka nisahihishe. Kuna kukua kwa kilimo na mchango wa kilimo. Mchango wa kilimo kwenye pato la Taifa uko kati ya 24% na 26%, lakini kilimo kwa miaka miwili ndio kimekua kwa 4.3% ya pato la Taifa kwa mwaka mmoja, lakini sekta yenyewe inachangia 24% mpaka 26%. Haya ni mambo ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo lilizungumzwa sasa na Mheshimiwa Mbatia, anasema Serikali iweke wazi ni hatua gani hadi sasa zilifikiwa katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano?

Mheshimiwa Spika, hii ni hoja nzuri tu, ni mtu anataka kujua. Nami nataka kumwambia, sasa hivi tunafanya tathmini. Tunataka tutakapokuja Bunge katika hili tutoe tathmini ambayo imekamilika na tunadhani kufikia Desemba, Tume itakuwa imemaliza kazi ya kufanya tathmini, ili tuje tuseme tumepiga hatua kiasi gani, tumefeli wapi katika utekelezaji wa huo mpango.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliambie Bunge Tukufu ni nini kikwazo cha kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano?

Mheshimiwa Spika, vikwazo vipo, lakini sio kwamba vinazuia kutekeleza. Mpango unaendelea kutekelezwa na malengo tuliyojiwekea yapo. Tumesema miundombinu, mmewasikia wenye kusimamia utekelezaji. Waziri wa Barabara ametengeneza; hakusema yeye, lakini barabara zinaendelea kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, miundombinu mingine ni reli; *study* imekamilika. Watanzania wanachotegemea kwao ni kufanya maamuzi tu ili tuanze kujenga reli mpya zaidi. Maana ile ilijengwa miaka ya Wajerumani.

Kwa hiyo, kazi inaendelea, lakini huwezi kuanza kujenga reli kabla huja-*study*. *Study* imekamilika, wataitazama halafu tutaona jinsi hatua nyingine inayofuata, lakini nia ni hiyo.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya umeme; gesi inatolewa Mtwara, tena kwa kasi kubwa, ili tuondokane na *problem* ya kutegemea mafuta mazito ambayo yanatu-*coast* kweli kweli! Ndiyo tunatekeleza Mpango. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbatia tutakuja kufanya *study* halafu baadaye tutaliambia Bunge wakati ukifika, utekelezaji umefikia wapi. Maana hiyo hatua

na *study* hiyo ndiyo itatusaidia kutengeneza Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano inayokuja.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine, Mheshimiwa Mbatia anashauri kwamba, katika Bajeti ya Mwaka 2014/2015, vipaumbele vingekuwa afya, utawala bora, elimu, nyumba na makazi, michezo na sanaa, ajira na ulinzi, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sisi tunasema siyo mawazo mabaya. Lakini sasa ngoja tuje tuanze kutengeneza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ili tuone. Maana vipaumbele vya mpango huu ndiyo hivi tunavyotekeleza, hatuwezi kubadilisha katikati, lakini mpango ujao sasa tutatazama haya maoni na mimi naomba ayaweke ili yaje yatusaidie huko mbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo yanayohusiana na mchango wa wenzetu katika Kambi ya Upinzani, sasa nizungumzie wengine waliosema. Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, yeye alisema pato la mwananchi sasa hivi ni Dola 700. Anauliza: Je, mwenendo huu tutaweza kufikia kiwango cha Dola 3,000 ifikapo mwaka 2025?

Mheshimiwa Spika, swali zuri tu! Ni swali zuri na swali ambalo limechingwa vizuri kwa makini. Lakini tunachosema ni kwamba, pato la wastani la mwananchi mwaka 2013 Dola 742. Tangu Dira ilipoanzishwa mwaka 2000, pato la mwananchi lilikuwa Dola 319. Sasa leo liko 742. Ukifanya mahesabu, utaona hili pato linakua kwa asilimia kadhaa.

Mheshimiwa Spika, ikiwa uchumi huu utabaki hivi hivi bila mabadiliko, pato letu litakuwa Dola 1,657 ifikapo mwaka 2025. Bado tutakuwa tumeingia kwenye uchumi wa kati, lakini kwa daraja la chini. Ila ukitaka kufika 3,000 uchumi lazima ubadilike. Nasi tunadhani, kwa miaka 10 iliyobakia, uchumi utabadilika kwa sababu utakuwa uchumi wa gesi; utakuwa uchumi wa chuma cha Liganga. Kwa hiyo, lazima *economy* ita-*pick up,* na lazima itabadilika.

Kwa hiyo, tunadhani ukuaji huu unaweza ukatufikisha huko tunakotaka kwenda. Suala ni kujipa matumaini, na ukiweka Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu, usiwe na haraka nao; ni lazima ufanye kazi kwa bidii ku-*achieve* hicho unachotaka kukipata.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Haroub Shamis anasema kasi ya ukuaji wa uchumi ni ndogo, Bajeti ya Mwaka 2015 haiendani na Malengo ya Dira. Yeye anasema, kwa maoni yake, inakua kwa 0.1%.

Mheshimiwa Spika, nadhani mahesabu tu ya Mheshimiwa Haroub ndio yaliharibika tu. Maana yeye alichoona ni kwamba, tulisema mwaka 2012 uchumi ulikuwa kwa 6.9%, halafu mwaka huu umekua kwa 7%. Sasa yeye anachukua ile moja, ile 0.1% anasema ndio kukua. Hapana! Nimeshaeleza maana ya kukua. Ni lile pato la Taifa la mwaka jana ukilinganisha na pato la Taifa la mwaka unaofuata.

Kwa hiyo, ukilinganisha unaona uchumi umekuwa *stable,* unaendelea kukua kwa asilimia zile. Hii nayo ni kaelimu kazuri tu.

Mheshimiwa Spika, aliendelea nafikiri mahali kusema imewezaje Tanzania kuwa nchi moja kati ya nchi ambazo uchumi wake unakua kwa kasi?

Mheshimiwa Spika, ni kama nilivyoeleza kwa jibu la Mheshimiwa Nyambari, uchumi wetu unakua katika nchi hizo za Afrika. Lakini kwa sababu sisi ni nchi masikini, *infrastructure* na mambo mengine hayapo ukuaji huo ndio unaweza ukaonekana *development* inakuwa *slow,* lakini jitihada zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Esther Matiko wakati akichangia sasa, kama mwenyewe siyo kama Msemaji wa Upinzani; maana amesema kama Mpinzani halafu akasema kama Mheshimiwa Esther. Hapo sasa alisema, katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Serikali iliahidi kutekeleza miradi 80 katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, lakini mpaka sasa ni takribani miradi 12 tu ndiyo imetekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hesabu hii mimi ilinishinda kujua ni miradi gani anayosema? Tunachosema ni kwamba, huu mpango ni wa muda mrefu na kuna miradi mingine huwezi kuitegemea ikamalizika kwa mwaka mmoja au hata miwili. Ukitaka kujenga Reli ya Kati huwezi kuijenga kwa mwaka mmoja! Utajenga kwa muda. Ukitaka kujenga bandari, nao ni mradi, na kuna miradi mingine ambayo itaanzwa, lakini itaendelea, itaingioa tena kwenye Mpango unaofuata kwa sababu ni miradi ya muda mrefu. Maendeleo siyo kitu cha kulipua. Maendeleo ni *progressive*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, kama unajenga nyumba, ukishamaliza msingi, unaanza matofali. Ukianza matofali, unaweka paa. Huwezi kuanza na paa halafu ndiyo ukaweka matofali. Lazima uanzie chini, unakwenda! Kwa hiyo, ni *progressive!* Kwa hiyo, nilitaka kumtia moyo Mheshimiwa Esther kwamba, mambo yanaenda vizuri tu asiwe na wasiwasi sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa David Silinde anasema vipaumbele ni vingi na miradi ya maendeleo haitekelezwi kwa tija kutokana na kuwa ni vingi. Hapana! Labda useme miradi ndiyo mingi, lakini vipaumbele ni vilevile vitano. Ni vitano tu. Ni miundombinu, ni kilimo, ni viwanda na rasilimali watu ambayo inajumuisha elimu, afya, na kadhalika. Ni hivyo hivyo!

Hata ukienda kwenye *BRN* utavikuta ni hivyo hivyo! Utakuta ni miundombinu, reli, nishati, barabara, *agriculture,* halafu elimu; ndiyo vipaumbee vyetu. Hicho ni cha kwako! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu anasema utekelezaji wa miradi ya *BRN* fedha zinatolewa kwa ajili ya utekelezaji, ila mpango haujaainisha *Key Performance Indicators.*

Mheshimiwa Spika, mpango huu una *Key Performance Indicators.* Wale Mawaziri wote ambao wanasimamia sekta zenye *BRN* wanazo *indicators* ambazo ndizo zinatumika kupima *performance*. Kwa hiyo, kama mambo hayaendi, wanaenda na hizo *indicators*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ernest Silinde alisema miradi ya maendeleo, hususan ya barabara, haitekelezwi kwa wakati na hivyo kuongezea mzigo gharama.

Mheshimiwa Spika, hatukupata nafasi ya kumsikiliza Dkt. Magufuli, lakini hili jambo limeelezwa vizuri wakati Mheshimiwa Magufuli akiwa analeta hoja yake hapa. Kwa hiyo, mimi sidhani kama kuna jipya sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, yeye alikuwa na matatizo yake ya barabara ya Kidahwe – Nyakanazi. Tumeshamjibu kwamba ile barabara kama zilivyo barabara nyingine, iko katika mpango na inasimamiwa na Wizara ya Ujenzi, inajengwa kutokea pande mbili; na Waziri Dkt. Magufuli alishaeleza hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Machali alikuwa ameuliza kitu kinachofanana na hicho kwamba, hotuba inakinzana na takwimu zilizoko mle. Lakini nilishamjibu yeye mwenyewe nje ya Bunge kwamba, ile ilikuwa ni *typing error.* Suala ni kilometa 50 huku na 50 upande wa pili, jumla zinakuwa kilometa 100, ambazo ndizo zinapewa Mkandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Selemani Jafo alitaka Serikali ifanye haraka kukamilisha Bandari Kavu ya Kisarawe. Tunakubaliana naye na maandalizi ya kutekeleza mradi huo wa Kisarawe yameanza. Mtaalamu Mwelekezi, *Royal Hosting* wa Uholanzi anatarajiwa kuanza kazi ya kufanya upembuzi yakinifu Julai hii inayokuja na kukamilisha mwezi Januari, 2015.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gudluck Ole-Medeye alisema Serikali ijenge barabara, hususan maeneo ya Vijijini. Tunakubaliana naye, kwa sababu usipojenga na ukajenga *Highways* ambazo hazina *connection* na Vijiji, bado huja-*solve problem*. Kwa sababu uchumi uko Vijijini hasa wa kilimo na lazima barabara zile ziwe *connected*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mariam Kisangi alisema kasi ya ujenzi wa barabara za pembeni za kupunguza msongamano Dar es Salaam kama Mbagala – *Jet* – *Airport* – Tabata zipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, ushauri wake tumeuzingatia. Alielezea Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Serikali inaendelea na kazi ya ujenzi wa barabara na kupunguza msongamano Dar-es-Salaam. Kwa upande wa barabara ya Mbagala – *Jet* – Kona, imekamilika kwa kiwango cha lami.

Katika Mwaka 2014/2015 barabara ya Msongora – Kivule – Kitunda itajengwa kilometa tatu kwa kiwango cha lami. Eneo la Kitunda hadi Kivule na barabara ya Kinyerezi – Kifurumsingwa – Mbezi Louis itajengwa kilometa tatu kwa kiwango cha lami. Hayo ndio majibu tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ritta Kabati alikuwa anataka tu kujua juu ya Uwanja wa Ndege wa Nduli kule Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasema, ule uwanja wa Nduli uko kati ya viwanja 11 ambavyo viko katika *priority* vinavyofanyiwa kazi na ambavyo vitaingizwa katika mpango baada ya usanifu kukamilika.

Kwa hiyo, viko viwanja vingine 11, siwezi kuvitaja hapa kwa sababu muda wenyewe; na hata hivyo Mheshimiwa Kabati hakutaka vingine, alitaka hicho hicho tu cha kwake, cha Nduli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, alitaka kujua ni mkakati gani umewekwa kwa ajili ya kuendeleza kiwanja cha ndege cha Tanga?

Mheshimiwa Spika, jibu lake ni kwamba, sambamba na viwanja vingine 11 katika mwaka 2014/2015 Serikali imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kiwanja cha ndege cha Tanga. Mhandisi Mshauri alianza kazi hiyo mwezi Aprili, 2014 na anatarajiwa kukamilisha mwezi Februari, 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda alisema Mpango haujaainisha jitihada za kumaliza ujenzi wa daraja la Kilombero kwa kuwa fedha iliyotengwa ni Shilingi bilioni saba tu kwa mwaka 2014/2015 wakati gharama ya kumaliza ujenzi wa daraja hilo ni takribani Shilingi bilioni 37.

Mheshimiwa Spika, jibu lake ni kwamba, mradi huu ulianza kutekelezwa Januari, 2013 kwa gharama ya Shilingi bilioni 55 ambapo mpaka Mei Mkandarasi amelipwa Shilingi bilioni tisa amekamilisha 10% ya kazi. Kwa hiyo, pesa itaendelea kupatikana na ujenzi wa kujenga hili daraja utaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda aliendelea kuzungumzia juu ya miradi ya barabara katika ukanda wa *SAGCOT,* miradi ya *SAGCOT* miongoni mwa miradi yenye kuleta matokeo makubwa sasa. Hiyo barabara inayopita kwenye maeneo ya *SAGCOT* iko katika mpango.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe aliuliza mbona miradi ya umeme tangu mwaka 2005 inasemwa, lakini bado haijakamilika? Swali hili limejibiwa. Nadhani anaweza kulijibu vizuri Mheshimiwa Profesa Muhongo, lakini habari tulizonazo kwenye Tume ni kwamba, Mradi wa *North West* ulishapitia hatua hiyo ya upembuzi yakinifu. Lakini Serikali iliamua kuongeza uwezo kutoka *KV 220* kwenda *KV 400.* Hii inalazimisha kudurusu upembuzi yakinifu.

Katika Mwaka 2014/2015 mradi utafanyiwa usanifu wa kina, *detailed design,* kulipa fidia na watakaopisha mradi wa kupima Mkuza kutoka Mbeya hadi Sumbawanga. Mradi wa *North West Grid* unatarajiwa kukamilika mwaka mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ignatus Aloyce Malocha alisema Serikali nipeleke umeme haraka katika Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, jibu lake linafanana na hilo hilo, maana hiyo ndiyo itatokea kwenda Sumbawanga mpaka itafika kule inakokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Horoub Othman anasema, kusuasua kwa utekelezaji wa miradi ya umeme, kama vile Kinyerezi na Kiwira, sasa imekuwa ni takribani miezi 40.

Mheshimiwa Spika, hili nadhani limeelezwa vizuri na Profesa na inasimamiwa vizuri pale kwa nguvu ya sayansi na teknolojia. Lakini habari tulizonazo sisi ni kwamba, *Kinyerezi One,* mitambo ya ujenzi na njia za usafirishaji umeme hadi vituo vya kupoozea umeme vya Kimara na Gongo la Mboto unaendelea. Mradi huu utakamilika mwaka 2014/2015.

Kinyerezi Two mwaka 2014 mitambo ya kufua umeme itaagizwa na kufungwa na Mkandarasi ambaye anaitwa *Mitomo Corporation* kutoka Japani. Mradi utakamilika mwaka 2015/2016.

Kinyerezi Three, utatekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Katika mwaka 2014/2015 kazi zitakazofanyika ni kukamilisha upembuzi yakinifu, tathmini ya athari za mazingira na kijamii, kukamilisha Mkataba wa Ubia wa Uundwaji wa Kampuni ya Ubia na uteuzi wa Wajumbe wa Bodi, kuendesha *Kiwira Coal Project, Mega Watt 200.*

Hatua iliyofikiwa ni kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la ujenzi wa mitambo. Njia ya umeme msongo wa *KV 400* wenye urefu wa kilometa 100 kutoka eneo la Mgodi hadi Uyole.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo alizungumza sambamba na ujenzi wa bomba gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam, miradi mingine ya miundombinu kama barabara na uwanja wa ndege anashauri itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, nasema ushauri unazingatiwa kwa sababu, uwanja ule wa Mtwara na kwa nguvu na ukubwa wa uchumi unaoelekezwa Kusini kutokana na gesi na viwanda, hakuna namna unavyoweza kupuuza ukarabati au ujenzi wa kiwanja hiki cha Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, tena, alizungumzia na wengine wengi; Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa James Daudi Lembeli na wenye

maandishi walizungumzia Reli ya Kati. Nadhani Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi amefanya kazi ya kutueleza vizuri kuhusu Reli ya Kati na hatua zilizofikiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani aliuliza, vichwa vya treni vinavyoagizwa na Serikali ni vingapi?

Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Waziri ameshalijibu na jibu lake ameshalipata.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala kwamba Serikali iliahidi kutengeneza barabara katika kiwango cha lami kutoka *Old Korogwe* kwenda Bumbuli. Nasema katika bajeti ya mwaka 2014/2015 barabara hii imetengewa Shilingi bilioni 120 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, ndiyo mwanzo wenyewe wa kuendelea.

Mheshimiwa Nyambali Nyangwine aliuliza, kilimo ni miongoni mwa Sekta za *BRN* lakini ardhi ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya kilimo haijajumuishwa katika *BRN*. Nasema, hili ni jambo la kweli na tumeshaliona, lakini tunaenda hatua kwa hatua. Tunadhani hatua itakayofuata ya *BRN,* ardhi itaingizwa kwenye *BRN* ili ku-*balance* kati ya *agriculture* na *land development*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, alisema Tanzania licha ya kuwa na mifugo mingi haina viwanda. Hili nalo limeshajibiwa na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo. Sisi tunadhani ni vizuri ku-*encourage private sector* waanze kuingiza kwenye mipango ya ujenzi wa viwanda vya nyama ili tuweze kuuza mazao ya mifugo na kujipatia fedha za kigeni kuliko hali ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Daffa Shekifu, alisema Serikali isaidie wakulima wadogo kwa kuwapa pembejeo. Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge unazingatiwa ipasavyo, na mpango wa miaka mitano unasisitiza juu ya ukuzaji wa kilimo.

Mheshimiwa Stella Manyanya, alisema masoko ya mazao ya kilimo siyo ya uhakika. Nakubaliana naye kabisa, ndiyo maana kwa kweli tunaanzisha ile kitu inaitwa *agriculture commodity exchange*. Sasa hivi kwa kweli katika eneo ambalo hatujafanikiwa sana, niawaambie wakulima, tuli-*liberalize* tukategemea kwamba tutaweza kutumia sekta binafsi kununua, lakini matatizo ni makubwa kuliko tulivyoyategemea.

Waheshimiwa Wabunge, nataka nimalize sasa hoja yangu kwa kusema yafuatayo:-

Kwanza niwashawishi Waheshimiwa Wabunge wote muunge mkono ili tupitishe bajeti, wote bila kujali Chama, kwa sababu huwezi kudai maendeleo na bajeti unakataa. Hiyo ni *contradiction*. Unataka maendeleo na bajeti hutaki, yaani unataka tukae kwenye mawe. Sasa tutafanyaje maendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema hivyo kwa sababu kuna *leader* wa *opposition* hapa na baada ya yeye kuondoka Mheshimiwa Mbunge naye alisema wanaosema ndiyo ni wanafiki. Lakini nilimsamehe kwa sababu ni kijana; unajua kukua kuna matatizo. Wakati mwingine ukifika *age* fulani hivi, unaweza kufanya mambo ambayo ukikua zaidi kidogo unashangaa kwanini ulikuwa unayafanya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huwezi ukawaambia watu wa CCM wakatae bajeti, na sera ya kwao na ilani ya kwao, eti wavunje Serikali, *hallow*! Yaani hata ungelala tu ukafikiri, ungeacha kusema hayo maneno, kwa sababu hayawezekani. Sisi wawindaji kule huwa tunatega mitego, lakini kwa

masharti, kwamba ukitega, wanyama wasikuone wakati unatega. Sasa wewe unatega na wanyama wanakuona, hawawezi kupita kwenye mtego wako. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, suala la Mheshimiwa Lugola, mambo mawili ya mwisho kabisa! Mheshimiwa Lugola amezungumzia rushwa, nami nasema rushwa ni *problem*, lakini haiwezi kumalizwa kwa urahisi na Serikali kupitia TAKUKURU. TAKUKURU inangonja taarifa.

Kwa hiyo, ni lazima jamii yote kabisa ichukie rushwa. Lakini jamii haiwezi kuchukia rushwa bila kuongozwa. Wanaotakiwa kuongoza ni sisi wote tuliomo humu. Lakini kabla hujaongoza, jamii inakuangalia; hivi huyu anatuongoza kuacha rushwa, anafanana na kuongoza?

Maana lazima uonekane kwamba kweli wewe una sifa za kuwaambia achani rushwa. Lakini kama unafanya miaka mitatu, halafu una ghorofa sita, na biashara huna na kodi hulipi, halafu unawaambia; utakuwa unasema tu. Kama mhubiri anavyosema, fuateni ninavyowaambia, maana siyo mimi, mimi ni msemaji wa Mungu, lakini msifuate matendo yangu. Lakini kwa sisi binadamu hapa, matendo yetu ni lazima. Wasifuate matendo yako, basi usiseme. Maana kuongoza ni kuonyesha njia.

Mheshimiwa Spika, tukubali, hii ni *problem! Is a cancer* kwa maendeleo yetu! Kila kitu kinaweza kuwa *substandard* kwa sababu ya rushwa. Kabisa! Nafurahi Waziri wa Fedha anataka kutazama ile Sheria ya Manunuzi, *is a problem also*. Mtu ananunua chupa Sh. 2,000/= na huku inauzwa Sh. 500/=, lazima kuna kichaa fulani hapo! *(Makofi)*

Mwisho kabisa, nawaomba wote tushirikiane katika kuhakikisha kwamba jamii yetu inakuwa na amani kwa sababu amani ndiyo pembejeo ya kwanza ya maendeleo. Kama hakuna amani, hata mfanyaje! Fujo tu, halafu mwendelee! Mbona Somalia haiendelei? Popote palipo na fujo kuna *problem*. Kwa hiyo, tubishane, lakini tukubaliane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, wakati namwongezea Mheshimiwa Waziri muda, nilikuwa nimetumia kifungu cha 28(2) siyo cha tano. Kwa hiyo, ni cha pili. Cha tano ni cha usiku; cha pili ni cha mchana. Mheshimiwa Kiwia.

TAARIFA

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru naomba nimpe taarifa mzungumzaji aliyetoka kuzungumza kwamba siyo kweli kwamba wafanyabiashara ndogo ndogo kwa jina la Machinga walivamia eneo la Msikiti na kufanya biashara na kusababisha ibada kutokufanyika katika mazingira ambayo ni tulivu. Wafanyabiashara katika maeneo haya ya Makoroboi Msikitini wamekuwepo kwa muda mrefu, wamekuwa wakifanya shughuli zao bila matatizo, na hata milango ya Msikiti kuweza kuwawezesha waumini kuingia Msikitini na kutoka bila tatizo lolote lile.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea ni Operesheni iliyofanyika usiku wa manane ambayo naifananisha na Operesheni yoyote ya kigaidi iliyoingilia maeneo ya wafanyabiashara hawa kwa maeneo ya Makorobohi na maeneo mengine Jiji la Mwanza na kuharibu vitu vingi na kuchukua mali nyingi na kuwasababisha wafanyabiashara wadogo wadogo kubaki katika hali ya umasikini na hali ya simanzi bila kujua nini cha kufanya.

Kwa hiyo, siyo kweli kwamba wafanyabiashara wadogo hawa wamevamia eneo la Msikiti. Ndiyo taarifa nilitaka kumpa mzungumzaji aliyetoka kuzungumza.

SPIKA: Ahsante, nashukuru, Mheshimiwa Mnyika! Mheshimiwa Waziri unataka ujibu? Haya, sawasawa, mtabishana hapa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, kwanza taarifa hiyo siikubali, kwa sababu nimefanya utafiti na angesimama hapa aseme maeneo niliyoyasema 12 kama hayakutengwa kwa ajili ya Machinga. Yapo na pale hayamo. Hapo yeye anapopasema hapakukubaliwa. Kwa hiyo, tunaendelea tu. *(Kicheko/Makofi)*

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na kanuni ya 105 (1) kwamba baada ya Bunge kukamilisha mjadala wa makadirio ya Wizara zote, ndani ya siku sita kabla ya Hotuba ya Bajeti kusomwa Bungeni, Serikali kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti itafanya majumuisho kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, hii kanuni ni kanuni ambayo kama kwa mwongozo wako ikitumika vizuri, inaweza kutunasua kwenye tatizo tulilonalo linalosabishwa na Katiba mbovu Ibara ya 90 ambayo…

MHE. MOSES J. MACHALI: Aaaaah! *(Kicheko/Makofi/Minong'ono)*

SPIKA: Mwacheni aseme nimsikilize mimi nataka kumwelewa! *(Kicheko/Makofi)*

MHE. MOSES J. MACHALI: Acheni fujo nyie!

SPIKA: Hebu endelea! *(Minong'ono)*

Waheshimiwa subirini bwana, tusikie! Endeleo Mheshimiwa Mnyika, na wewe Mheshimiwa Machali siyo kazi yako. Mheshimiwa Mnyika endelea! Endelea Mheshimiwa!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katiba Ibara ya 90 inasema, kama Bunge litakataa Bajeti ya Serikali, Rais analivunja Bunge. Katiba hii mbovu inafanya kwamba hata kama Wabunge wanaona bajeti ni mbaya, wanapiga kura ya ndiyo kwa kuhofia Bunge kuvunjika. Hii ni Katiba mbovu.

SPIKA: Sasa mwongozo ni nini?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nakuomba, kwa sababu kanuni ya 105 ilitoa fursa ya zile siku za majumuisho ambayo wakati tunapitisha bajeti ya kila Wizara, ulisema

tunachopitisha ni *provisional,* wakikaa kule kuna marekebisho yatafanyika. Lakini nimesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wakati anasoma bajeti, hotuba ya Kamati iliyopitia bajeti ya Serikali majibu ya Mawaziri ambayo wamejibu, hakuna taarifa mahususi iliyotolewa mpaka sasa kwamba katika zile siku sita ni Wizara zipi ambazo tulikubaliana wakati tunashika mishahara ya Mawaziri Serikali ilisema itakwenda kukaa na Kamati ya Bajeti na kufanya marekebisho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naelewa kwamba, naelewa kwamba, naelewa kwamba… *(Minong'ono)*

SPIKA: Sema vizuri ndiyo unayo…*(Minong'ono)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Naomba tusikilizane basi! *(Minong'ono)*

MBUNGE FULANI: Halafu wewe Mnyika, msumbufu sana wewe!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Wapo wanaodai kuwa, kwa kuwa watoa hoja; mtoa hoja mkuu, Waziri wa Fedha na Manaibu wake hawajajibu hoja, basi fursa hiyo ya kujibu kwao hoja, ndiyo itatumika kusema yale ambayo yamejitokeza kwenye majumuisho.

Mheshimiwa Spika, huku ni kuweka mkokoteni…

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie, huku ni kuweka mkokoteni mbele. Kwa sababu sisi Wabunge wakati Kamati ya Bajeti inasoma ripoti yake, wakati Waziri anasoma hotuba yake, angekuwa amesema hiki na hiki na hiki tumekubaliana; hiki na hiki na hiki kimerekebishwa, michango ya Wabunge ingekuwa tofauti, na mjadala ungekuwa tofauti kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako ili uwezeshe siyo tu majibu ya Mawaziri, bali taarifa kamili ya Kamati ya nini kilijiri katika zile siku sita, kipi kimekubaliwa, kipi kimekataliwa, iwasilishe hapa Bungeni ili ituongoze katika kufanya maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

SPIKA: Mwongozo siyo hotuba jamani! Hata uksoma kanuni, Mwongozo siyo hotuba. Utaratibu wetu uko hivi; baada ya kujadili hotuba zote, ziko siku sita na kazi hiyo imefanyika ya siku sita. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Mnyika nimemwandikia ki-*note,* nikimwambia karibu, ulikuwa haupo! Kamati ya Uongozi ilikaa, ikasikiliza yale yote ambayo walikubaliana kuyafanyia mabadiliko. Hivi leo kabla hawa hawajaingia, Mwenyekiti ataeleza maeneo gani wamekubaliana kufanya mabadiliko. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuko sahihi, lakini, naomba mnisikilize vizuri wote. Lakini tofauti kidogo ambayo anaieleza ni kweli kwamba mambo haya yalitakiwa yafanyike kabla ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango hajafanya na Waziri wa Fedha. Lakini kutokana na mfumo mzima wa Katiba, umebana nafasi. Matokeo yake, tumekubaliana kwenye Kamati ya Uongozi, tufanye haya tunayofanya leo, na kwamba hatukuacha hatua yoyote, isipokuwa tumekwenda *ahead* kwa sababu kulikuwa bado kuna mashauriano mengi sana yalikuwa yanaendelea. *(Makofi)*

Kikao cha Kamati ya Uongozi kilikaa na kikapitia, nami ndio nilikuwa Mwenyekiti, na taarifa atakayoisoma Mwenyekiti ni taarifa yangu mimi, kwa sababu kile kikao mimi ndio nilikuwa Mwenyekiti.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni, na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wote muwahi.

(Saa 7.32 mchana Bunge liliahirishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti! Ah, Makamu wake!

MHE. FESTUS B. LIMBU - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa kuniteua kuwasilisha taarifa hii katika Bunge lako Tukufu kwa niaba yao.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 98(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Bunge ya Bajeti ina jukumu la kuchambua mambo muhimu yalijotokeza katika Kamati za Kisekta wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014 unaoisha tarehe 30 Juni, 2013 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 unaoanza tarehe Mosi mwezi ujao, Julai. Aidha, kwa mujibu wa kanuni ya 105 (1) Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti imepewa jukumu la kufanya majumuisho kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta kama zilivyowasilishwa kwenye Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ninayoiwasilisha ni mrejesho kwa Bunge lako Tukufu wa matokeo ya majadiliano hayo. Hivyo ninayo furaha kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Kamati yangu imetekeleza jukumu hilo kikamilifu na kazi hiyo imefanyika tangu tulipowasili hapa Dodoma kwa ajili ya Mkutano huu wa Kumi na Tano wa Bajeti ulioanza tarehe 6 Mei, 2014.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu wa hoja za Kamati mbalimbali za kisekta unafanyika kwa mara pili tangu Kamati ya Bunge ya Bajeti uianzishe rasmi mwezi Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, nielezee jinsi Kamati ilivyofanya kazi. Kama ilivyofanyika mwaka 2013 Kamati imekutana na Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati zote zilizowasilisha hoja zao kwa Mheshimiwa Spika. Aidha, Mawaziri na Manaibu Waziri wa sekta zilizokuwa zina hoja, walifika mbele ya Kamati kwa ajili ya kutoa ufafanuzi kuhusu hoja hizo. Hatua hii ililenga kupata maoni yao kuhusu hoja hizo ili hatua zaidi ziweze kuchukuliwa kama inavyostahili.

Mfano, kwa maeneo ambayo yalihitaji fedha za nyongeza, Kamati ilihitaji kupata mchanganuo juu ya maombi ya fedha hizo kutoka kwenye Wizara husika ili kujiridhisha kuhusu uzito na umuhimu wa maombi ama mahitaji hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri wa Fedha ndio mwenye dhamana juu ya masuala ya fedha na bajeti, Kamati ilimshirikisha mara kwa mara wakati wa kusikiliza hoja za Kamati za kisekta kwa ajili ya kupata uelewa wa pamoja.

Aidha, Kamati ilifanya kazi kwa ushirikiano na wataalam kutoka Hazina kwa kuwa wao ndio wanahusika na uchambuzi wa mambo ya fedha pamoja na ugawaji wa fedha kwenye mafungu mbalimbali ya bajeti ya Serikali. Pamoja nao, Kamati ilishirikisha Wataalam kutoka Ofisi Rais, Tume ya Mipango kwa kuwa Tume hiyo ndiyo inahusika moja kwa moja na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wataalam hao walishirikiana vyema na Kamati katika kujadili na kushauri masuala mbalimbali yanayohusu taratabu za ugawaji wa fedha kwenye mafungu mbalimbali, hatua ambayo ilisaidia Kamati kufanya maamuzi. Aidha, kwa kuwa baadhi ya

wataalam hao walikuwa ni Wawakilishi wa Serikali, walikuwa wakiwasiliana na Serikali mara kwa mara kwa ajili ya kupata maelezo kuhusu maombi ya fedha za nyongeza na kutoa ufafanuzi wa hoja nyingine ambazo zilihitaji maelezo ya ziada.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha ufuatiliaji wa hoja hizo, Kamati yangu imeainisha hoja hizo na namna zilivyoshughulikiwa katika mfumo wa bango kitita lililoambatanishwa pamoja na taarifa hii ambayo naamini imeshagawiwa na kama haijagawiwa, basi inaendelea kugawiwa. Bango kitita hilo lina sehemu ama *column* kuu tano.

Column ya kwanza inahusu hoja za Kamati za kisekta zilizoletwa kwenye Kamati na *column* ya pili inahusu maelezo ya Serikali ambayo yametolewa kupitia wataalam kutoka Hazina na Tume ya Mipango walioshiriki katika vikao vya Kamati.

Sehemu ya tatu au *column* ya tatu ni maelezo ya Kamati ya Bajeti; na *column* ya nne inahusu kiasi cha fedha zilizoridhiwa na Kamati ya Bajeti na kupendekeza zitolewe na Serikali; na sehemu ya tano ni kiasi cha fedha ambacho Serikali imeridhia kuongeza.

Mheshimiwa Spika, sasa nielezee yatokanayo na mijadala ya hoja. Kamati ilipokea takribani hoja 74 kutoka katika Kamati za Sekta kumi. Kati ya hoja hizo 74, hoja 17 zilihusu maombi ya bakaa ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwenye mafungu ya Wizara na Taasisi mbalimbali kwa mwaka huu unaokwisha wa 2013/2014. Hoja 49 zilihusu maombi ya fedha za nyongeza kwa mwaka wa fedha ujao, yaani mwaka wa 2014/2015 na hoja nane zilihusu masuala ya kisera.

Mheshimiwa Spika, kati ya hoja 49 zilizowasilishwa kwa ajili ya maombi ya fedha za mwaka ujao, hoja saba zilihusu miradi ya maendeleo kwa mwaka wa 2014/2015 na hoja 42 zilihusu malipo ya madeni, posho za chakula na kadhalika. Kamati imechambua kwa kina hoja zilizohusu ongezeko la fedha na kuazimia kupendekeza nyongeza ya fedha katika mafungu 13, kati ya mafungu 23 yaliyoombewa fedha za nyongeza.

Aidha, kulikuwa na hoja za mafungu mawili ambayo yaliongezewa fedha baada ya mashauriano ndani ya Serikali na mafungu husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano ya Kamati na Wizara ya fedha pamoja na michango ya Waheshimiwa Wabunge wakati wa mijadala ya bajeti ya sekta mbalimbali, Serikali iliahidi na kutoa bakaa ya fedha za bajeti kwa mwaka unaomalizika kwa mafungu kadhaa kwa kadri hali fedha itakavyoruhusu hadi kwisha kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maombi ya fedha kwa ajili ya mwaka wa fedha ujao na kufuatia mashauriano na Serikali kwa kuzingatia hali halisi ya kifedha, Wizara ya fedha imekubali kuyaongezea mafungu 15 jumla ya Shilingi bilioni 165.82. Kati ya kiasi hiki, Shilingi bilioni 130.95 zimeelekezwa kwenye matumizi muhimu ya kawaida yaliyokosa fedha na Shilingi bilioni 34.9 zimeelekezwa kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa mafungu na namna yalivyoongezewa fedha ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Jeshi la Zimamoto na uokoaji, yaani Fungu Na. 14 limeongezewa Shilingi milioni 898.8 kwa ajili ya posho ya chakula, yaani *ration allowance* ambayo Kamati imeridhia iongezwe kutoka Sh. 5,000/= kwa siku hadi Sh. 6,000/=.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Fungu Na. 16 limeongezewa Shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kugharamia mahitaji mbalimbali ya uendeshaji wa Ofisi hiyo. Aidha,

kwa kutambua umuhimu wa uendelezaji wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Ofisi hiyo, Kamati imeridhia kiasi cha Shilingi bilioni tano ziongezwe ili kufanikisha azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi - Fungu Na. 28 limeongezewa Shilingi bilioni 16.3 kwa ajili ya posho ya chakula ambayo imeongezeka kutoka Sh. 5,000/= hadi Sh. 6,000/= kwa siku na Shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ununuzi wa sare. Hivyo, Jeshi la Polisi jumla limeongezewa Shingi bilioni 18.8.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza - Fungu 29, limeongezewa Shilingi bilioni tano kwa ajili ya posho ya chakula ambayo pia imeongezeka kutoka Sh. 5,000/= hadi Sh. 6,000/= kwa siku.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kupambana na Kuzia Rushwa - Fungu 30 imeongezewa Shilingi milioni 868.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika huko Arusha na Shilingi bilioni moja kwa ajili ya mafunzo ya vijana 392 walioajiriwa.

Mheshimiwa Spika, Fungu 38 - Ngome imeongezewa jumla ya Shilingi bilioni 36.2 ambapo kati ya hizo Shilingi bilioni 23.2 ni kwa ajili ya kugharamia posho za chakula na Shilingi bilioni 10 ni kwa ajili ya kununulia mafuta ya kuendeshea zana na Shilingi bilioni tatu ni kwa ajili ya mafunzo na mazoezi ya zana mpya za kivita.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhia posho ya chakula kwa fungu hili iongezeke kutoka Sh. 7,500/= hadi Sh. 8,500/= kwa siku kutokana na hali halisi ya maisha ya Askari hasa ikizingatiwa kuwa posho hii haikuwahi kupanda kwa muda mrefu, licha ya maombi hayo kuwasilishiwa Serikalini mara kadhaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyongeza ya mahitaji ya mafuta, mafunzo na mazoezi ya zana mpya za kivita, Kamati ilizingatia umuhimu wa utunzaji wa zana hizo mpya ili kuepuka madhara yatokanayo na kutokutunzwa kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa - Fungu 39 limeongezewa Shilingi bilioni nane kwa ajili ya kugharamia posho ya chakula. Kamati imeridhia ongezeko la posho hiyo kutoka Sh. 7,500 hadi Sh. 8,500/= kwa siku kutokana na hali halisi ya maisha ya Askari.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria fungu 41 imeongezewa Shilingi milioni 600 kwa ajili ya malipo ya ruzuku kwa wanafunzi 600 wa Sheria wanaofanya mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika - Fungu 43 imeongezewa jumla ya Shilingi bilioni 23.25 kwa mchanganuo ufuatao:-

(a) Shilingi bilioni nne kwa ajili ya kulipia sehemu ya deni la madawa ya pamba yaliyoahidiwa na Serikali kwenye bajeti inayoisha, lakini haikutolewa kabisa. Ahadi ya Serikali ilikuwa Shilingi bilioni 6.3.

(b) Shilingi bilioni tatu ni kwa ajili ya kulipia ruzuku ya mbegu za pamba za *quton* ambazo zilikuwa ziuzwe kwa wakulima kwa bei ya Sh.1,200/= kwa kilo, lakini Serikali ikatoa ruzuku ya Sh. 600/= kwa kilo. Jumla ya ruzuku ilikuwa Shilingi bilioni 4.8, lakini kutokana na ukweli kwamba mbegu zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.8 hazikuota, sasa zitalipwa Shilingi bilioni tatu.

(c) Shilingi bilioni 3.25 ni kwa ajili ya kuchangia fidia ya fedha ambazo zingelipwa kwa Halmashauri za Wilaya na wanunuzi wa Pamba kama Cess ambayo ni sawasawa na 2%, na 3% itatolewa kwenye mafungu ya Wizara ya Kilimo na Chakula kama alivyoeleza mapema leo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Lengo la hatua hii ilikuwa ni kupandisha bei ya kuanzia ya mkulima wa pamba katika msimu huu hadi kufikia Sh. 750/= kwa kilo. Vinginevyo, bei ingekuwa chini ya bei ya soko ya mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii - Fungu 52 imeongezewa jumla ya Shilingi bilioni 33.5. Kati ya hizi, Kamati imeona umuhimu wa kuongeza fedha kiasi cha Shilingi bilioni tatu kwa fungu hili katika eneo la uimarishaji wa afya ya mama na mtoto, kutokana na kutambua umuhimu wa usimamizi wa afya inayomhusu mama na mtoto.

Vilevile Kamati imetambua umuhimu wa usambazaji wa dawa katika hospitali zetu unaofanywa na Wizara ya Afya kupitia TAMISEMI. Hivyo Kamati imeridhia kiasi cha Shilingi bilioni 25 ziongezwe kwa ajili hiyo. Aidha, Shilingi bilioni 5.5 zimeongezwa kwa ajili ya kuanza kulipia sehemu ya deni la *MSD*.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uchukuzi - Fungu 64, Kamati imeridhia iongezewe Shilingi bilioni 14 kwa ajili ya kuwezesha kununua vichwa saba vya treni ambapo mahitaji ya Wizara hii ni vichwa 60. Katika bajeti mbili zilizopita, yaani 2012/2013 na 2013/2014 vimenunuliwa vichwa 21. Hivyo, nyongeza hii ya vichwa saba itawezesha kufikia angalau nusu ya idadi ya mahitaji halisi na hivyo kuongeza ufanisi wa Shirika la Reli Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji - Fungu 93 imeongezewa Shilingi bilioni 838.8 kwa ajili ya posho ya chakula kutoka Sh. 5,000/= hadi Sh. 6,000/= hasa kwa kuzingatia posho hiyo nayo haikuwahi kuongezwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo - Fungu 96 Kamati imeridhia Mfuko wa Vijana uongezwe Shilingi bilioni mbili kuwawezesha vijana kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, maombi yote haya ya fedha ni ya ziada. Kutokana na umuhimu wake kama yalivyowasilishwa na Kamati ya Kisekta, Kamati imelazimika kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kuona namna ya kupata fedha hizi.

Itakumbukwa kwamba wakati kupitisha maombi ya fedha ya nyongeza katika mwaka wa fedha unaomalizika mwezi huu, Kamati kwa kushirikiana na Serikali, walikubaliana kuongeza kiasi cha Shilingi bilioni 513 nje ya Bajeti iliyowasilishwa. Hivyo ilibidi ukomo, yaani *sealing* ya Bajeti ya Serikali ibadilishwe ili kukidhi mahitaji hayo ya ziada.

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanywa na Kamati kufuatia nyongeza ya fedha iliyofanywa mwaka wa fedha unaoisha, imeonyesha kuwa utekelezaji wake haukuwa wa kuridhisha kutokana na ukweli kwamba mafungu yote yaliyoongezewa fedha chini ya utaratibu huo, hayakupata fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

Kwa msingi huo, kwa mwaka wa fedha ujao, Kamati ikaona busara kuja na utaratibu mwingine ambapo kwa kushauriana na Wizara ya Fedha iliamua kupitia upya viwango vya bajeti vilivyoidhinishwa kwa kila fungu na kuazimia kupunguza kaisi cha 5% kutoka katika matumizi ya kawaida katika mafungu mbalimbali. Pia, kupunguza bajeti ya ununuzi wa magari ya Serikali kwa asilimia 50. *(Makofi)*

Hatua hii kwa pamoja imewezesha kupatikana kiasi cha Shilingi bilioni 165.819. Pamoja na kwamba mahitaji halisi yaliyopendekezwa na Kamati ya Bajeti ya awali yalikuwa Shilingi bilioni 225, kwa kutambua hali halisi ya kifedha, Kamati imelazimika kuridhia kiasi hicho cha Shilingi bilioni 165.819 zilizopatikana kutokana na makato hayo ili ziongezwe kwenye mafungu yaliyowasilisha maombi ya fedha za nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha hizi zitakatwa kutoka mafungu mbalimbali, Wizara ya Fedha itatoa mwongozo wa namna fedha hizo zitakavyokatwa kwa kutambua kwamba hatua hii itakuwa na athari tofauti kwa mafungu mbalimbali. Aidha, utaratibu wa kukata hautahusisha maeneo yanayolindwa, yaani *protected items*. Naomba kurudia. Aidha, utaratibu wa kukatwa utakaofanywa na Wizara ya Fedha hautazingatia maeneo yanayolindwa, yaani *protected items*.

Mheshimiwa Spika, mafungu mengine yaliyoombewa fedha za nyongeza na Kamati za Kisekta hayakuweza kuongezewa fedha kutokana na upungufu wa fedha. Kamati inaishauri Serikali iendeleze juhudi katika ukusanyaji wa mapato ili fedha hizo zipatikane na zikishapatikana ziwasilishwe Bungeni kwa Mfumo wa Bajeti ya nyongeza, yaani *supplementary budget*.

Mheshimiwa Spika, yaliyojitokeza wakati wa Uchambuzi; kama nilivyotangulia kusema awali, uchambuzi huu unafanyika kwa mara ya pili toka kuanzishwa kwa Kamati ya Bajeti. Uchambuzi huu wa Kamati umeonyesha kuanza kuzoeleka baada ya Kamati kuja na utaratibu mpya wa kushughulikia maombi haya bila kuathiri sura ya bajeti inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, tofauti na ilivyojitokeza mwaka 2013 wakati tunaanza utaratibu huu, ambapo Kamati za Kisekta ziliwasilisha hoja kama vile kuomba watumishi na kadhalika, safari hii Kamati hizo zilizingatia ushauri uliotolewa na Kamati ya bajeti na kuwasilisha hoja mahususi zenye maslahi ya Taifa. Naomba nitumie fursa hii kuzipongeza Kamati zote za Kisekta zilizowasilisha hoja zao kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa na Kamati ya Bajeti kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wakati wa kutekeleza jukumu hili, Kamati imekutana na changamoto mbalimbali. Kitu kipya wakati wote kina changamoto zake. Kamati imebaini changamoto mbalimbali ikiwemo ya mafungu mengi kutokutengewa fedha za kutosha katika miradi ya maendeleo, na kile kidogo kilichotengwa kutotolewa. Hivyo, kusababisha miradi mingi ya maendeleo kutotekelezwa kikamilifu au kutokamilika kwa wakati.

Utaratibu uliotumika wa kupitisha hoja mahususi kupitia Kamati hii ya Bajeti umewezesha kubaini hali hiyo. Hivyo, Kamati inaamini kwamba katika mwaka ujao wa fedha utaratibu huo mpya utaendelea kuboreshwa na maeneo yanayoonekana kuwa na upungufu yataboreshwa na kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo ya kipaumbele, Kamati inatambua umuhimu wa kugharamia maeneo hayo hususan kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile maji, umeme, kilimo, viwanda, uvuvi na mifugo na kadhalika. Ingawa maeno hayo yalipewa msisitizo katika bajeti ya mwaka unaomalizika na yaliongezewa fedha, fedha hiyo haikutoka yote.

Kwa maeneo hayo, safari hii Kamati inasisitiza umuhimu wa kuhakikisha kuwa fedha katika maeneo hayo zinatolewa kama ilivyokusudia kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha ujao, Kamati ilipokea hoja nyingi kwa ajili ya manunuzi ya kawaida kuliko miradi ya maendeleo. Hii imetokana na mahitaji mahususi katika katika matumizi hayo ya kawaida.

Kamati inendelea kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa kubainisha vyanzo vipya vya mapato ili kuweza kukusanya mapato mengi yatakayogawiwa kwa maeneo mbalimbali ya kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Napenda nimshukuru sana Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum na Manaibu wake; Mheshimiwa Adam Kigoma Malima na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Kamati.

Nawashukuru kwa dhati wataalam wote kutoka Hazina na Tume ya Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Kamati za kisekta hadi kukamilika kwa bango kitita. Naomba niwatambue wataalam hao wakiongozwa na Kamishna wa Bajeti, Ndugu John Mihayo Cheyo, Ndugu Emmanuel Tutuba, Ndugu Ezekiel Mpanda, Ndugu Edwin Makamba, Ndugu Robert Masatu, Ndugu Lilian Wawa na Nancy Kitajo.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua hoja hizo na kuweza kufanya maamuzi magumu, hususan kwa aina, utaratibu uliotumika kupata fursa kwa ajili ya mafungu mengine.

Wajumbe wa Kamati ni kama wailioorodheshwa kwenye taarifa hii. Naomba nisiwataje, lakini nimtambue Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Andrew Chenge na Wajumbe wengine ni kama walivyoorodheshwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upya wa Kamati hii, majukumu mazito iliyonayo pamoja na changamoto zilizopo, Wajumbe hawa wamefanya kazi kwa uvumilivu, kwa umakini na umahiri mkubwa kuhakikisha kwamba wanatekeleza majukumu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, wale wanaosema kwamba Kamati hii haikufanya kazi, napenda nikuhakikishie kwamba Kamati hii ina watu mahiri, watu ambao wana uzoefu mkubwa na wanajitolea na ni wazalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda Bunge lako Tukufu liiamini Kamati hii na iendelee kuitumia; watu wanajituma, wanafanya kazi masaa mengi sana bila kuchoka na bila kudai malipo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati inayoongozwa na Ndugu Elisa Mbise na Makatibu wa Kamati, Ndugu Lina Kitosi, Ndugu Michael Chikokoto na Ndg. Michael Kadebe kwa kuihudumia vyema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Huu ndiyo mrejesho ambao ulitakiwa kwa sababu safari hii, tofauti na mwaka wa jana, muda ulikuwa kidogo umebana sana. Siyo hivyo tu, kutokana na utekelezaji wa bajeti iliyopita, mpaka watu wanakutana kwa bajeti tunayoendelea nayo haukuwa mzuri. Pia nayo ikawa ni hoja nyingine nzito. Kwa hiyo, hapa tulipofikia nadhani tumekwenda vizuri.

Sasa namwita Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Nchemba, dakika 15.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. NCHEMBA): Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe neno la faraja kwa familia yangu, mke wangu na watoto wetu watatu kwamba *very s*...

SPIKA: Mheshimiwa, wala hawapo, ulishatoa zamani. Naomba uendelee sasa.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. NCHEMBA): Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia mambo mengi, nitumie fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Fedha kuweza kupitia na kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja na nyingine atasema Mheshimiwa Waziri na nyingine tutajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, mimi nashughulikia sera, na kwa kiwango kikubwa mijadala mingi ililenga zaidi kwenye upande wa misamaha ya kodi na ililenga zaidi kwenye upande wa namna tutakavyoweza kukusanya mapato mengi zaidi ili kuweza kupeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tangu niungane na Bunge hili, hakuna mwaka ambapo Waheshimiwa Wabunge hawakuongelea suala la kupunguza misamaha ya kodi; na hakuna mwaka Mkaguzi wa Hesabu za Serikali hajawahi kuongelea ajenda ya kupunguza misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, nami nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, ni miezi sita tu tangu niondoke kwenye Kamati ya Bajeti. Mara zote tulikuwa tukilia na tukiona kwamba Serikali haijawa na nia njema, ama ya dhati ya kuleta Muswada wa kufuta misamaha ya kodi. Sasa uungwana ni vitendo.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu pamoja na Wabunge kuonesha kwa dhati kwamba wanataka sana kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija, tumeshaleta Muswada huo na ulishasomwa kwa mara ya kwanza.

Sisi kama Serikali, na kama Wizara ya Fedha, nia yetu iko pale pale. Kwa hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge tutakaposoma Muswada huo kwa mara ya pili na tutakapojadili tuweze kulimaliza tatizo hilo ambalo limekuwa ni kilio cha muda mrefu cha Wabunge na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili naomba lisichanganywe. Lisichanganywe na ajenda ya uwekezaji, ikaonekana labda kufuta misamaha ni kukimbiza wawekezaji. Ni vyema tukaelewa vyema, mara zote Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Waheshimiwa Wabunge, Kambi Rasmi ya Upinzani, pamoja na Kamati ya Bajeti, tumekuwa tukisema tufute misamaha isiyo na tija. Nasi tunalenga kwenye misamaha isiyo ba tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, athari za kutokufuta misamaha ya kodi ni nyingi sana. Moja, kama Waheshimiwa Wabunge ambavyo wamesema, tunaposamehe kiwango kikubwa cha fedha, zaidi ya Shilingi trilioni 1.56, maana yake ni kwamba mzigo ule unabebwa na wanyonge, unabebwa na walalahoi unabebwa na wafanyakazi. Lakini ndicho kinachosababisha pia fedha zisiende kwenye miradi ya maendeleo. Kwa hiyo leo hii tuoneshe nia ya dhati na dhamira zetu za ukweli tushughulikie tatizo hili ili liweze kwisha.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa nia yetu siyo kukimbiza wawekezaji, yule mwenye dukuduku na kipengele chochote anachodhani kitakimbiza wawekezaji, aje akisemee hapa, kwa maana ndiyo kazi tuliyotumwa na Watanzania. Lakini kwa yale ambayo uwepo wake hauathiri shughuli za uzalishaji ni vyema fedha hizo zikaenda kutoa huduma za maendeleo katika shughuli nyingine.

Jambo hili lilisemwa kwa nguvu sana na Mheshimiwa Keissy, Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mheshimiwa Kangi, na tumeshalileta.

Namwomba Ndugu yangu Mheshimiwa Deo, Ndugu yangu Mheshimiwa Kangi na Mheshimiwa Keissy, Mheshimiwa Deo hujawahi kuunga mkono bajeti yoyote tangu tuje hapa, naomba uweke historia kwa sababu jambo hili tumeshalipatia suluhisho la kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba leo hii sheria hizi za misamaha tusipozifuta, kuna mikataba na kuna mikataba ya Kimataifa ambayo inasema ukishaingia mkataba na mwekezaji kwamba atapata faida hiyo kisheria, maana yake atafaidi misamaha hiyo kwa miaka 25 mingine ijayo, *for policy stability*. Ukisema uache wakati wengine ulishawapa, utaingia kwenye tatizo la *double standard* na mikataba ya Kimataifa.

Kwa hiyo, sisi tumesema kwa ile ambayo haiathiri uchumi kwa kweli tuweze kuifuta ili mikataba itakayoingiwa kuanzia leo na kuendelea iweze kuepuka tatizo la aina hiyo. Hatuendi kufukua makaburi, maana wengine wameanza kusema, sasa mikataba si iliishaingiwa? Sisi hatuendi kufukua makaburi, tunasema kuanzia leo tuache kunung'unika, tuchukue hatua, maadam Watanzania wanataka hilo, Waheshimiwa Wabunge wanataka hilo, basi tuitendee haki nchi yetu ili tuweze kupiga hatua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmesema hayo; Mheshimiwa Ntukamazina, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Mkosamali, Mheshimiwa Mwanjelwa na wengine, tuunge mkono jitihada hizi tuonyeshe dhamira zetu kwamba ni kweli tulikuwa tunataka kuchukua hatua kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunasema nchi yetu inakopesheka, leo hii nchi yetu inapata misaada; hivi kama tutaruhusu uingiaji wa mikataba wa kusamehe kwa miaka 25, nani ana uhakika miaka 25 ijayo Tanzania itakuwa bado inakopesheka? Nani ana uhakika miaka 25 ijayo Tanzania itakuwa bado inapata misaada? Kwa sababu hata miaka 15 ijayo ukitaka kufuta misaada, kama sheria haikuwa imefutwa, utaingia kwenye mgogoro kwamba tayari mlishaingia mikataba. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa kweli tuonyeshe nia ya dhati kwenye hili na tuweze kuchukua hatua inayostahili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge walilliongelea kwa dhati, lilikuwa linahusu manunuzi. Zaidi ya asilimia 75 ya bajeti ya Serikali ni manunuzi. Jambo hili lina matatizo, alilisemea sana Mheshimiwa Conchesta, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Saidi, Mheshimiwa Maryam, Mheshimiwa Shabiby, Mheshimiwa Mwambalaswa, Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Faith Mtambo, Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale na Mheshimiwa Kalogeris.

Ni kweli hata Mtanzania wa kawaida jambo hili analishuhudia. *Cement* dukani inajulikana bei yake, kama ni Sh. 17,000/=, ukienda kununua kwa mchakato ule wa kitaalam, wakati mwingine inakuwa Sh. 30,000/= ama na kuendelea, na vifaa vingine vingi vinanunuliwa hivyo hivyo. Kuna Mheshimiwa Waziri mmoja alikuwa anatoa mfano kwamba siku moja alikuwa anasafiri kwa tiketi ya ndege, daraja lile lile, akaamua siti ya pili amkatie mke wake kwa gharama binafsi. Gharama ya mke wake ilikuwa mara tatu ya ile inayokatwa kwa sheria hizi za manunuzi.

Mheshimiwa Spika, sasa hatua iliyochukuliwa na Serikali, kwanza sheria iliyokuwa inatoa mwanya huo ilikuwa Sheria Na. 21 ya mwaka 2004. Lakini mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge kwamba mwaka 2011 tulibadilisha sheria hiyo, na Sheria Na. 7 imepunguza matatizo haya, lakini lililokuwa linakosekana ilikuwa kanuni. Lakini kanuni tayari ilishatangazwa kwenye gazeti kuwa kuanzia mwaka 2013 mwishoni mpaka sasa imeendelea kutumika.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunalofanya, tunategemea katika mwaka wa fedha ujao tukamilishe kuziba mianya hiyo kwa kuleta Sera ya Manunuzi ili kuweza kuweka utaratibu ambao utawiana na soko la bidhaa hizo ili kuweza kuepuka gharama za bidhaa zile kupandishwa zaidi ya mara mbili hata mara tatu na kupunguzia Serikali mzigo kufuatana na Sheria hiyo ya Manunuzi.

Kwa hiyo, kwenye hili Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tunakuwepo kule zinakofanyikia kazi nyingi za manunuzi, kwenye Halmashauri sisi ni Wajumbe, nawaomba tushiriki. Nami naagiza wale ambao wako chini ya Wizara yetu, tunao Wakaguzi. Pale ambapo wataona bei elekezi, pale ambapo wataona sheria, pale ambapo wataona kanuni, pale ambapo wanaona sera imekiukwa tuweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, hilo sisi kama Wizara tumesema tutapenda tutakapokuja muda mwingine tuwe na mifano ya aina hiyo, na tutafuatilia yale ambayo yanabainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hata lile nililotangulia kulisema, la kwenye misamaha; tumeshalisemea sana; tutakapokuwa tumepitisha hii ya sasa, na hapa nasema kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, litakalotoka ni agizo la Mheshimiwa Waziri. Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali aangalie pia hata ile misamaha ambayo itaonekana ina tija aikague kama kweli ilifanya kazi ile ambayo ilikuwa imekusudiwa kufikiwa ili tuweze kumaliza kabisa tatizo hilo. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo lilijitokeza kwa kiwango kikubwa, na niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tunapokuja Bungeni tusitoe taswira ambazo ni hasi kwa Watanzania. Watanzania wanapata taswira hasi. Jambo moja lilijengwa sana hapa, ni kama vile Serikali haisikilizi mtu. Hili jambo linawachanganya Watanzania, na kwa kweli Serikali inapokea ushauri, inaufanyia kazi na ule ambao unafaa inautekeleza.

Mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Bajeti. Mwaka wa 2013 tulilazimisha sana kodi ya simu, nami nilikuwa Mjumbe, na mpaka leo hii sijawahi kukana; tulitaka kweli kila kadi ikatwe kodi; na Serikali ilichukua. Hata lile la *money transfer,* Serikali ilichukua, hata hili la kupunguza misamaha ya kodi, Kambi Rasmi mmesema tangu mje hapa, Kamati ya Bajeti, *CAG*, na Serikali imechukua ndiyo tumelileta sasa hivi. Sasa tutekeleze ili tusiwachanganye wananchi. *(Makofi)*

Lingine ambalo limesemwa sana ni lile la madeni. Hata Kamati imesema na mwaka huu inaweza ikaonekana kama vile Serikali haisikilizi. Mwaka 2013 nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, tuliilalamikia Serikali kwanza kwa nini inaweka *ceiling* na huku inatuambia tunakopesheka? La tatu, kwa nini tusikope tumalize miradi?

Hata kwenye ripoti yetu ya mwaka wa 2013 ya Kamati tuliandika kama Kamati ya Bajeti. Nanukuu: "Kamati ya Bajeti haioni tatizo kwa Tanzania kuendelea kukopa, kwani deni lake ni hilivu." Ndiyo ulikuwa msimamo wetu, na Serikali katika mwaka huu uliopita 2013/2014 haijakopa kuliko kiwango ilichopitisha kwenye bajeti. Lakini mwaka huu Kamati ya Bajeti imesema deni hili pamoja na Serikali kusema ni himilivu, limekuwa mzigo mkubwa kwa Taifa. *Just one year.* Kwa hiyo, Watanzania wakisikiliza wanaona hawa! Mwaka 2013 tungefuata ule utaratibu, tungepeleka Shilingi trilioni 30.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2013 tuliomba Mheshimiwa Dkt. Limbu hata awe na masaa ya ziada ili atutengenezee nondo za kuibana Serikali iweze kukopa hata tupate Shilingi trilioni 30.

Kwa hiyo, mambo haya wakati mwingine sisi tuyamalize humu kwa humu kwa sababu Watanzania tukiwapa taarifa nyingi sana wanakuwa katika hali ya wasiwasi sana.

Jambo la mwisho, kwa sababu naona kengele imeshagongwa, ni jambo la madeni ya Wazabuni.

Ndugu zangu na Ndugu Watanzania, hili jambo tumeshaliona kama Wizara na tumesema katika robo mwaka ya kwanza tutajitahidi kuhakikisha jambo hili tunakwenda nalo kwa wakati ili tusilimbikize sana, na niombe mabenki wala wasiwafilisi watu wetu kwa sababu wametoa huduma Serikalini, watupe muda katika robo ya kwanza ya mwaka sisi tujitahidi ili kuweza kunusuru maisha ya watu wetu hawa. Jambo hili limesemwa na Mheshimiwa Aeshi, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Maria Hewa na wengine. Nawapongeza wote mliosema hili, lakini sisi tumeshalichukua.

Mheshimiwa Spika, naomba tu nitoe rai, kwa wale wanaohakiki madeni haya, wasiibebeshe Serikali mzigo. Kwa kuwa kila Wizara ina Mhasibu, kila Wizara ina Mkaguzi wa Ndani na hawa wako ndani ya Wizara ya Fedha, mimi nitoe rai kwamba kama kuna madeni yatatoka kwenye Wizara, yakaletwa kwamba yanastahili kulipwa; yakija yakikaguliwa na Wizara mama ya Fedha ikajulikana kulikuwepo na hewa, yule aliyepitisha kwamba Wizara ya Fedha inatakiwa kulipa haya madeni, aanze kutafuta kazi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Wakaguzi walioko kwenye Wizara na wale walioko Wizara ya Fedha, wamesoma Vyuo vile vile na nchi yao ni hii hii. Kwa nini tukague mara mbili wakati walioko kule ni Wakaguzi na walioko huku ni Wakaguzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme hili, na wote wanaohusika, Maafisa Masurufu wazingatie hili. Sasa kama watasema nasema kama nani hapa, nasema kwa niaba ya Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge ambao walileta mahitaji yao na walisema hata wanaogopa kuunga mkono bajeti hii; nao ni Mheshimiwa Badwel, Mheshimiwa Mama Kilango, Mheshimiwa Sara, Mheshimiwa Munde, Mheshimiwa Vicky Kamata, Mheshimiwa Kakoso na Mheshimiwa Kitandula.

Wizara ya Fedha itazingatia mahitaji ya Majimbo yenu. Mheshimiwa Rage kila wakati amekuwa akililia deni la pale kwake, Mheshimiwa Bukwimba, Mheshimiwa Leticia Nyerere, pamoja na mambo ya Wakuu wa Wilaya yaliyosemwa na Wakuu wa Wilaya tulionao humu, sisi kama Serikali tutazingatia yale ambayo yamesemwa, yanayogusa baadhi ya Majimbo, na kwa kweli kwa Mheshimiwa Badwel nilifika mwenyewe, jambo hilo tutaongea ili liweze kupatiwa suluhu.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mambo ni mengi, mengine tutayajibu kwa kuwapelekea Wabunge kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu jambo moja ambalo lilileta taswira tofauti, ni kuhusu kwamba Watanzania wanalipa kodi kidogo kuliko Kenya.

Mheshimiwa Spika, Watanzania kwa mujibu wa Sensa wako milioni 45. Walio chini ya miaka 15 ni asilimia 44, kwa hiyo, ni sawa na watu milioni 20.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Saa imefika! Mheshimiwa Kighoma Malima!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. NCHEMBA): Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa pili, Mheshimiwa Kighoma Malima, dakika 15.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM KIGHOMA MALIMA): *Bismilah Rahman Rahim!*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake zote na kwa afya inayoniwezesha kusimama hapa mbele yenu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze pia kwa kukushukuru wewe na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzetu wote ambao tumefanya nao kazi kwa muda wa siku hizi 10 zilizopita katika kuboresha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, naomba uniruhusu niishukuru sana Kamati ya Bajeti. Sana, sana, sana! Katika uwepo wetu mle ndani, tofauti kabisa na wengine wanavyopenda kusema na nini, lakini kazi iliyofanyika mle ni kubwa sana, sana, sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika yote hayo, naomba nikupongeze wewe kwa kuthubutu kwamba tuwe na utaratibu huu ambao unawezesha Bunge kuwa na mchango mkubwa zaidi kwenye bajeti ya Serikali kuliko ilivyokuwa inakuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa kuchukua ushauri wa CCM wa kuunganisha Vyama hivi katika Serikali kwa sababu Mheshimiwa…*(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wa…

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, anayeongoza kikao ni mimi.

Waheshimiwa Wabunge, na ninyi mna midomo tu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. A. MALIMA): Mheshimiwa Spika, muda wangu.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, endelea.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K.A. MALIMA): Mheshimiwa Spika, ninaomba niipongeze ...

(Hapa Wabunge fulani walishangilia kwa kupiga makofi na vigelegele)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tuendelee muda hautoshi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K.A. MALIMA: Mheshimiwa Spika, ninaomba niipongeze sana michango ya Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani, hasa wawakilishi wa Mipango na Wawakilishi wa Fedha, kwa sababu tumeifanyia kazi na tumeichukua na ilikuwa ni michango *constructive criticism* tunaenda kuifanyia kazi. Hii bado ninaamini kwamba, inatokana na hali hii mpya ya Serikali ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, kila nyakati ya historia ina mambo yake na mazingira mahususi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, inayotengeneza mikakati maalum ya kufikia malengo ya maendeleo yake kama inavyojipangia. Sisi Tanzania hatuna tofauti.

Mheshimiwa Spika, ninalisema hili, kwa sababu kwenye kuitafakari na kuichambua Bajeti kwa muda wa siku kumi, tumeizungumzia kwa namna nyingi sana. Bajeti yoyote ya umma ina mambo makuu manne. Inaweza ikawa Bajeti ya Taasisi, lakini Bajeti ya Umma ya Serikali ina mambo makuu manne. Inakuwa na misingi ya kisiasa *(Political Objectives)*. Inakuwa na misingi ya kiuchumi, kuwianisha rasilimali na uwezo *(Allocation of Resources)*. Inakuwa na misingi ya kiuhasibu, kuhakikisha zile *balance* zake zinakwenda sawasawa. Mwisho, inakuwa na misingi ya kiusimamizi *(Public Management of Budgeting)*. Hiyo ndiyo misingi na ni somo hasa kubwa ambalo wenzetu wanalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, misingi ya kwanza ya *budgeting* historia yake inatokana na Marekani huko miaka 80 iliyopita, tangu wakati wa akina Mr. Paul Samuelson na wenzake.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, kuna hoja ambazo zimetoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, inawezekana sisi kama Taifa, inabidi tuangalie kama mfumo wetu wa kibajeti au utaratibu wetu wa bajeti unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaamini kwamba, Bajeti yetu inakwenda vizuri. Utaratibu wetu wa maandalizi ya Bajeti unakwenda vizuri. Vile vigezo tulivyotumia kusema labda Bajeti yetu ina matatizo, *Budget Deficit*. Nilikuwa ninaangalia tu kwenye tathmini, kwenye nchi zilizoendelea kwa miaka mitano au sita iliyopita, karibu asilimia za nchi *Budget Deficit,* imetoka kwenye asilimia 1.2 hadi asilimia 8.0, kwa wastani wa nchi hizi kubwa kubwa zote. Kwa hiyo, ni kigezo ambacho tunatumia kuangalia ufanisi wa Bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kila nchi ina mambo yake yenyewe, ninaomba niitumie nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba, tunapojitazama hili tunaloleta mbele yenu na tunaloenda kulifanyia kazi, kuna mengine ambayo hatujayasema, ambayo lazima tuyaseme, yawe ni makubaliano baina ya sisi Serikali na Bunge kwa upande mmoja na Wananchi wa Tanzania wanaotuangalia huko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya tunayokubaliana yanahitaji utekelezaji huko nje tunakokwenda. Kuna Mwandishi mmoja aliyesema; kila mwaka *Havard School of Economics* wana mkusanyiko wa Wachumi wao wakubwa wanakaa kufanya tathmini, waliandika wakasema hivi: "*It is humble nature of the small things that initially trigger off growth, such as relaxing specific constrains on private activity.*" Kuna vile vitu vidogo vidogo ambavyo vikichukuliwa kwa dhati vinaleta mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wamelia, Serikali imepokea. Jambo la kwanza kabisa ni kwenda kufanya mabadiliko makubwa ndani ya Mfumo wa Matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza kufanya mabadiliko, hatusemi mabadiliko madogo madogo, lakini mabadiliko yake ni nini? Kama alivyosema Mheshimiwa Mwigulu, pale kwenye chupa ya maji, ukiwa unanunua kwa ajili ya kampuni yako, huwezi kununua chupa hii ya maji ya shilingi 3,000. Huwezi kufanya safari ya kutoka Dar es Salaam kwenda Arusha kwa shilingi milioni moja kwa gari. Gari gani hiyo hata ndege hatuitumi mafuta kiasi hicho!

Mheshimiwa Spika, katika udhibiti wa *Public Financing* kuna *Financial Discipline*. Sasa kwa majukumu haya ambayo Mheshimiwa Rais ametupatia, kwa niaba ya Waziri wa Fedha,

ninaomba nitoe ahadi kwenu kwamba, huko tunakokwenda sasa tunataka tutengeneze mfumo ambao ndani ya Sekta ya Umma, kwanza kabisa, tuanze kuona nidhamu katika matumizi ya fedha. Ndiyo tunasema ni hayo Mapinduzi madogo madogo, ambayo msipoyafikia hamwendi. *You will have business as usual. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tumesema hivi; manunuzi ya vitu vidogo kama mbolea na madawa ya kilimo, tusipofika sehemu tukasema kwa sababu Watanzania asilimia 70, uhai wao unatokana na kilimo, tuangalie vile vitu vidogo vinavyofanya kilimo kibadilike, hatutoki. Tutakaa tunapiga blabla tu lakini hatutoki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumesema tunazo taasisi tatu za udhibiti; udhibiti wa mbolea, udhibiti wa mbegu na udhibiti wa madawa. Lazima tuhakikishe kwamba, taasisi zile zinapewa fedha za kuweza kwenda chini kwenda kufanya ukaguzi wa aina yoyote, ili watu wasijitengenezee utajiri kwa kulimbukia kwenye umaskini.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo tumelizungumzia, kwa karibu ni uwekezaji. Tumezungumzia uwekezaji wa Miradi Mikubwa, *Public Sector Investments.* Tumezungumzia suala la miundombinu, reli, barabara, mawasiliano, lakini kubwa kabisa katika mambo mengine tumesema Sekta ya Umeme. Tumekubaliana na Kamati ya Bajeti kwamba, kwa mwaka huu, Serikali ipunguze matumizi yake kwenye nishati ya umeme na tuweze kuangalia utaratibu wa kukaribisha sekta binafsi kama inavyofanyika nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatumia mabilioni ya mahela kwenye mafuta. Hela zile zinaacha kutumika kwenye vitu vingine. Sasa pale ambapo sekta binafsi inaweza kuingia iingie na ndiyo utaratibu wa nchi nyinginezo zote.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezunguzwa, ambalo Serikali tumelipokea ni suala la vyanzo mbadala. Waheshimiwa Wabunge, wamezungumzia sana suala hili. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, amezungumzia suala la *Deep Sea Fishing* na wengine wamezungumzia suala la kilimo.

Mheshimiwa Spika, ikiwa tunakubaliana kwamba, asilimia 70 ya Watanzania maisha yao yako kwenye kilimo, ni lazima tukitazame kilimo katika sura totauti. Moja, kwanza kabisa tuseme hivi; kwenye kukitathmini kilimo kitakwimu, kilimo kina mambo manne. Kila unapoona wanasema kilimo kinakua kwa asilimia nne, kina mambo manne; ina kilimo, ina mifugo, ina uvuvi, ina misitu. *That is the international statistics domination* ya kilimo. Tunachosema, ni kwamba mle ndani kila mtu ana mabadiliko madogo madogo, kwa mfano uvuvi; ukisema kwenye uvuvi tutumbukize suala la *aqua culture,* suala la kupanda mbegu za samaki, Thailand, Indonesia, Malaysia, huko kote hata hawazungumzii kwa sababu samaki wanapandwa, unakuwa na shamba lako samaki.

We can do it in Lake Victoria. Mheshimiwa Dkt. Kamani amesema. Amekuja hapa ameomba pesa za *aqua culture* na Serikali tumetoa. Kwamba, twende huko tukaangalie ili tujenge huu utamaduni wa kubadilika. Hatuwezi tukawa tumesimama miaka yote kama tulivyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Vita Kawawa na Mheshimiwa Saidi Nkumba ni kuhusu malipo ya Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, hili limezungumzwa asubuhi na sisi Serikali tunaliona. Kila tunapotoa fedha ziende kwa ajili ya wakulima na wajanja wengine wakizitumia pale katikati zinakuwa hazifikii lengo. Matokeo yake ni nini? Tunakubaliana mambo matatu. Kwa ruhusa ya Waziri wa Fedha, ninaomba niseme yafuatayo:-

Moja, kuanzia sasa *Capital Expenditure* yoyote, matumizi ya fedha za umma kwa ajili ya Miradi, lazima iwe na tathmini ya *value for money*. Lazima iwe na tathmini ya kusema sasa Mradi huu pesa zinaingia kweli. Matokeo yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, kuna Miradi mingine ina miaka mitatu, kila ukienda unakuta pesa ni hizo hizo, milioni 60 mwaka huu, milioni 60 mwaka kesho, milioni 60 mwaka kesho kutwa. Ukienda kuuangalia ule Mradi una mabadiliko gani hakuna.

Mheshimiwa Spika, sasa mle ndani kuna vichaka vinajificha.

Kitu kingine ambacho tumekubaliana na Waziri wa Fedha ameridhia tuliseme ni kwamba, tutakipa nguvu zaidi kitu kinachoitwa *Economic Inteligency Unit*. Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, alilizungumzia kwenye mchango wake. Kubwa zaidi, kuna Kitengo kinachoitwa *Financial Expenditure Trucking Unit,* kimezubaa zubaa mle kama miaka mitatu chini ya Kamishna wa Bajeti. Tumekubaliana kwamba, Kitengo hiki ni lazima kipewe nguvu na kipewe meno. Ikibidi tutarudi humu ndani ya Bunge, kuipa nguvu na meno, ili watu watakaokuwa wanafanya kazi kwenye Kitengo cha *Financial Expenditure Trucking Unit,* wawe wana uwezo wa kwenda kuingia sehemu yoyote kwa wakati wowote, kuangalia matumizi ya Serikali. Tukifikia hatua hiyo, watu wakaingia woga na pesa za Serikali tutakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni badiliko makubwa. Kwa kiasi fulani ni lazima mabadiliko haya yaanzie sehemu. Tumeyaona kwenye matumizi ya mbolea, miaka na miaka. Mbolea watu walikuwa wanaitia *cement,* chumvi na kadhalika, lakini Bunge hili liliridhia kuwa na *Tanzania Fertilizer Regulatory Authority*. Tulikuwa na suala la *EWURA* na kuchanganya mafuta. Bunge liliporidhia kuwa na *EWURA,* mambo yanakwenda yakibadilika badilika. Kwa hiyo, ninaamini kabisa katika uthubutu huu tutafikia sehemu ambayo tunaweza tukajenga usimamizi wa uchumi mkubwa na wenye ufanisi zaidi katika Tanzania.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la nafasi ya Taasisi za Fedha katika maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu. Taasisi za Fedha hazishiriki kwenye kilimo, hazishiriki kwenye biashara za kati kwa maana ya *Small and Medium Enterprises.*

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana kimsingi, …

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaposikiliza ninaomba tunyamaze.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. A. MALIMA): Mheshimiwa Spika, tumekubalina kwamba, kupitia Benki Kuu, tunakwenda kufanya tathmini ya ni kiasi gani Taasisi za Fedha zinaweza zikaingia kwenye kuchangia Uchumi wa Tanzania, badala ya kutegemea tu kwamba, zitafanya biashara ya *Treasury Security* na *Treasury Bills* na kadhalika na kadhaiika.

Taasisi ya Fedha ikitaka kupata ushirikiano wa karibu na Serikali na Nigeria wamefanya, ili kuzihamasisha Taasisi za Fedha kushiriki, zile Taasisi za Fedha ambazo zinaonekana zina mchango mkubwa zaidi kwenye *Small and Medium Enteprises,* zina mchango mkubwa kwenye kilimo, zina mchango mkubwa kwa wachimbji wadogo wadogo, zimepewa unafuu fulani wa kodi na kadhalika na kadhalika ili ziweze kupanua shughuli zao kuwafikia Wakulima na Watanzania wenye kipato cha chini

Mheshimiwa Spika, tumesema na sisi tutakwenda kuangalia mifano hiyo ili kujenga hali ya uwezeshaji; lakni siyo uwezesheshaji tegememezi. Kuna ile *Dependency Empowerment,*

ambayo mtu anakuja anapata pesa halafu akiondoka hapana. Vikundi vinavyofikia vigezo vinavyoweza kukopesheka, vipate pesa hizo kwa sababu Taasisi za Fedha zinazo hizo fedha, zisiridhike kufanya biashara na Serikali tu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie suala la uwekezaji wa Serikali. Jambo moja ambalo nilitaka kulisema ni kwamba, tumefanya maamuzi ya makusudi, kila mwaka kuna matumizi ambayo yanayojirudia, ambayo yanawea kuepukika. Moja ya matumizi hayo ni majengo yetu ya fedha ya Ubalozi nje ya nchi. Kuna maeneo mengi ambayo huko nje Tanzania ina viwanja. Tumekubaliana badala ya kila mwaka kutumia pesa kwenye kodi ya viwanja, wenzetu hawafanyi hivyo. Mnapoingia kwenye makubaliano na nchi ile mnayoifikia, mnapewa kiwanja. Tuna viwanja Nigeria, tuna kiwanja Misri, tuna kiwanja Saudi Arabia, tuna kiwanja India, tuna kiwanaja Adis Ababa. Tumekubaliana sasa kwamba, badala ya kila mwaka kutumia shilingi bilioni 14 mpaka 15 kwa ajili ya kulipa kodi ya nyumba, tuanze kujenga zile nyumba kama wanavyofanya wenzetu. Baada ya muda wa miaka mitano, sita, hatutakuwa na hoja hii tena.

Balozi anapopanga nje na Ofisi yake inapopanga nje, huwezi kusema hutomtumia hela. Usipomtumia hela watamtosa nje. Sasa tufike sehemu tuseme sawa ni gharama, *is a capital expenditure* kubwa, lakini Serikali tumefikiria, tumeshauriana na Kamati ya Bajeti, tumeridhiana kwamba, katika hili tuangalie namna ya kuwashirikisha Taasisi ambazo zina fedha kama Taasisi za Hifadhi za Jamii na kadhalika. Kwa sababu hata hivyo, kutumia shilingi bilioni 13 mpaka 14 kila mwaka kwa ajili ya pango, badala yake tukatumia kuwalipa ambao wamejenga majengo nje, inaweza kutupatia unafuu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ninaomba niseme kwamba, haya mabadiliko ya kiusimamizi, *Economic Management* na *Financial Management* tunayoyazungumzia, yanataka kuthubutu. Usipokuwa na uthubutu, tutabakia kila mwaka tunalalamika tunarudi nyuma. Hili tunalolizungumza ni lazima liwe na ubia wa pamoja baina ya Bunge na Serikali, ili tuweze kuwafikishia Watanzania kile ambacho ni matarajio yao. Hakina itikadi, kina suala la kwamba, lazima tufike sehemu ambayo hizi hatua tunazochukua ili zitekelezeke, lazima twende huko tukawe wakali zaidi na ikibidi turudi humu Bungeni tuweke adhabu kali, kwa ajili ya wale ambao kwa makusudi kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuna watu hawasikii tu, wana uharibifu wa moja kwa moja. Huwezi ukawa mharibifu unaharibu milioni 400 mpaka 500m halafu unapewa adhabu ya faini ya shilingi milioni mbili! Lazima tufike sehemu tuamue, ama tunataka tuendekezane kwenye haya mambo ya kusema unajua haki za kibinadamu na kadhalika au tufike sehemu tuseme tuingize nidhamu ya lazima, tuwe wakali na ukali hatua zile lazima zianze kuchukuliwa humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona kwenye nchi za wenzetu, wanafanya mambo ya utani, sasa hivi inafika hatua, mtu anabaka mototo anapewa adhabu ya mwaka mmoja. Nchi nyingine mtu akibaka mtoto anauawa au adhabu nyingine kali, unakuta matukio yale ni macheche watu wanaogopa. Sasa na sisi tufike sehemu tuseme kwamba mwizi wa fedha za umma, mwizi wa fedha za Wakulima, mwizi wa Fedha za Ushirika, adhabu yake iwe kubwa. Ukimpa adhabu ya shilingi 500,000 wakati yeye kaiba shilingi 500,000,000 haisikii. Hayo ni maamuzi ambayo Serikali itakuja Bungeni tuamue wote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu Sheria ya Bajeti …

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, muda wako umekwisha.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. A. MALIMA): Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata muda huu, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwanza, kwa kutujalia sisi wote kuwa na afya njema. Leo tumejaa kwa wingi sana katika Bunge hili. Vilevile, ninatoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi Mheshimiwa Spika, pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti, ambao kwa muda wote huu mmeliongoza Bunge hili kwa imani toka tumewasilisha mapaendekezo haya ya Mapato pamoja na Matumizi ya Serikali ya Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninachukua fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), kwa kutoa maelezo ya ufafanuzi wa kina kuhusu hoja mbalimbali ambazo zinahusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2013/2014 pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2014/2015. Kwa namna ya kipekee, ninaomba niishukuru Kamati ya Bajeti, ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Ninawashukuru vilevile Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Adam Malima na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, kwa kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitakuwa muungwana kama sijachukua fursa hii kumshukuru vilevile Waziri Kivuli wa Fedha, Mheshimiwa James Mbatia, kwa Hotuba yake aliyoiwasilisha hapa. *(Makofi)*

Kipekee, nawashukuru Wataalamu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa mara ya kwanza Hazina katika eneo hili la vyanzo vya mapato, tumefanya kazi bega kwa bega na Wataalamu wetu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuja na mapendekezo haya. Tutaendea kuwashirikisha wakati tunatafuta *proposal* za vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, Watalaamu wa Hazina tumekuwa hatulali ama tunalala usiku mwingi sana toka tumefika Dodoma; nawashukuruni, tusivunjike moyo, tuendelee na kazi. Pale tutakapopata changamoto sisi tuendelee na kazi. Leo tunahitimisha Bajeti ya Serikali, tutalala saa zilizobakia lakini kesho tutaamka tutasimama kama tulivyokuwa tunasimama tuendelee na kazi. Tupo pamoja kwenye hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili mapendekezo tuliyokuwa tumeyatoa, Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza ni 188 na kwa njia ya maandishi tumepata michango ya Wabunge 36.

Kuna maeneo mbalimbali yamesemwa na ninaamini kwamba, kwa sababu hoja zilikuwa nyingi, Waheshimiwa Wabunge, hoja zote zilikuwa ni za msingi na zenye kujenga. Mimi naamini hoja ambayo kila mmoja alikuwa akiitoa alikuwa ana lengo la kujenga, tunajenga nyumba moja. Kitu ninachoamini ni kwamba, kinachotoka mdomoni ndicho kilichopo moyoni. Kwa hiyo, tunatarajia Waheshimiwa Wabunge, wakati tunachukua baadhi ya mapendekezo ambayo mmeyatoa, tunakwenda kuyafanyia kazi, tunaomba tukija hapa tupate *support* yenu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Tumeliona hili, kumeanza kuwa na changamoto fulani hususan Mheshimiwa Naibu Waziri, ameliongelea suala la misamaha ya kodi. Tumeona sasa kwa sababu Serikali imechukua hatua madhubuti, Wabunge mmekuwa mkilisemea hili, mimi toka ninavyofahamu kuangalia na kusikiliza Bunge, misamaha ya kodi imezidi, Serikali ifute misamaha ya kodi. Hii ndiyo ilikuwa *slogan* ya Bunge na ilikuwa *slogan* ya Wabunge. Tumechukua hatua hiyo ya kuleta Miswada ya Sheria, mingine tumeanza kuifuta kwenye *Finance Bill* tayari.

Tunaamini tunachokisema kiko katika mioyo yetu, kwa sababu Serikali ina nia ya dhati ya kutekeleza mapendekezo yenu. Tunaleta mapendekezo ya kufuta baadhi ya misamaha ya kodi, ambayo kwa kina kabisa tumeifanyia kazi, tumejua kwamba hii misamaha ndiyo isiyokuwa na tija na Taifa hili. Tunaomba mtu-*support* kwenye hili. Tunaomba sana Waheshimiwa Wabunge, hili tumekuwa tukilifanyia kazi Serikalini, muda wake wa kuanza kulitekeleza ni sasa, tunaomba *support* yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna eneo ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza na mimi kama Waziri wa Fedha, mwanzo nilikuwa Naibu, nimeshiriki sana kwamba, Serikali sasa imekosa ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato na hatutaki kusikiliza vyanzo vipya ambavyo tayari vipo kwenye *Five Year Plan.* Mheshimiwa Spika umeunda Kamati maarufu tunaiita Kamati ya *Chenge One* na vilevile *Big Results Now*.

Inasikitisha, kama *Five Year Development Plan* Serikali ndiyo ambayo ime-*develop*, inasikitisha kuona *initiative* ya Serikali ya *Big Results Now* tunaendelea nayo na matunda yameonekana. Inasikitisha leo tumefanya kazi na Kamati bega kwa bega, inatugeukia leo eti hatutaki kusikiliza vyanzo vipya vya mapato!

Let us be fair na maeneo maalum ambayo nataka kuyaonesha, mwenzangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ameonesha lakini kwa uchache wa muda hajaifanya hiyo kazi.

Ni jambo ambalo sisi kama Serikali limetusikitisha lakini hatujavunjia moyo, tutaendelea kufanya kazi na Kamati ya Bajeti na *proposals* zao wanazozitoa pamoja na zenu Waheshimiwa Wabunge, tutakwenda kuzifanyia kazi; na tukizileta hapa tuone kwamba, hivi ndivyo vyanzo ambavyo vinatekelezeka. Maana kinachotolewa hapa, Wabunge kweli tunaweza tukafikiria eneo hili kesho tutapata mapato, sawa, si vibaya lakini tunaomba nafasi sisi kama Serikali, twende tukafanye kazi ili tunapotekeleza sasa tuwe tunatekeleza tunakwenda *smoothly* ili kuona vyanzo vya mapato.

Kuna maeneo mawili au matatu naomba nitoe angalizo, ambayo tumeanza kuyafanyia kazi na yalileta *block on the way,* kwa sababu wakati *proposals* zilipokuwa zinaletwa, tulichukua na hatujafanya *analysis* ya kutosha. Hatukufanya *analysis* ya kutosha na matokeo yake sasa tumepata tabu katika maeneo haya na ni maeneo ambayo kiukweli tumekosa mapato.

Eneo la *simcard* mwenzangu alilielezea, kweli ukiangalia eneo hili tungeweza wengi tukasema kwamba, kila mtu atozwe shilingi 500 au 1,000. Tumelifanya hilo, sina haja ya kuelezea *results* ya eneo hilo, kwa sababu tulifikiria tutakwenda kutoza kodi ile na ikatekelezeka, lakini matokeo yake tumekuja Desemba tumebadilisha sheria. Eneo lile sasa tumeligeuza kuwa ni *exercise duty*, tumeliona. Kwa pengine namna kama hiyo tungekuwa tumepata nafasi ya kufanya *analysis* ya kutosha, nadhani leo tungekuwa tunazungumza vitu vingine.

Eneo la *money transfer*, wakati tumeanza kutekeleza hili, nashukuru sana Kamati ya Bajeti kwa kuleta vyanzo kama hivi. Chanzo hiki cha *money transfer* tuliambiwa tunaweza tukapata bilioni 25.5, mwaka huu ambao tunamalizia. Makusanyo halisi mpaka sasa hivi ni bilioni 18.8 na kwa sababu kumekuwa na ugumu fulani wa kulitekeleza, ni eneo ambalo

linatekelezeka, lakini tungepata tu fursa ya kupata *analysis* kidogo vipi tutatekeleza ndiyo ingekuwa vizuri zaidi. Tumelibadilisha na sasa hivi kwenye *Finance Bill* tumeweka *proposal* nyingine, ni eneo lile lile lakini ni lazima tupate muda wa kwenda kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo la huduma ya simu, tuliambiwa tutaweza kupata bilioni 600 kwa kuimarisha tu usimamizi wa utozaji wa kodi kwenye Makampuni ya Simu. *TCRA* nayo imehimizwa sana kusimamia, lakini *indicative revenue* ambayo tuliwekewa tupate ni bilioni 600. Tulipobadilisha *simcard* kuwa *exercise duty* na maeneo mengine *amount* ambayo tumekuwa tukipata kama *revenue* ni ndogo sana, wakati tuliambiwa eneo hili tutapata shilingi bilioni 600.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, ninachowaomba sisi kama Serikali tupo pamoja, sote tunajenga nyumba moja, Serikali haiwezi ikaona chanzo cha mapato halafu ikakataa tu kukusanya. Sisi ndiyo Serikali, tunasimama saa nyingine unasikia huruma, Mama Anne Kilango anasimama anasema kwake anahitaji wakunga 15, lakini mapato ama utekelezaji unakuwa mgumu kwa sababu ya ukosefu wa fedha pamoja na mambo mengine. Sasa tukiwa tunapewa vile vyanzo, naomba tupate fursa, Wataalamu tunao wa kutosha na wengine tunaweza tukashirikiana pamoja na Wabunge kuweza kufanya *analysis* ya kutosha, jinsi gani kodi inaweza kutozwa. Tutashirikiana pamoja kwenye hili na kamwe sisi hatutaona chanzo cha mapato halafu tukasema hatutakitoza. Sisi ndiyo tunaotekeleza bajeti na tunaujua ugumu wa kutekeleza bajeti hii na sisi ndiyo tunaujua ni ugumu gani tunauoupata kama bajeti haijatekelezeka.

Eneo moja la Uvuvi wa Bahari Kuu; namshukuru sana Mheshimiwa Hamad Rashid, amekuwa akipigia sana kelele kwamba, lazima tupate mapato kwenye Uvuvi wa Bahari Kuu. Amekwenda amerudi amejitahidi na sisi sasa imetubidi tufanye kazi ya ziada kwenye eneo hili. Mheshimiwa Hamad Rashid, tutalifanyia kazi eneo hili, lakini naomba ieleweke kwamba, ni eneo ambalo linahitaji nguvu nyingi na linahitaji *investment*.

Amelizungumza Mheshimiwa Dkt. Kamani, imetubidi mimi pamoja na mwenzangu Mheshimiwa Samia Suluhun twende Zanzibar kwenye Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Tumefanya na sisi *research*, tumekuwa tukibadilishana *articles* nyingi sana na ninaamini kwamba, eneo hili litazaa matunda hivi karibuni. Siyo eneo ambalo tunaweza tukasema leo tubadilishe chanzo kimoja cha mapato, kwa sababu kuna *revenue* kwenye uvuvi wa Bahari Kuu na tukapata mapato kesho. Eneo hili linahitaji umakini wa hali ya juu, linahitaji *investment* na linahitaji *bold decision;* tutafanya Mheshimiwa Hamad Rashid. Tunakushukuru sana kwa hilo.

Waheshimiwa Wabunge wengi mmesimama mkasema Bahari Kuu, lakini Mheshimiwa Hamad Rashid anaposimama akisema Uvuvi wa Bahari Kuu anajua nini anamaanisha. Anajua *exactly* nini anamaamisha. Siyo uvuvi wa kwenda kutupa nyavu ukavua samaki, hapana, ni uvuvi wa Bahari Kuu kwenye *international waters,* ni kitu ambacho ni tofauti na tunachokiona sisi.

Mheshimiwa Spika, wengine wakawa tu wanatofautisha mbona *prawns* tunaweza kuwavua. Kuna *fountain* hapa nje, ingekuwa ya maji ya chumvi tungeweza kuweka *prawns* na wakakua na tukaweza kuvuna. Hapa tunazungumzia Uvuvi wa Bahari Kuu na tunachokizungumzia hapa ni wale Samaki aina ya Chuna, ambao tunaweza tukafikiria leo wapo lakini kesho wakawa tayari wameshahamia Msumbiji. *Scenario* ni tofauti kabisa. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tunataka muda kama Serikali, twende tukalifanyie kazi na tutalifanyia kazi kwa kina na tutakuja na mapendekezo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Hamad Rashid tunaomba tuchukue hiyo *commitment* kwako pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba, eneo tutakwenda kulifanyia kazi kwa pamoja.

Kwa sababu wewe ni mtaalamu wa mambo hayo, pia tutape *consultation* yako kwenye hili. Tunaomba uunge mkono hoja ili twende tukalifanyie kazi eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lilikuwa ni kuhusiana na Deni la Taifa. Deni la Taifa ni kitu ambacho kila siku tunasimama inabidi tuelezee, lakini tutakuwa tunaelezea kila siku. Hii ni ajenda ambayo sasa hivi inapatikana sana kwenye *media* hasa baada ya kaka yangu Mheshimiwa Kangi Lugola kuzungumza pamoja na maadui wa bajeti, adui mmojawapo ni Deni la Taifa. Inawezekanaje Deni la Taifa likawa adui wa bajeti sijaelewa!

Deni la Taifa limekuwa likikua kwa sababu *trend* ya kwenda Deni la Taifa haimaanishi kwamba, mfano, mwezi Julai, 2013 deni lilikuwa *this much* na leo ni *this much*. Kwa hiyo, watu wana-*compare* pale tofauti ya ukuaji ni kwa sababu tumechukua mikopo mingi na kuna maelezo tofauti.

Tunasema kwamba, Deni la Taifa linakua ama liko katika hali ilivyo, kwa sababu ni kitu ambacho ni *movable,* yaani ni kitu ambacho hakipo *static*. *Data* za leo za Deni la Taifa haziwezi kuwa *data* za kesho, kwa sababu kuna baadhi ya mikopo ambayo ilichukuliwa miaka 40 au 50 nyuma, ina-*mature* leo na inabidi tuanze kulipa leo ama kuna *interest rates* ambazo inabidi leo uwe unalipa na kuna mambo mengi. Kwa hiyo, ukuaji wa Deni la Taifa unasababishwa na mambo mengi, pamoja na kuchukua baadhi ya mikopo kwa sababu mkopo *treatment* yake na hususan mikopo ambayo siyo ya kibiashara, *treatment* yake pale unaposaini ina maana inaingia katika *database* yako kama ni Deni la Taifa.

Sisi kama Serikali wakati tunachukua deni hili, tunachukua kwa uangalifu, kwa sababu tuna sheria, hatuchukui deni hili au hatuchukui mkopo bila kuangalia sheria. Vilevile tunahakikisha fedha ambazo tunazichukua ni fedha ambazo zinakwenda kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hatuwezi tukachukua tukatumia halafu tukaona kwamba hakuna uzalishaji, maana yake nini? Mapato tunayopata ndiyo tunayokwenda kulipia Deni la Taifa ambalo halikuwa na tija.

Mheshimiwa Kangi Lugola, Deni la Taifa si adui wa bajeti kabisa. Mwaka jana tulipokuwa hapa ulileta picha na ulikuwa unasema kwa nguvu sana jinsi wanawake wa kwenye Jimbo lako wanavyopata tabu kwenye maji. Sasa mwaka huu mimi na Profesa tunahangaika, katika *portion* yetu ya *Non Concession Borrowing,* yaani mikopo ambayo siyo mikopo nafuu, mikopo ya kibiashara, eneo moja ambalo tutakwenda kulifanyia kazi kwa nguvu yote ni eneo la kuweka miundombinu ya maji nchini. Maana yake ni nini? Hata kwa Mheshimiwa Kangi naye atapata maji. Sasa inakuwaje eneo lile tunakwenda kuchukua mkopo? Kwa sababu ndiyo mikopo ambayo inapatikana kwa haraka zaidi na tunajua Wabunge wengi mmesimama mnaonesha ile dhiki ya kutokupatikana maji katika Majimbo yenu, twende tukapeleke! *(Makofi)*

Sasa baadaye Deni la Taifa litakua kwa sababu tumechukua ule mkopo, sasa inakuwa yenyewe ndiyo adui wa bajeti a*u otherwise* pengine inawezekana kuna siku ikaja Serikali ikawa haikopi, tumesema *stop*, tunafuta jamani Waheshimiwa Wabunge wamesema Deni la Taifa limekuwa kubwa basi tusikope, sawa! *With our twelve trillion* sijui tutagawanaje na tunataka maendeleo kwenye kilimo, barabara, umeme na kila kitu.

Tanzania is a developing country. Sisi ni nchi ambayo inaendelea, kwa hiyo, hilo eneo hatuwezi kuliepuka kwa sababu kasi ya maendeleo yetu na kasi ya mahitaji yetu, haijakidhi vyanzo vyetu vyenyewe vya ndani. Kwa hiyo, pamoja na hatua nyingine, tutaendelea kuchukua hii mikopo, lakini mikopo tutaendelea kuichukua kwa uangalifu, kwa kuzingatia sharia, lakini tutaendelea kuichukua mikopo hii ili twende tukawekeze katika Miradi ya Maendeleo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tunaomba mtu-*support* kwenye hili na tunasema tena kwamba, Deni la Taifa linahimilika kwa vyanzo vyote. Nasema tena, Deni la Taifa linahimilika kwa vyanzo vyote. Tunaomba tusimame sote kuhakikisha kwamba, fedha zinazopelekwa ambazo zimechukuliwa kwenye mikopo hii, ziwe zinatumika kama zilivyo.

Mheshimiwa Spika, tumekuja na wazo sisi kama Serikali la kupunguza umri wa magari ya kutozwa ushuru wa uchakavu kutoka miaka kumi hadi minane. Kuna sababu nyingi na sisi Serikali kama tunaleta *proposal* haimaanishi kwamba tupo *against* na Wananchi, hapana. *Is a high time now* kuona kwamba hata Mwananchi ambaye ana uwezo wa kununua gari, basi ainunue gari hiyo ambayo itakuwa ina umri wa miaka minane na siyo kumi. Sababu ni nyingi, siku nawasilisha bajeti Waheshimiwa Wabunge nilimwona hata Mheshimiwa Mbowe ali-*rise* kidogo wakati nampa *data.* Kuna mambo mengi, ajali *is one of the thing,* lakini kuna mambo mengi ambayo yanasababishwa na uchakavu wa gari.

Kwanza, tunalinda mazingira, tunapunguza matumizi ya fedha za kigeni na mambo mengine pamoja na ajali. Waheshimiwa Wabunge, wakati *proposal* hii tumeileta mwaka jana au mwaka juzi, tulirudishwa kwa nguvu zote mliikataa. Tunasubiri tena, sisi tunaleta. Matokeo yake sasa, nchi hii tulipata *revenue* kubwa, yaani *revenue* ilikuwa ni 226% ya ile *estimation* kwa sababu magari yaliingia.

Mheshimiwa Spika, wakati tumetangaza tu ile kodi ya 25%, magari ya Japan ambayo yanauzwa Dubai na *elsewhere,* yalishuka *drastically*. Bei ilishuka sana na watu sasa wakawa wanaingiza magari kwa wingi. Kwa nini kama tunaleta *proposal* tunasema hiki si ndiyo chanzo cha mapato basi tungezidisha zaidi ya umri sasa leteni zaidi ya miaka 15, ingekuwa hiyo ndiyo sababu na tungepata fedha kweli, lakini hilo siyo lengo.

Tanzania sasa imekuwa ndiyo *dumping country*, imekuwa nchi ambayo wenzetu wanaotengeneza huko, wanasubiri sana wakati kama huu kuona ni jinsi gani wanaweza wakacheza na bei, Wananchi wa Tanzania waje kuchukua magari kutoka huku tuliko. Sasa kwa nini mtu gari ya miaka minane yeye aende akai-*dump* kama iko nzima? Inachukuliwa anakuja kuuziwa Mtanzania. Bei ilishuka, nimepata taarifa hata bei ya Prado ikauzwa dola 3,000 baada ya kutangaza tuongeze ule ushuru.

Mheshimiwa Spika, hatukosi kutoa huu mfano, sasa hivi bandarini kuna magari 1,000. Bandarini kuna mtu amenunua magari 1,000 peke yake, yamekwama pale anashindwa kuyatoa, *TRA* wanaanza kuyapiga mnada. Anasubiri kitu gani, maana yeye kwanza aliyaleta kwa sababu anajua *definitely* hapa atatoa tu, kwamba haya ni magari ambayo hakuna *policy measure* isipokuwa ni ushuru wa 25%. Ameyaleta ameshindwa kuyatoa. *A thousand vehicles,* mtu mmoja, awe amepata fedha kokote, lakini asije akatuletea sisi humu ndani magari ambayo yana umri kama ule! Anachelea hawezi kuyapeleka kwingine, anayaleta Tanzania kwa sababu ndiko tunakoyapokea.

Sasa Waheshimiwa tukisema tunataka miaka minane, Mtanzania huyu huyu atakwenda kununua gari lililo nafuu, lenye umri mdogo wa miaka minane. Wabunge mnakataa lakini tuone ukweli, huu ndiyo ukweli ulivyo. Tunakaa na Waheshimiwa wengine, wanafanya biashara ya magari, *I know*. Sasa najua kwamba, wengi wetu tunaweza tukalipinga kwa kusingizia eti Mwananchi atashindwa kununua. Gari lile alilokuwa akilinunua miaka kumi kwa dola zile zile 3,000, atalinunua lenye umri wa miaka minane kwa dola zile zile 3,000. Kwa sababu atalipeleka wapi? Tanzania ndipo linaponunuliwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu wanachokifanya, wanakwenda katika *total ban,* sisi hatujataka kwenda kwenye *total ban,* tumesema *gradually* tutataka tupunguze huu umri.

Wenzetu wakienda kwenye *policy* kama hii wanakwenda kwenye *total ban*, hakuna ku-*compromise*, hakuna nini, wana-*ban* kabisa. Kuna nchi nyingine gari ni la umri wa miaka minne tu na nyingine miaka mitano huingii.

Kwa hiyo, jamani tukileta hizi *proposals* tumezifanyia kazi kwa kina kabisa na tunaleta hapa kwa masilahi ya hao hao Wananchi ambao sisi sote tunawawakilisha. Waheshimiwa Wabunge, hili ni jambo linguine, tunaomba tutakapolileta mlifikirie. Mtanzania ataweza kupata gari kwa bei nafuu, lakini ambayo ni mpya kabisa.

Mheshimiwa Spika, *at the same time* tumeshashauriana na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani katika kuimarisha *inspection*. *Inspection* ya magari nalo ni eneo lingine ambalo limezungumzwa. Sasa katika mafungu hayo ambayo tumeongeza, kuna mengine ni kwa ajili ya askari, labda mengine yatakwenda kwenye *ration allowance*. Angalau tuongeze *ration allowance,* lakini wafanye kazi yao ikiwa ni pamoja na kufanya *inspection* ya magari, maana tunasema ongeza, ongeza, lakini ukimwangalia aah anafanya kazi yake inayostahiki. Sisi kama Serikali tunaongezea watu *ration allowance,* wakiwemo askari pamoja na askari wa barabarani, lakini tunaomba wafanye kazi yao ya *inspection* kuhakikisha magari yanakuwa *inspected* kikamilifu kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni *Pay As You Earn (PAYE),* ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge. Sikuwepo lakini ninaamini Mheshimiwa Celina Kombani, naye amelizungumzia. Tumepunguza asilimia moja kutoka 13% ya *PAYE* mpaka 12%, lakini ni ahadi yetu kwamba, eneo hili tutakwenda kupunguza *gradually* mpaka ifikie *single digit*. Sababu ambazo Waheshimiwa Wabunge mmezitoa, kwa lengo la kutaka sasa hivi ndiyo tupunguze mpaka tufikie *single digit* leo hii, ni nyingi lakini mojawapo ni katika kuimarisha hali hii ya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, tunajua na ndiyo maana wakati tunashusha ile kodi kwa asilimia moja, *at the same time* tunapandisha kiwango cha mshahara wake, ambacho kinapanda zaidi kuliko ile *percent* ambayo sisi tumeshusha. Kwa hiyo, hilo ni eneo ambalo tutakwenda nalo *gradually*, wakati tunapunguza *PAYE* tutakuwa vilevile tunaboresha masilahi kupitia mishahara hii ya wafanyakazi. Tunalo, sisi Serikali ndiko wafanyakazi wengi wanafanya kazi hizo, tunahakikisha tutalichukua kwa nguvu zote na ndiyo maana mara hii tumeweza kuongeza kima kwa asilimia kubwa kidogo, lakini tumepunguza kidogo kwenye *PAYE*.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lilikuwa ni suala la madai, mwenzangu alizungumza kidogo, lakini ninaomba nisisitize kidogo kwenye eneo hili. Tunapokwenda kwenye Bajeti yetu ya 2014/2015, tunachukua sana *experience* ya 2013/2014. Tunajua kuna Wakandarasi ambao wanadai sana Serikalini na hawajalipwa, wana-*suffer* na wengine hata wanachukuliwa *assets* zao kwa kukosa fedha ambazo ingepaswa walipe. Kwa hiyo, tunapokwenda *priority* yetu ni kuanza kulipa madeni ya wakandarasi na wazabuni, hususan tukianza na wazabuni ambao wako katika mikoa.

Pamoja na madai ya Watumishi, labda pengine itaonekana Serikali kwa nini haifanyi hivi! Tumekuwa tunafanya hivi kidogo kidogo, lakini kuna mambo mengi ambayo yametokezea mwaka huu ambao tunaumalizia. Kwanza, hatutaweza kulipa kama hatujafanya uhakiki. Tumefanya hakiki mbalimbali na ninaomba ku-*share* na ninyi matokeo ya uhakiki wetu, ambao unasababisha kwa kiwango kikubwa kuchelewa kulipa madai haya ya Wakandarasi pamoja na Watumishi.

Mheshimiwa Spika, tulimpa kazi *Internal Auditor General,* aende akafanye *auditing* ya madai ya Walimu. Madai yaliletwa ofisini kwa ajili ya malipo, lakini kwa sababu hatutaweza

kulipa mpaka tufanye uhakiki, *Internal Auditor General* alifanya kazi ya uhakiki maalum kutokana na madai. Faili la madai kutokana na madai lilikuwa lina upana mkubwa kidogo, lakini *amount* ya madai yale ilifikia zaidi ya shilingi bilioni 19, hiyo ndiyo *amount* ya madai ambayo ililetwa ili Hazina tulipe.

Mheshimiwa Spika, tulipofanya uhakiki ambao ulichukua karibu miezi minne, *Internal Auditor General* amekwenda mpaka kwenye Halmashauri, kama mdai anaitwa Sanya au *somebody*, lakini amewasilisha madai mengi sana; anadai posho ya safari, posho ya utumishi, hajaongezewa hiki, risiti yake hii haijalipwa. Kuna Baba kama huyu ambaye ninatoa taarifa yake, wakati tunaletewa ile hoja madai yake yalifikia shilingi milioni 600, lakini hatuku-*doubt,* tukasema kwa sababu sisi tunafanya uhakiki twende kwenye Halmashauri.

Tumekwenda tumepata *particulars* za yule mtu na tulimfuata mpaka nyumbani kwake. Kaka yangu wewe unadai, hebu kwanza tuambie unadai kiasi gani maana hapa tunaona unadai shilingi milioni 600. Yule kaka alianza kushangaa, shilingi milioni 600! Kwa sababu huwezi kufikiria hata na yeye hakuweza kufikiria kwamba anaidai Serikali shilingi milioni 600. Akasema hapana, ninachokidai mimi, akaenda akachukua risiti zake, alikuwa ameweka *copy,* anazo risiti zake, risti moja baada ya nyingine, anachokidai ni shilingi 600, 000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo *scenario* ambayo tunaipata. Madai yale yote tulipokwenda kufanya uhakiki wa mtu kwa mtu, kutoka shilingi bilioni 19.4 yameshuka mpaka shilingi bilioni tano. Kinachodaiwa kwa Serikali ni shilingi bilioni tano. Hiyo ndiyo hali ambayo inatukuta sisi Hazina, lakini tunasema kwamba, hatutalipa kama hatujafanya uhakiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhakiki ni lazima na safari hii tutakwenda *even further*. mwenzangu Mheshimiwa Malima amesema, yeye aliongelea eneo la *procurement*, lakini sisi tutahakikisha kwamba, wale wote wanaoleta hayo madai, maana ni Watendaji ambao tunawalipa kwa fedha hizi za walipa kodi, tutawachukulia hatua. Tuko *serious* kwenye hili, Serikali hii iko *serious* kwenye hil,i tutawachukulia hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *scenario* nyingine ambayo tuliipata Serikali inadaiwa shilingi trilioni 1.43. Shilingi trilioni, siyo milioni, ni trilioni, *we are talking about* kama hizi *exemption* tunazozitoa inadaiwa Serikali. Tumekwenda kufanya uhakiki, tulichokikuta kinadaiwa ni shilingi bilioni 143. Kwa hiyo, tunajua Wakandarasi na Wazabuni wanadai, lakini tunaiweka Serikali katika *position* mbaya kwamba, kwanza, tutachelewa kukulipa mpaka tukufanyie uhakiki, sasa unavyoleta madai ya uongo ndivyo ambavyo tutachelewa kukulipa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninyi ndiyo ambao mnakaa kwenye Halmashauri na Watendaji, tunaomba eneo hili tulisimamie kwa nguvu zote, kwa pamoja. Serikali hatuwezi kusimama peke yetu tukaweza kukamilisha kila kitu. Lazima mtusaidie na ni lazima sisi Waheshimiwa Wabunge tufanye kazi yetu, tukija hapa sote tuwe tumewajibika katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, tunapokwenda hiyo tutaipa *priority* lakini hatutalipa kama hatujafanya uhakiki na tutaendelea ku-*strengthen* vilevile Ma-*auditor* kwenye taasisi. Tuna wasiwasi mkubwa kwamba, hata hao ma- *auditor* wanaofanya kazi kwenye taasisi, kwa sababu wao wanapaswa wazipitie zile taarifa kabla ya kuzileta Hazina, tuna wasiwasi na utendaji wao. Tutafutilia tuone hawa hawawi *compromised,* wafanye kazi yao kama inavyostahiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine kubwa lilikuwa ni kuhusiana na baadhi ya mafungu kutopelekewa fedha za kutosha. Nimelizungumza hili na ninaendelea kulisisitiza tena, bajeti yetu

mpaka mwezi Mei *performance* yake ilikuwa *around* 75%, tumezidi kidogo kwa sababu kuna mapato tumeyapata katika kipindi hiki *between end May* na *June*. Ninasisitiza tena kwamba, tuna-*admit* kwamba, bado kidogo lazima tupate uwezo mzuri zaidi wa kukusanya mapato na tutatafuta vyanzo vipya vya mapato kwa kushirikiana na ninyi Waheshimiwa Wabunge.

Tunaomba sana pale pale ambapo fedha zitakuwa zimepelekwa kwa 30% au 40%, jambo la kwanza ambalo tunapaswa tulitazame ni kama ile asilimia imetekeleza kile ambacho kimekusudiwa. Tunapokwenda 2014/2015 tutakuwa *even tight* kama hujaleta ripoti ya utekelezaji na tutakwenda kufuatilia hicho ulichokitekeleza, hatuta-*disburse* fedha yoyote. Fedha ambayo tuta-*disburse* ni eneo ambalo tutapata ripoti ya utekelezaji na kuhakikisha kwamba, kilichokuwa kimeainishwa ndicho kilichotekelezwa.

Kwa hiyo, Waheshimiwa tunaomba tuwajibike katika hili. Sisi tuko kwenye Halmashauri, kwenye hiyo Miradi inakotekelezwa, tunaomba sana sote kwa pamoja tusaidiane katika eneo hili na pale ambapo tutaona kuna ubadhirifu wa fedha tuseme. *Sometimes* inakuwa mko huko kwenye Majimbo mnaona baadhi ya haya mambo, tusisubiri tuje Bungeni ndipo tuyazungumze. Unaweza ukazungumza huko uliko, tupe tu taarifa kwamba, hili ni jambo ambalo linatokezea huku, kama wewe mwenyewe hujaanza kuchukua hatua zinazofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu kwa upande wa Washirika wa Maendeleo tunakokwenda ndiyo itakuwa mbaya zaidi, kwa sababu *approach* ambayo itatumika ni *performance based disbursement*. Watakwenda kuangalia *performance* imekamilika na ndivyo walivyotarajia, *indicators* ziko sawa, ndipo wata-*disburse*. Hakuna eneo lingine, *there won't be any free money, there will be only money* kwa ajili ya utekelezaji.

Approach hiyo ndiyo ambayo tutaanza kuichukua sisi Serikalini, *performance based disbursement*. Sasa Waheshimiwa Wabunge kama tutataka maji kwa Wananchi, kile ambacho tumekipeleka tunaomba tuhakikishe kimesimamiwa vya kutosha, kimeleta matokeo, halafu tuje ku-*disburse* fedha nyingine. Wenzetu wameamua na kama wameamua ni lazima sisi ndiyo tuanze kuamua kwanza kabla ya wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna eneo lingine Waheshimiwa Wabunge tumelizungumza sana kuhusiana na vyanzo vya mapato. Tumeweka kodi na safari hii msamiati mkubwa ambao umetokezea hasa kwenye *media* zetu ni kwamba, bajeti hii inategemea pombe na sigara. *I was even surprised,* kwa sababu ukiangalia hiyo *calculation* ni 0.6% ya *total budget* ndiyo *revenue* yake.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati tunakwenda kwenye vyanzo vipya, hatutakuwa tuna-*abandon* vile vyanzo vya kodi ambavyo vipo. Sekta inakua tutatoza kodi, hatutarudi nyuma, lakini tuwe wakweli. Waheshimiwa Wabunge, wengi mliposimama kudai kodi ya mfanyakazi ishuke kutoka 13% kwenda 12%, kila mmoja alikuwa na sababu zake na zote ni za msingi. Mfanyakazi huyo hakuweza kufika Dodoma kuja ku-*lobby* kwa Wabunge, ninyi wenyewe ndiyo mme-*feel*.

Leo tumetangaza vyanzo vya mapato, wafanyabiashara wakubwa wako Dodoma; haiwezekani! Hakuna mtu anayetaka kulipa kodi na sababu zitaelezwa nyingi. Ukimpa mtu nafasi ya kukuelezea; mimi maana yake bora, kodi hii sijui sekta yangu itakua, mimi mkinitoza kodi hii itanikwaza nitaondoka! Mtu atakwambia sababu zake. Sisi tuna vitengo chungu nzima tunavifanyia kazi hivi vyanzo vya kodi. *Tuna Task Force* inakaa, inakesha. Safari hii tumekwenda na Wataalam wetu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tunasema hebu eneo hili, wamekwenda wamefanya kazi. Waheshimiwa leo wanakuja wanazungumza kwamba, aah, eneo hili Serikali

imetangaza lakini msitutoze kwa sababu sisi tutapata hasara. Nani atakwambia anapata faida? Hataki kulipa kodi, nani atasema anapata faida? Kodi lazima italipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mfanyakazi anatozwa kodi, na mfanyabiashara kama anapata faida atatozwa kodi. Kodi lazima ilipwe. Waheshimiwa tunaomba, tuwe pamoja kwenye hili, kodi lazima ilipwe. Kama tunasema deni la taifa linakua, tukisimama kutokukopa maana yake fedha ya ndani ndiyo ifanye kazi. Kama mfanyabiashara hataki kulipa kodi, anaona anapata hasara…

MBUNGE FULANI: Ahame! *(Kicheko/Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Huo ndiyo ukweli. Tunakuja tuna-*negotiate*, natumiwa *message* Waziri utakwenda pale utaadhirika; *I am ready to fight* kodi ilipwe. *(Kicheko/Makofi)*

Eneo lingine ni kuhusiana na *CHC*. Nadhani hili lilizungumzwa sana na Mheshimiwa Mariam Msabaha. Tunatoa tu taarifa kwamba, tulim-*consult CBE,* Chuo chetu cha Biashara, kufanya kazi kuhusiana na kuendelea ama kutokuendelea kwa *CHC*. Ripoti yake tayari imeshatuelekeza na itapita katika ngazi za Serikali ili kuwa *adopted*.

Mshauri Mwelekezi katika mchanganuo wake, ameonesha kwamba, kwanza, mapato ya *CHC* yanatokana na makusanyo ya madeni, mauzo ya samani na ubinafsishaji. *CHC* yenyewe sasa hivi kwa sababu ile kazi imeshakwenda muda mrefu, utaona hata yale mapato yameshuka, kwa sababu kazi za ubinafsishaji sasa hivi zimeshuka sana. *Existence* ya *CHC* na wakati Serikali inaendelea kuimarisha Msajili wa Hazina, ambazo kazi zake karibu zinalingana na *CHC,* tumeona katika *spirit* ile ile ya kubana matumizi ya Serikali kwamba, *CHC* imalize muda wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *capacity* kubwa imejengeka kwenye *CHC* na tunaahidi kwamba, wafanyakazi wale wataendelea kufanya kazi zile wakati tuna *institution* yetu iliyokuwa *strengthen* ya *Treasury Registrar.* Kwa hiyo, tutaleta rasmi Bungeni kwa sababu lilikuwa ni Azimio la Bunge la kuongeza muda na sisi tuko katika *government machinery* kuangalia tunakwenda kisheria jinsi ya ku-*wind up CHC*. Kwa hiyo, wafanyakazi tunaowahitaji, tuna *capacity* pale tumejenga na tutaleta taarifa, lakini ni maamuzi sasa kwamba, *CHC* imalize muda wake. *At the same time,* Ofisi yetu ya *Treasury Registrar* tuweze kui-*strengthen* ili tuweze kuchukua kazi zilizobakia na kazi mpya ambazo zitakuwa hapo baada ya *CHC* kuwa *winded up*.

Hoja zilikuwa nyingi na kulikuwa kuna hoja nyingine vilevile ya kupunguza tozo ya ufundi stadi kutoka asilimia sita hadi nne. Tumeingalia na hii hoja wameifanyia kazi sana wenzetu wa Kamati ya Bajeti na mwaka jana tulipunguza kutoka asilimia sita mpaka tano. Tutaiangalia kwa mapana zaidi, kwa sababu kodi hii si kodi ambayo inakwenda kwenye matumizi ya Serikali. Sote tuna ndugu zetu ambao wako Vyuo Vikuu na hawana uwezo lazima wapate mkopo kutoka Serikalini. Kwa hiyo, *SDL* ndiyo chanzo ambacho tunatumia kwa ajili ya kuwapa wanafunzi mikopo. Kwa hiyo, tutaendelea kuiangalia wakati vilevile tunatanua wigo wa kodi hii kwenye Mashirika mengine.

Kulikuwa kuna eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge, mmelisisitizia sana kuhusiana na kuendelea kwa matumizi ya *Electronic Fiscal Devices*. Serikali tutaendelea kulisimamia eneo hili, kwa sababu lina *advantage* kubwa. Kama alivyosema Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola, adui mmoja wa bajeti ni rushwa na rushwa nyingine inayotokea ni kwa sababu watu wanakutana; wakati tunafanya malipo tunakutana tunaweza tuka-*negotiate* hata kama ni ile haki yako ama haki ya mwingine wewe unaweza uka-*negotiate*. Sasa

matumizi yetu kusisitiza tumieni *Electronic Fiscal Devices* kwa sababu mnalipa kodi *electronically,* hamna haja ya kukutana na mtu wa *TRA*. *(Makofi)*

Sasa hii nyingine nayo imekuwa ni ajenda ambayo inapelekwa, yaani sijaelewa! Tuna nia nzuri, kama unachukia rushwa tumia *EFD*. Kama unachukia rushwa basi wewe hakikisha yule ambaye anakuja kuchukua malipo huonani naye, lipa *electronically* basi. *At the same time* wakati tunataka watu watumie hizi *EFD,* Waheshimiwa Wabunge, mdai risiti mnapofanya manunuzi. Vilevile tudai risiti, hakuna ku-*compromise,* mwuza duka anashangaa ukianza kumwomba risiti *no, you have too*. Dai risiti yako. Kama tunataka maji yaende sehemu fulani, dai risiti uone ile kodi inapokwenda Serikalini itakwenda kutengeneza miundombinu ya maji.

Sasa kama wewe mwenyewe hujajitahidi katika eneo hili, tunakuja mimi kijijini kwangu, Jimboni kwangu, hakuna maji, vijiji saba havina maji; ni kweli lakini wewe umefanya wajibu wako gani, tuanze kudai risiti. *I wish* ningekuwa na uwezo wa kufanya ukaguzi nione *how much* mmefanya manunuzi na mmedai risiti, lakini siwezi. Hiki ni kitu ambacho *serious* lazima tuanze kulipa uzito wa pekee eneo hili. *(Kicheko/Makofi)*

Bajeti hii inayokuja kama hatujashirikiana sote hatutaweza kuitekeleza. Tutakuja mwakani tunaidai Serikali hujafanya hiki, hujafanya hiki, hakuna mtu atakayesema mimi sijafanya hiki kwenye kutekeleza wajibu wangu. Sote tuapaswa tusimamie utekelezaji wa bajeti hii, ni wajibu wetu sote.

Kwa hiyo, tunaomba tuhimize matumizi ya *EFD*. Wengine walifanya mtaji kwenda kupotosha tu, tulifanya mtaji wengine tuna nia njema. Tunaondosha kodi kwenye mashine za *Electronic Fiscal Devices*, wafanyabiashara waweze kupata hii kwa bei nafuu. Vilevile kuna baadhi ya Mabenki yamesema yako tayari kuwakopesha wafanyabiashara waende wakachukue *EFD* watumie. *EFD* ni kama wewe mwenyewe unafanya biashara umenunua kompyuta yako nyumbani, *is yours,* lakini bado Serikali ina-*sacrifice* mapato yake. Kwa sababu ukishakutoa zile gharama zako pamoja na gharama za ununuzi, kuna kodi pale unasamehewa. Kwa hiyo, ni sawa sawa tu kwamba, Serikali imekupa ile *EFD*.

Tunaomba tuwe Mabalozi kwa wafanyabiashara kwa wanaostahiki kutumia *EFD,* yaani kuwashajihisha matumizi haya. Tutapunguza rushwa kama si kuondosha kabisa, vilevile mfanyabiashara atakuwa anakatwa kodi yake inavyostahiki, kutakuwa hakuna *presumptive tax,* lakini vilevile Serikali itapata mapato yake inavyostahiki na hivyo eneo lingine tutaangalia la kusimamia matumizi yenyewe. Mradi Serikali imepata mapato yake, vilevile Waheshimiwa hili nalo tutakuwa tuna wajibu nalo.

Kulikuwa kuna hoja hii ya malimbikizo, nadhani nimeshaielezea vya kutosha. Ucheleweshaji wa fedha, tumeelezea tutajitahidi, kama tutasimamia vizuri vyanzo vyetu vya mapato, lakini kama tutasimamia vizuri matumizi haya ya Serikali.

Hoja nyingine tumepewa *alert* kwamba, Washirika wa Maendeleo sasa wanahama kutoka kuchangia misaada ya kibajeti kwenda kuchangia miradi. Serikali ijiandae kupokea utaratibu huu kwa kuainisha Miradi muhimu ambayo itakuwa na matokeo makubwa. Tumelichukua na ndilo eneo ambalo tunalifanyia kazi kwa sasa. Tuko katika *negotiations* kukubali *exactly* Miradi gani ambayo italeta matokeo makubwa na tuko na wenzetu vizuri zaidi.

Sasa hivi kuna baadhi ya washiriki wameshaainisha maeneo ambayo watakwenda ku-*support* kwanza, kwa mfano, tukichukulia *DFID* UK, yeye amesema atakwenda ku-*support* eneo la elimu na maji. *Approach* yake ni *approach* ambayo atatumia *performance*. Sasa hivi tunakwenda kuangalia ni jinsi gani sasa ataweza yeye kusimamia *performance,* lakini Serikali

ndiyo iwe ina *ownership*. Kwa maana hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mna kazi kubwa sana katika kulisimamia hili. Naamini kwamba, tutakwenda tu vizuri, *Inshallah.*

Mwisho, mambo yalikuwa mengi wenzangu wameshayasema mengine, lakini naomba kusisitiza kwamba, tutajitahidi, tumejipanga vizuri, tutatekeleza, tunaomba *support* yenu, tutakuwa pamoja kwenye hili hususan utekelezaji huu wa bajeti. Tunaomba sana tuwe pamoja. Eneo kubwa ambalo tutalisimamia vilevile ni katika matumizi. Tunahamasisha sana matumizi ya TEHAMA kwenye maduhuli. Tunahamasisha sana taasisi zetu hususan Taasisi za Serikali katika kupunguza matumizi, kuna kazi za *consultancy* zinafanywa, tuna *consultant* wetu wa ndani ambao wanafanya kazi nzuri sana.

Eneo kubwa ambalo tunaendelea kuliimarisha ni eneo letu la *E-Government Agency*, Tunataka sasa hizi Taasisi zote za Serikali wakati wanataka ku-*procure consultancy* hususan katika wale ambao wanaweka Mifumo ya TEHAMA, *capacity* kubwa na nzuri inapatikana *E-Government Agency*. Wana *capacity* kubwa ya kutengeneza hii Mifumo ya TEHAMA lakini kwa gharama nafuu kweli. Kwa hiyo, tunasisitiza kwamba, ili tujenge cha kwetu sisi wenyewe, kwa hiyo, kupunguza hii tutakwenda na tutaimarisha eneo hili. Vilevile tunataka taasisi zote sasa tuwe tunaelekea kwa *E-Government Agency* katika kufanya *consultancy* hizi za mifumo hii ya TEHAMA.

Serikali tumeambiwa tupunguze matumizi ambayo si ya lazima, tumeanza. Naishukuru sana Kamati ya Bajeti, wakati tumekuja kusoma hapa, maeneo ambayo tumepata zile fedha, shilingi bilioni 165, kwanza, ni katika eneo kubwa la ununuzi wa magari. Ununuzi wa magari tumekata kwa asilimia 50, hatukwenda hapo tu, sasa hivi Hazina tayari tumeshaandaa Mwongozo ambao tutaupeleka kwenye *Cabinet* wa kufanya *bulky procurement*. Magari sasa yatakuwa yananunuliwa kwa pamoja na yatakuwa yananunuliwa kwa *manufacturer* siyo *agency* hapa kati kati. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hakuna taasisi ambayo itakuwa inanunua gari yenyewe. Mwongozo utatolewa na magari yatakuwa yananunuliwa kwa *manufacturer.* Tunahakikisha kwamba, fedha ambayo inataka kutumika kununulia magari, tumeikata hii na tumeikata kwa makusudi mazima. Kuna mafungu yameweka gari aina hiyo hiyo shilingi bilioni 270, kuna mafungu gari ya aina hiyo hiyo shilingi bilioni 250, *anyway* tukasema kwanza *slash* halafu tunatengeneza mwongozo ziende zote zikanunuliwe kwa pamoja zitakuja kuchukuliwa. *(Makofi)*

Huu ni uamuzi mgumu na tutasikia lawama nyingi lakini tumeamua. Tumeamua na hili tutakwenda nalo sana. Tunaomba Waheshimiwa, mtu-*support* naamini kwamba, sote tunajenga nyumba moja na naamini kwamba, tunachokisema kutoka kwenye mdomo, ndicho kinachotoka mioyoni mwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani nimejaribu kuweka hoja vizuri zaidi, tutaendelea kutoa ufafanuzi kwa maandishi hoja ambazo hatujazitolea majibu. Nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, tumetoa *views* zetu nzuri, zina nia ya kujenga.

Mwisho kwa udhati, nawatakia Waislam wote Ramadhani Mubarak, pamoja na Wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana. Hoja hii imeungwa mkono. Sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 107(2)(b), tunapasa kufanya uamuzi kwa kuita mtu mmoja kwa jina lake na atajibu kadiri anavyofikiria inafaa. Asubuhi alitukumbusha Mheshimiwa John Mnyika kwamba, hili pia ni matakwa ya *paragraph* ya 90(2)(b) ya Katiba. Yeye amesema Katiba mbovu, hiyo sawa sawa lakini ndiyo inayotumika sasa.

Naomba ipigwe kengele, waingie wote walioko nje na naomba tukitulia tu kila mtu atasikia jina lake na ataweza kujibu anavyostahili. Tuna *register* hii ambayo ina majina yote, tutaita kufuatana na hii *register* isipokuwa kuna maombi maalum, kuna watu wanapaswa kusafiri usiku huu, tutawapeleka kidogo mbele kusudi waweze kusafiri. Kwa hiyo, naomba kengele ipigwe, siku hizi kengele yenyewe haina hata kelele.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kila mtu akae mahali pake. Wakati wa kupiga kura kila mtu akae mahali pake tupate utulivu.

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo tunaanza.

(Hapa Wabunge walipiga kura kuiamua Bajeti)

Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda - Ndiyo
Mhe. Samuel John Sitta - Ndiyo
Mhe. Job Yustino Ndugai - Ndiyo
Mhe. Anne Kilango Malecela - Ndiyo
Mhe. William Vangimembe Lukuvi - Ndiyo
Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu - Ndiyo
Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli - Ndiyo
Mhe. Prof. Mark James Mwandosya - Ndiyo
Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi - Hakuwepo
Mhe. Stephen Masatu Wassira - Ndiyo
Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe- Ndiyo
Mhe. Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa- Hakuwepo
Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia - Ndiyo
Mhe. Sophia Mattayo Simba - Ndiyo
Mhe. Bernard Kamillius Membe -
Mhe. Mathias Meinrad Chikawe - Ndiyo
Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika- Hakuwepo
Mhe. Cellina Ompeshi Kombani - Ndiyo
Mhe. Gaudentia Mugosi Kabaka - Ndiyo
Mhe. Samia Hassan Suluhu - Ndiyo
Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa- Ndiyo
Mhe. Prof. Annas Kajumulo Tibaijuka - Ndiyo
Mhe. Eng. Christopher Kajoro Chiza - Hakuwepo
Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe- Ndiyo
Mhe. Dkt. Fenella Ephraim Mukangara- Ndiyo
Mhe. Dkt. Abdallah Omari Kigoda - Ndiyo
Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo- Ndiyo
Mhe. Dkt. Asha-Rose Mtengeti Migiro - Ndiyo
Mhe. Lazaro Samuel Nyalandu - Ndiyo
Mhe. Dkt. Seif Seleman Rashidi - Ndiyo
Mhe. Dkt. Binilith Saatano Mahenge - Hakuwepo
Mhe. Saada Mkuya Salum - Ndiyo
Mhe. Dkt. Titus Mlengeya Kamani - Ndiyo

Mhe. Jaji Frederick Mwita Werema - Ndiyo
Mhe. Dkt. Milton Makongoro Mahanga- Ndiyo
Mhe. Adam Kighoma Malima - Ndiyo
Mhe. Agrrey Deaisile Joshua Mwanri - Ndiyo
Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa - Ndiyo
Mhe. Pereira Ame Silima – Ndiyo
Mhe. Mahadhi Juma Maalim – Ndiyo
Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga – Ndiyo
Mhe. Ummy Ally Mwalimu – Hakuwepo
Mhe. Dkt. Abdulla Juma Abdulla Saadalla– Ndiyo
Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge – Ndiyo
Mhe. George Boniface Simbachawene– Ndiyo
Mhe. Stephen Julius Masele – Hakuwepo
Mhe. January Yusuf Makamba – Ndiyo
Mhe. Dkt. Charles John Tizeba – Ndiyo
Mhe. Amos Gabriel Makalla – Ndiyo
Mhe. Angellah Jasmine Kairuki – Ndiyo
Mhe. Janet Zebedayo Mbene – Ndiyo
Mhe. Jenista Joakim Mhagama – Ndiyo
Mhe. Dkt. Pindi Hazara Chana – Hakuwepo
Mhe. Godfrey Weston Zambi – Ndiyo
Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba – Ndiyo
Mhe. Dkt. Kebwe Stephen Kebwe – Ndiyo
Mhe. Kaika Saning'o Telele – Ndiyo
Mhe. Juma Selemani Nkamia – Ndiyo
Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa – Ndiyo
Mhe. Hassan Athumani Ngwilizi – Ndiyo
Mhe. Andrew John Chenge – Ndiyo
Mhe. Luhaga Joelson Mpina – Hakuwepo
Mhe.Victor Kilasile Mwambalaswa – Ndiyo
Mhe. William Mganga Ngeleja – Hakuwepo
Mhe. Dr Hamisi Andrea Kigwangalla - Hakuwepo
Mhe. Lediana Mafuru Mng'ong'o – Ndiyo
Mhe. Margaret Simwanza Sitta – Ndiyo
Mhe. Said Mohamed Mtanda – Ndiyo
Mhe. Peter Joseph Serukamba – Ndiyo
Mhe. James Daudi Lembeli- Ndiyo
Mhe. Prof. Peter Mahamudu Msolla – Ndiyo
Mhe. Anna Margareth Abdallah – Hakuwepo
Mhe. Edward Ngoyai Lowassa – Ndiyo
Mhe. Kabwe Zuberi Zitto – Hakuwepo
Mhe. Rajab Mbarouk Mohammed – Hapana
Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe – Hapana
Mhe. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi – Hapana
Mhe. Vincent Josephat Nyerere - Hapana
Mhe. Esther Nicholas Matiko – Hapana
Mhe. Mch. Israel Yohana Natse – Hapana
Mhe. Pauline Philipo Gekul – Hapana
Mhe. David Ernest Silinde – Hapana
Mhe. Meshack Jeremiah Opulukwa – Hapana
Mhe. John John Mnyika – Hapana
Mhe. James Francis Mbatia – Hapana

Mhe. Ezekiah Dibogo Wenje – Hapana
Mhe. Tundu Antiphas Mughwai – Hapana
Mhe. Felix Francis Mkosamali – Hapana
Mhe. Magdalena Hamis Sakaya – Hakuwepo
Mhe. Moses Joseph Machali – Hapana
Mhe. Godbless Jonathan Lema – Hakuwepo
Mhe. Halima James Mdee – Hapana
Mhe. Rose Kamili Sukum - Hapana
Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa - Hapana
Mhe. Joseph Roman Selasini – Hapana
Mhe. Masoud Abdallah Salim - Hakuwepo
Mhe. Suzan Anselm Jerome Lyimo - Hapana
Mhe. Dkt. Antony Gervas Mbassa - Hapana
Mhe. David Zacharia Kafulila – Hapana
Mhe. Eng. Mohamed Habib Juma Mnyaa – Hakuwepo
Mhe. Salum Khalfan Barwany – Hakuwepo
Mhe. Cecilia Daniel Paresso – Hapana
Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi – Hapana
Mhe. Asaa Othman Hamad – Hapana
Mhe. Raya Ibrahim Khamis – Hapana
Mhe. Christina Lissu Mughwai – Hapana
Mhe. Haroub Muhammed Shamis – Hapana
Mhe. Khatib Said Haji – Hapana
Mhe. Mkiwa Adam Kimwanga – Hakuwepo
Mhe. Rukia Kassim Ahmed – Hapana
Mhe. Joshua Samwel Nasari – Hakuwepo
Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza – Hapana
Mhe. Lucy Fidelis Owenya – Hapana
Mhe. Sabreena Hamza Sungura – Hapana
Mhe. Mwanamrisho Taratibu Abama – Hapana
Mhe. Maida Hamad Abdalla – Ndiyo
Mhe. Rashid Ali Abdallah – Hakuwepo
Mhe. Munde Tambwe Abdallah – Ndiyo
Mhe. Bahati Ali Abeir – Ndiyo
Mhe. Abdul-Azizi Mohamed Abood – Ndiyo
Mhe. Chiku Aflah Abwao – Hapana
Mhe. Khalfan Hilaly Aeshi – Ndiyo
Mhe. Lameck Okambo Airo – Hakuwepo
Mhe. Mustapha Boay Akunaay – Hapana
Mhe. Abdalla Haji Ali – Hapana
Mhe. Juma Othman Ali – Ndiyo
Mhe. Mbarouk Salim Ali – Hapana
Mhe. Sara Msafiri Ally – Ndiyo
Mhe. Hussein Nassor Amar – Ndiyo
Mhe. Kheri Khatib Ameir – Ndiyo
Mhe. Abdallah Sharia Ameir – Ndiyo
Mhe. Abdulsalaam Selemani Amer – Ndiyo
Mhe. Amina Abdallah Amour – Hakuwepo
Mhe. Said Amour Arfi – Ndiyo
Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Hakuwepo
Mhe. Iddi Mohamed Azzan – Ndiyo
Mhe. Mussa Zungu Azzan – Ndiyo

Mhe. Omary Ahmad Badwel – Hakuwepo
Mhe. Faida Mohammed Bakar – Ndiyo
Mhe. Elizabeth Nkunda Batenga – Ndiyo
Mhe. Gosbert Begumisa Blandes – Ndiyo
Mhe. Lolesia Jeremiah Maselle Bukwimba – Ndiyo
Mhe. Ester Amos Bulaya – Ndiyo
Mhe. Selemani Said Bungara – Hakuwepo
Mhe. Felister Aloyce Bura – Ndiyo
Mhe. Agripina Zaituni Buyogera – Hapana
Mhe. Jerome Dismas Bwanausi – Ndiyo
Mhe. Josephine Tabitha Chagula – Ndiyo
Mhe. Kisyeri Werema Chambiri – Ndiyo
Mhe. Dkt. Cyril August Chami – Ndiyo
Mhe. Mary Pius Chatanda – Ndiyo
Mhe. John Momose Cheyo – Ndiyo
Mhe. Hezekiah Ndahani Chibulunje – Ndiyo
Mhe. Capt. John Zefania Chiligati – Ndiyo
Mhe. Diana Mkumbo Chilolo – Ndiyo
Mhe. Muhammad Amour Chomboh – Ndiyo
Mhe. Amina Andrew Clement – Ndiyo
Mhe. Dkt. Maua Abeid Daftari – Ndiyo
Mhe. Dkt. David Mathayo David – Ndiyo
Mhe. Mohammed Gulam Dewji – Ndiyo
Mhe. Deo Haule Filikunjombe – Ndiyo
Mhe. Josephine Johnson Genzabuke – Ndiyo
Mhe. Ali Juma Haji – Ndiyo
Mhe. Zahra Ali Hamad – Hakuwepo
Mhe. Hamad Ali Hamad - Hakuwepo
Mhe. Azza Hillal Hamad – Ndiyo
Mhe. Neema Mgaya Hamid – Ndiyo
Mhe. Shawana Bukheti Hassan – Ndiyo
Mhe. Maria Ibeshi Hewa – Ndiyo
Mhe. Mansoor Shanif Hiran – Ndiyo
Mhe. Agness Elias Hokororo – Ndiyo
Mhe. Yusuf Salim Hussein – Hapana
Mhe. Dkt. Terezya Pius Luoga Huvisa – Ndiyo
Mhe. Balozi Seif Ali Idd – Ndiyo
Mhe. Dkt. Christina Gabriel Ishengoma – Ndiyo
Mhe. Yahya Kassim Issa – Ndiyo
Mhe. Waride Bakari Jabu – Ndiyo
Mhe. Jadi Simai Jaddy – Ndiyo
Mhe. Selemani Said Jafo – Hakuwepo
Mhe. Asha Mshimba Jecha – Ndiyo
Mhe. Juma Sururu Juma – Ndiyo
Mhe. Riziki Omar Juma – Hakuwepo
Mhe. Hamoud Abuu Jumaa – Ndiyo
Mhe. Ritta Enespher Kabati – Ndiyo
Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu – Ndiyo
Mhe. Balozi Khamis Juma Suedi Kagasheki – Ndiyo
Mhe. Haji Khatib Kai – Hapana
Mhe. Naomi Amy Mwakyoma Kaihula – Hapana
Mhe. Moshi Selemani Kakoso – Ndiyo

Mhe. Innocent Edward Kalogeris – Ndiyo
Mhe. Vick Paschal Kamata – Ndiyo
Mhe. Josephat Sinkamba Kandege – Ndiyo
Mhe. Prof. Juma Athuman Kapuya – Ndiyo
Mhe. Mariam Reuben Kasembe – Ndiyo
Mhe. Rosweeter Faustin Kasikila – Ndiyo
Mhe. Sylvester Mhoja Kasulumbayi - Hapana
Mhe. Eustus Osler Katagira - Ndiyo
Mhe. Vita Rashid Mfaume Kawawa – Ndiyo
Mhe. Zainab Rashid Kawawa – Ndiyo
Mhe. Gaundence Cassian Kayombo – Hakuwepo
Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa – Hakuwepo
Mhe. Kheir Ali Khamis – Ndiyo
Mhe. Sadifa Juma Khamis – Hakuwepo
Mhe. Yussuf Haji Khamis – Hapana
Mhe. Muhammed Seif Khatib – Ndiyo
Mhe. Aliko Nikusuma Kibona – Ndiyo
Mhe. Mendrad Lutengano Kigola – Ndiyo
Mhe. Dkt. Pudensiana Wilfred Kikwembe – Ndiyo
Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete – Ndiyo
Mhe. Modestus Dickson Kilufi – Ndiyo
Mhe. Rosemary Kasimbi Kirigini – Ndiyo
Mhe. Mariam Nasoro Kisangi – Ndiyo
Mhe. Dunstan Luka Kitandula – Ndiyo
Mhe. Suzan Limbweni Aloyce Kiwanga – Hapana
Mhe. Grace Sindato Kiwelu – Hapana
Mhe. Highness Samson Kiwia – Hapana
Mhe. Silvestry Francis Koka – Ndiyo
Mhe. Capt. John Damiano Komba – Ndiyo
Mhe. Mussa Haji Kombo – Hapana
Mhe. Kombo Khamis Kombo – Hapana
Mhe. Maulidah Anna Valerian Komu – Hapana
Mhe. Al- Shaymaa John Kwegyir – Ndiyo
Mhe. Michael Lekule Laizer – Ndiyo
Mhe. Devotha Mkuwa Likokola – Ndiyo
Mhe. Dkt. Festus Bulugu Limbu – Ndiyo
Mhe. Alphaxard Kangi Ndege Lugola – Ndiyo
Mhe. Riziki Said Lulida – Ndiyo
Mhe. Livingstone Joseph Lusinde – Ndiyo
Mhe. John Paul Lwanji – Ndiyo
Mhe. Slyvester Massele Mabumba – Ndiyo
Mhe. Betty Eliezer Machangu – Ndiyo
Mhe. Salvatory Naluyaga Machemli – Hapana
Mhe. Zarina Shamte Madabida – Ndiyo
Mhe. John Shibuda Magalle – Hakuwepo
Mhe. Catherine Valentine Magige – Ndiyo
Mhe. Ezekiel Magolyo Maige – Ndiyo
Mhe. Faki Haji Makame – Hapana
Mhe. Eng. Ramo Matala Matani – Ndiyo
Mhe. Amina Nassoro Makilagi – Ndiyo
Mhe. AnnaMarystella John Mallac – Hapana
Mhe. Ignas Aloyce Malocha – Ndiyo

Mhe. Dkt. David Mciwa Malole	– Ndiyo
Mhe. Murtaza Ally Mangungu	– Ndiyo
Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya	– Ndiyo
Mhe. Abdul Jabiri Marombwa	- Ndiyo
Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni	– Ndiyo
Mhe. Augustino Manyanda Masele	– Ndiyo
Mhe. Donald Kelvin Max	- Hakuwepo
Mhe. Lucy Thomas Mayenga	– Ndiyo
Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka	– Ndiyo
Mhe. Kuruthum Jumanne Mchuchuli	– Hakuwepo
Mhe. GoodLuck Joseph Ole-Medeye	– Hakuwepo
Mhe. Zakia Hamdani Meghji	– Hakuwepo
Mhe. Mariam Salum Mfaki	– Hakuwepo
Mhe. Athumani Rashid Mfutakamba	– Ndiyo
Mhe. Subira Khamis Mgalu	– Ndiyo
Mhe. Godfrey William Mgimwa	– Ndiyo
Mhe. Zabein Mhaji Mhita	– Ndiyo
Mhe. Esther Lukago Minza Midimu	– Ndiyo
Mhe. Fatuma Abdallah Mikidadi	– Ndiyo
Mhe. Desderius John Mipata	– Ndiyo
Mhe. Mohamed Hamisi Missanga	– Ndiyo
Mhe. Faith Mohamed Mitambo	– Ndiyo
Mhe. Margareth Agnes Mkanga	– Ndiyo
Mhe. Dunstan Daniel Mkapa	– Ndiyo
Mhe. Nimrod Elirehema Mkono	– Ndiyo
Mhe. Mustapha Haidi Mkulo	– Ndiyo
Mhe. Ritta Louise Mlaki	– Hakuwepo
Mhe. Martha Moses Mlata	– Ndiyo
Mhe. Rebecca Michael Mngodo	– Hapana
Mhe. Herbert James Mntangi	– Ndiyo
Mhe. Ally Keissy Mohamed	– Ndiyo
Mhe. Hamad Rashid Mohamed	– Ndiyo
Mhe. Mohammed Said Mohammed	– Ndiyo
Mhe. Dkt. Haji Hussein Mponda	– Ndiyo
Mhe. Dkt. Augustine Lyatonga Mrema	– Ndiyo
Mhe. Maryam Salum Msabaha	– Hapana
Mhe. Assumpter Nshunju Mshama	– Ndiyo
Mhe. Abdul Rajab Mteketa	– Ndiyo
Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu	– Ndiyo
Mhe. Christowaja Gerson Mtinda	– Hapana
Mhe. Philipa Geofrey Mturano	– Hakuwepo
Mhe. Mtutura Abdallah Mtutura	– Ndiyo
Mhe. Thuwayba Idrisa Muhamed	– Hapana
Mhe. Philipo Augustino Mulugo	– Ndiyo
Mhe. Joyce John Mukya	– Hapana
Mhe. Hasnain Mohamed Murji	– Ndiyo
Mhe. Bernadetha Kasabago Mushashu	– Ndiyo
Mhe. Mussa Hassan Mussa	– Ndiyo
Mhe. Eugen Elishilinga Mwaiposa	– Hakuwepo
Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa	– Ndiyo
Mhe. Salome Daudi Mwambu	– Ndiyo
Mhe. Mch. Luckson Ndaga Mwanjale	– Ndiyo

Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa – Hakuwepo
Mhe. Clara Diana Mwatuka – Hapana
Mhe. Amina Mohamed Mwidau – Hakuwepo
Mhe. Charles John Poul Mwijage – Ndiyo
Mhe. Hussein Mussa Mzee – Ndiyo
Mhe. Shamsi Vuai Nahodha – Ndiyo
Mhe. Benedict Ngalama Ole-Nangoro – Ndiyo
Mhe. Yusuph Abdallah Nassir – Ndiyo
Mhe. Dkt. Emmanuel John Nchimbi – Hakuwepo
Mhe. Richard Mganga Ndassa – Ndiyo

(Hapa umeme ulikatika)

MBUNGE FULANI: Bajeti oyee! Bajeti himilivu.

(Hapa Wabunge fulani waliimba CCM, CCM, CCM)

SPIKA: Hebu wengine nyamazeni.

WABUNGE FULANI: Chama Dume!

SPIKA: Mnajua watu wanawasikiliza! Ninyi mnadhani watu hawawajui wanaoongea ni akina nani, mimi nafikiri muwe na adabu mnajulikana.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, wewe si uendelee tu inaongea hii?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: *Microphone* zinafanya kazi kwa nini tusiendelee?

MBUNGE FULANI: *Generator* iko wapi? *(Kicheko)*

WABUNGE FULANI: Hujaikalia?

SPIKA: Ninyi watu wazima muwe na uvumilivu, mambo mengine hayana hata maana.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, tuliambiwa *generator* inawaka baada ya dakika tano.

MBUNGE FULANI: Tumia tochi.

MBUNGE FULANI: Tochi hatuonani.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: *Mike* zinawaka, yule bwana akiwekewa taa tunaendelea.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Watakuwa wanaitika watu wengine, wataitika Siyo wengi. Watafanya vituko humu wewe acha tu. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Profesa Muhongo, nchi nzima giza. *(Kicheko)*

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Wewe acha urongo wako!

MBUNGE FULANI: Profesa Muhongo, nchi nzima giza. *(Kicheko)*

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Wewe acha urongo wako!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Keissy Namanyere hakuna umeme, unajuaje?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa rai, kila atakayeitwa jina, ajipige tochi athibitishe ndiyo tuendelee na zoezi. Ahsante sana. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Mbona *mike* zinawaka?

MBUNGE FULANI: CCM wanaogopa!

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba muwe na utulivu, kwa sababu tatizo hili si la hapa tu, ni katika *system* nzima mpaka ya Mtera huko. Wanachojaribu kufanya ni kushitua baadhi ya *turbines* kusudi angalau Dodoma tuweze kupata umeme. Sasa ni mwendo kama wa dakika 20 hivi, kwa sababu hata mkitoka huko nje ni giza kama ilivyo. Wanasema dakika 20 zijazo wanaweza. Tungependa kufanya hivyo, ngoja tusikilizane; tunachokisema, ukitoka hapa huko nje ni giza kama ilivyo!

MBUNGE FULANI: Mama la leo limalizwe leo, kama nusu saa tupo hapa tutasuburi hakuna tatizo.

SPIKA: Sikilizeni sasa mimi nazungumza, naomba mnisikilize. Shida yangu ni kwamba, hata mkitoka humu kuna giza nje. Kwa hiyo, dakika kama 20, wanajaribu ku-*facilitate generator* moja kwa ajili ya Dodoma. Naomba mvumilie kidogo. Huko nje kuna giza mnaweza kupata matatizo mengine.

MBUNGE FULANI: *Generator* ya Bunge vipi?

SPIKA: Hicho kitu kilichoharibika kimeharibu karibu vitu vyote. Kwa hiyo, msubiri dakika chache.

MBUNGE FULANI: Mama tunasubiri, *aluta continua.*

SPIKA: Tuongee kwa ukimya mliko huku, hizi kelelekelele hazisaidii.

(Hapa umeme ulirudi)

SPIKA: Pigieni kengele huko nje. Sasa hawa walikwenda wapi wakati kulikuwa na giza kila mahali!

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu, pamoja na kwamba ni kitendo kilichokuwa cha dharura, lakini bado Kanuni inataka niongeze muda wa dakika thelathini, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5) ili tumalize kazi iliyobaki, siyo kazi kubwa iliyobaki.

Sasa ninyi mlitaka tupige kura watu hatuwaoni tutapigiwa na Maruhani halafu. *(Kicheko)*

(Hapa upigaji kura uliendelea)

Mhe. Philemon Kiwelu Ndesamburo - Hakuwepo

Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile – Hakuwepo
Mhe. Steven Hilary Ngonyani – Ndiyo
Mhe. Cythia Hilda Ngowi – Ndiyo
Mhe. Ahmed Juma Ngwali – Hapana
Mhe. Juma Abdallah Njwayo – Ndiyo
Mhe. Said Juma Nkumba – Ndiyo
Mhe. Dkt. Lucy Sawere Nkya – Ndiyo
Mhe. Albert Obama Ntabaliba – Ndiyo
Mhe. Deogratias Aloyce Ntukamazina – Ndiyo
Mhe. Omari Rashid Nundu – Ndiyo
Mhe. Abia Muhama Nyabakari – Ndiyo
Mhe. Nyambari Chacha Maliba Nyangwine – Ndiyo
Mhe. Leticia Mageni Nyerere – Hapana
Mhe. Tauhida Cassian Galos Nyimbo – Ndiyo
Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka –
Mhe. Rashid Ali Omar – Hapana
Mhe. Asha Mohamed Omari – Ndiyo
Mhe. Nassib Suleiman Omar – Ndiyo
Mhe. Saleh Ahmed Pamba – Ndiyo
Mhe. Ismail Aden Rage – Ndiyo
Mhe. Rachel Mashishanga Robert – Hapana
Mhe. Mhonga Said Ruhwanya – Hapana
Mhe. Mch. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare – Ndiyo
Mhe. Jasson Samson Rweikiza – Ndiyo
Mhe. Mwanakhamis Kassim Said – Hakuwepo
Mhe. Said Suleiman Said – Hapana
Mhe. Moza Abedi Saidy – Hakuwepo
Mhe. Kidawa Hamid Saleh – Ndiyo
Mhe. Ramadhani Haji Saleh – Ndiyo
Mhe. Ahmed Ali Salum – Ndiyo
Mhe. Deo Kasenyenda Sanga – Ndiyo
Mhe. Muhammad Ibrahim Sanya – Hakuwepo
Mhe. Ali Khamis Seif – Hapana
Mhe. Haji Juma Sereweji - Hakuwepo
Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby – Ndiyo
Mhe. Abdulkarim Esmail Hassan Shah – Hakuwepo
Mhe. Henry Daffa Shekifu – Ndiyo
Mhe. Beatrice Matumbo Shellukindo – Ndiyo
Mhe. Fakharia Khamis Shomar – Ndiyo
Mhe. Namelok Edward Moringe Sokoine – Hakuwepo
Mhe. Jitu Vrajlal Soni - Ndiyo
Mhe. Suleiman Nchambi Suleiman – Hakuwepo
Mhe. Shaffin Ahmedali Sumar – Ndiyo
Mhe. Gregory George Teu – Ndiyo
Mhe. Salim Abdullah Turky – Ndiyo
Mhe. Martha Jachi Umbulla – Ndiyo
Mhe. Zaynabu Matitu Vulu – Ndiyo
Mhe. Anastazia James Wambura – Ndiyo
Mhe. Selemani Jumanne Zedi – Ndiyo
Mhe. Said Mussa Zubeir – Ndiyo
Mhe. Dkt. Faustine Engerbelt Ndugulile – Ndiyo

(Hapa ulipigaji kura ulikamilika)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutajipa muda kidogo ili tuweze kuhesabu. Nategemea mtasaidia huko nyuma. Naomba uvumilivu kwa muda mchache tu kwa sababu namba zenyewe zinaeleweka.

(Hapa kura zilihesabiwa)

SPIKA: Mheshimiwa Prof. Muhongo unaweza kutueleza kimetokea nini kuhusu umeme?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza, nianze kwa kuomba radhi kwa Wabunge kwamba, kwa bahati mbaya umeme umetuzimikia hapa. Nawaomba radhi na Watanzania wote, hiki ni kitu ambacho hakikutegemewa. Ingekuwa siku za nyuma, mwaka mmoja nyuma, tulizowea giza tungefurahia, lakini kwa sababu hatujazowea giza, imekuwa ni jambo la kushitukiza sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge na Watanzania wote, kilichotokea ni kwamba, kwa bahati mbaya, mitambo yote inayofua umeme; umeme wa maji, wa mafuta na wa gesi, tuna aina tatu, imetoka kwa mpigo, kwa pamoja. Sasa siyo eneo langu, mimi siyo *engineer,* lakini maelezo kwa kifupi yanasema kwamba, mtambo mkubwa kama wa Mtera ukitoka ghafla unaweza uka-*affect system* nzima ikawa na athari ya namna hiyo.

Kwa hiyo, *TANESCO* wanasema kwamba, hata wao imewachukua muda, walikuwa hawaelewi hitilafu imetokea wapi. Kila kitu kipo kwa *control* pale Ubungo, ndiyo wanaweza kuangalia *system* nzima ya umeme. Kwa hiyo, walichokifanya ni kurudisha na Gridi kama hii ikitokea, imewahi kutokea lakini siyo mara nyingi na siyo kwa wakati kama huu. Kwa hiyo, wanachofanya ni kurudisha umeme hatua kwa hatua. Walichofanya ni kutumia *standby generator* ya Mtera, kuruhusu uzalishaji wa Mtera uendelee na hapa tuweze kupata umeme na sehemu zingine Dar es salaam wanapata umeme. Kwa hiyo, itachukua labda muda kama nusu saa nchi nzima tena itapata umeme.

Nimewaagiza *TANESCO* wawaombe radhi Watanzania na watoe maelezo. Maelezo hayo *TANESCO* itayatoa jioni hii, ya haraka, lakini tunataka maelezo ya kitaalamu kwa nini imetokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, ndiyo maana tunataka kuboresha miundombinu ni kwamba; ingalikuwa tupo sehemu zingine, nadhani wote mmekaa sehemu ambazo kitu kama hiki kikitokea, mashine zingine zinazi-*switch* kwa haraka ili kutoruhusu giza kuingia.

Sasa kwa kwetu hapa, kwa sababu uwezo wetu wa umeme *installed capacity* ni *megawatt* 1,583, hiyo *system* huiwezi; ndiyo maana tukipata Kinyerezi One ya megawatt 150, Kinyerezi Two ya megawatt 240 na Kinyerezi Three ya *megawatt* 300, tukiwa na *megawatt* kama 500 za ziada, tutaweka *system* ambayo kitu kama hiki kikitokea, basi ile *system* inaweza ikaji-*switch* angalau zikawepo *megawatt* 500 kwa ajili ya umeme. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Watanzania poleni sana, lakini tunaendelea kuboresha miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Wengine walikuwa wanauliza *generator* la kwetu lipo wapi; lipo! Sasa ilipo-*switch* kule nalo lika-*switch off*. Kwa hiyo, mtikisiko ulikuwa mkubwa kiasi kwamba na haya majenereta yetu hapa hayaweza kuhimili mshituko huo. Kwa hiyo, siyo kwamba sisi hatuna majenereta tunayo, lakini yalipata msituko kwa pamoja. Mwanga mdogo tuliokuwa nao ni *generator* dogo la eneo la Utawala ndiyo lilikuwa linaonesha tu njia za kutokea.

Kwa hiyo, mimi nawashukuru kwa uvumilivu wenu, kwa sababu vinginevyo hata mngetaka kutoka mwende huko mitaani mngetokaje? Huwezi kujua nani yupo nyuma yako humwoni. Kwa hiyo, ndiyo maana nawashukuru sana kwa uvumilivu, tumeweza kuimaliza kazi vizuri, matokeo siyo tatizo. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni 68(7); wakati tukipiga kura baadhi ya Wabunge walitamka hapana. Sasa naomba mwongozo wako fedha za maendeleo zitahitajika kweli kwenda kwa maeneo ambayo Bajeti hii wameikataa kwa kusema hapana?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mfutakamba, unajua katika Dunia hata ukishika mkono wako utakuta vidole vingine virefu na vingine vifupi na vingine vifupi sana. Sasa ukisema kile kifupi kisipate mbona ni bure tu ni *democracy* tu iliyopo.

T A A R I F A

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa kuhusu nini umeme?

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, hapana, natoa taarifa kwa mzunguzaji ambaye ametoka kuzungumza. *(Kicheko)*

SPIKA: Taarifa yako naikataa. Mwongozo nilipewa mimi.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, natoa taarifa kwamba, Bajeti ni *policy issue*, ni suala la kisera.

SPIKA: Mheshimiwa usiharibu hali ya hewa, hebu kaa chini tu. Kwa nini unaharibu hali ya hewa? Hii ni *democracy*.

(Hapa matokeo ya kura yalitangazwa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, matokeo yapo kama ifuatavyo:-

Idadi ya Wabunge Kikatiba tunatakiwa kuwa 357 kama tungekuwa *Full House*. Sasa hivi kwa wale ambao wapo ni 355, lakini idadi ya Wabunge waliopo na waliopiga kura ni 300. Wabunge ambao hawakuwepo Bungeni hapa wakati tunapiga kura ni 54. Kura ya mtu ambaye alishindwa kuamua hakuna. Waliosema Hapana ni 66 na waliosema Ndiyo ni 234. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2014/2015 imepita kwa wingi wa kura. *(Makofi)*

(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 yalipitishwa na Bunge)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014 *(The Appropriation Bill, 2014)*

(Kusomwa Mara ya Kwanza)
THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BILL SUPPLEMENT

No. 1 *20th June, 2014*

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 25 Vol 93 dated 20th June, 2014

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

THE APPROPRIATION ACT, 2014

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Section *Title*

1. Short title.
2. Interpretation.
3. Issue of Shs.19,853,331,000,000 out of Consolidated Fund.
4. Appropriation of moneys voted.
5. Power of the Minister to borrow.
6. Power of the Minister to reallocate certain appropriated money.

SCHEDULE

NOTICE

The following Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam
23rd June, 2014

OMBENI Y. SEFUE
Secretary to the Cabinet

A BILL
for

An Act to apply a sum of Nineteen Trillion, Eight Hundred Fifty Three Billion, Three Hundred Thirty One Million Shillings out of the Consolidated Fund to the Service of the year ending on the thirtieth day of June, 2015, to appropriate the supply granted for that year, to authorize the reallocation of certain appropriations and to provide for matters connected with those purposes.

ENACTED by the Parliament of the United Republic of Tanzania.

1. This Act may be cited as the Appropriation Act, 2014.

2. The expressions used in this Act shall each have the meaning ascribed to it in the Public Finance Act.

3. The Treasury may issue out of the Consolidated Fund and apply towards the supply granted for the service of the year ending on the thirtieth day of June, 2015, the sum of Nineteen Trillion, Eight Hundred Fifty Three Billion, Three Hundred Thirty One Million Shillings.

4. The sum granted by section 3 shall be appropriated to the purposes and in the amounts specified in the second, third, fourth and fifth columns respectively of the Schedule to this Act.

5.-(1) The Minister may, at any time or times not later than the thirtieth day of June, 2015, borrow within or outside the United Republic or partly within and partly outside the United Republic, any sum or sums not exceeding, in the whole, the sum of Nineteen Trillion, Eight Hundred Fifty Three Billion, Three Hundred Thirty One Million Shillings, by way of loan, advance, the issue of bills or bank overdraft and on such terms and conditions as the Minister may deem expedient, and may charge that loan or advance on any of the assets of the United Republic, including securities forming part of the Consolidated Fund. (2) Any money borrowed under this section shall be placed to the credit of the exchequer account and shall form part of the Consolidated Fund, and be available in any manner in which that Fund is available.

(3) Any money borrowed under this section shall be subject to repayment not later than the thirty-first day of October, 2015, and any sum required for the repayment of any money so borrowed, and of any interest payable in respect of that money shall be charged on and paid out of the Consolidated Fund.

(4) The powers conferred upon the Minister by this section shall be in addition to the powers of the Minister under the Government Loans, Guarantees and Grants Act.

6. -(1) Where the Minister is satisfied that it is necessary in the public interest that provision be made for defraying the expenditure of any Region, Ministry or Department of the Government in excess of any sum voted for it or for any service for which no sum

is voted, and that it would be detrimental to the public interest to postpone the expenditure until provision can be made for it by the National Assembly, he may notwithstanding any provision to the contrary in this Act or any other written law, authorize the application of any surplus arising out of savings in the Consolidated Fund or any vote in the Schedule to this Act (other than votes for pensions, gratuities or other retirement benefits, or for widow's and orphans' pension) for or towards the excess or service.

(2) Where the Minister authorizes the application of any surplus under this section, he shall cause to be laid before the National Assembly, not later than at the meeting next after the date of the authorization, a supplementary estimates Bill or Statement of reallocation, as the case may be, in accordance with the provisions of the Constitution.

(3) The Minister may delegate all or any of the powers conferred upon him by this section to any public officer subject to such limitations as the Minister may specify.

(4) The provisions of section 22 of the Public Finance Act, shall not apply to the powers conferred upon the Minister by this section.

(5) The Minister may, by certificate under his hand, reallocate any sums arising from savings in the Consolidated Fund to any of the purposes specified in the second, third, and fourth columns respectively of the Schedule to this Act, and where this occurs, the provisions of section 3 and 4 shall take effect as if the total sum granted out of the Consolidated Fund and the amounts appropriated for the purpose specified in such certificate were raised by the amount or amounts specified in the certificate.

SCHEDULE

(*Made under section 4*)

_____

OBJECTS AND REASONS

_____

The object of this Bill is to apply the sum of Shillings **19,853,331,000,000** out of the Consolidated Fund to the Service of the Financial Year 2014/2015.

_____

MADHUMUNI NA SABABU

_____

Madhumuni ya Muswada huu ni kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ya jumla ya Shilingi **19,853,331,000,000**.

Dar es Salaam
23rd June, 2014

SAADA MKUYA SALUM,
Minister for Finance

Muswada wa Sheria ya kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014 *(The Appropriation Bill, 2014)*

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya shilingi Trilioni Kumi na Tisa, Bilioni Mia Nane Hamsini na Tatu, Milioni Mia Tatu Thelathini na Moja kwa Matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa Mwaka Unaoishia Tarehe Thelathini Juni, Elfu Mbili na Kumi na Tano, kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa Mwaka huo, kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo *(A Bill for an Act to Apply, a Sum of Nineteen Trillion, Eight Hundred Fifty Three Billion, Three Hundred Thirty One Million Shillings out of Consolidated Fund to the Service of the Year ending on the Thirtieth day of June, 2015 to appropriate the Supply granted for that year, to authorize the reallocation of certain appropriations and to provide for matters connected with those purposes)*.

(Muswada Uliotajwa Hapo Juu Ulisomwa Bungeni Kwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014 *(The Appropriation Bill, 2014)*

(Kusomwa Mara ya Pili)

(Muswada wa Sheria ya Serikali uliotajwa hapo juu Ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Pili)

Muswada wa Sheria ya kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014 *(The Appropriation Bill, 2014)*

(Kusomwa mara ya tatu)

(Muswada sheriaya Serikali Uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge ni kama tumefunga sasa shughuli yetu ya Bajeti. Tumefunga kwamba, pamoja na ajenda mlizopewa zile ndiyo sasa Bajeti ya Serikali. Sasa kazi

ambayo tunatakiwa kuifanya kuanzia kesho ni kupitisha Sheria ya Fedha. Hii tuliyomaliza ni Sheria ya Matumizi, ya kesho ni Sheria ya Fedha.

Kwa hiyo, Sheria ya Fedha kama mtakavyoona kifungu chetu, kwa wale wanaopeleka *amendment* tulisema wanatakiwa wapeleke kwenye Kamati kusudi waweze kujadiliana. Kutokana na kazi zilizokuwa nyingi katika kipindi kimoja hiki ile *Finance Bill* haiko tayari.

Kwa hiyo, kesho asubuhi tutakuwa na kipindi cha maswali, baada ya maswali tutaahirisha mpaka saa kumi na moja ili Azimio la Afrika Mashariki liweze kuingia sasa kumi na moja kesho jioni. Wakati huo siku nzima ya kesho, Wizara ya Fedha, Kamati ya Bajeti na wengine ambao watakuwa wamepeleka *ammendments*, wataendelea kujadiliana kuhusiana na *Finance Bill* ambayo inatakiwa ifanyike.

Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa uvumilivu wenu wa hali ya juu sana, tumeweza kufikia hapa na tunavyojadiliana vizuri hata kama una mawazo huyapendi lakini yanajenga. Kwa hiyo, katika kuzungumza ndiyo tunavyopata akili zaidi kuliko kila mtu angekubali vilevile. Kwa hiyo, mimi nawapongezeni wote kabisa mmefanya kazi vizuri na Mawaziri wetu nawapongeza sana, pamoja ugeni wao katika eneo hilo, kazi kubwa wamefanya. Haya mliyosema hapa sisi tutawafuatilia, tusingependa mpate aibu mwaka mwingine, maana mmesema maneno mazito sana hapa na mkayatende vile mlivyoyasema. *(Makofi)*

Naamini Watanzania watakuwa pamoja na ninyi, mradi ninyi wenyewe msibadilike. Kodi ni kodi tu, kama kesho mtapitisha Sheria ya Kodi maana yake ni Sheria, hakuna namna nyingine yoyote ile. Kwa hiyo, mimi niwashukuru sana wote na Wataalamu wetu tunawashukuru sana hapo mlipofikia. Mmemaliza kazi na kwenye *Finance Bill* napo mshirikiane, msiposhirikiana nako kutaleta matatizo. *(Makofi)*

Mimi naishukuru sana Kamati yangu ya Bajeti, kwa sababu hata mseme vipi, wanafanya kazi usiku. Kama sasa hivi kuna Miswada mingi tu na nawashukuru Wenyeviti wa Kamati nyingine na ninyi pia mkamilishe, kusudi timu nzima ikae ipitie hii Miswada ambayo itakuja wiki inayoanzia kesho ili tuweze kuwa na kitu kizuri ambacho kitarudisha nidhamu ya Bajeti katika nchi yetu ambayo inahitajika sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 2.20 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 25 Juni, 2014 Saa Tatu Asubuhi)